

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI  
ZANZIBAR**

Mhe. Pandu Ameir Kificho	- SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa

- 10.Mhe. Juma Duni Haji -MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
- 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed -MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
- 12.Mhe. Abdilllah Jihad Hassan -MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
- 13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna -MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
- 14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid -MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
- 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui -MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
- 16.Mhe. Said Ali Mbarouk -MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
- 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman -MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
- 18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga -MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali -MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
- 20.Mhe. Machano Othman Said -MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni

- |                                    |  |
|------------------------------------|--|
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman       | - Mwanasheria Mkuu   |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi             | -Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka              |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad            | - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake           |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya      | -Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais                                  |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis       | - Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame        | -Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi         |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | -Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni              |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla       | - Jimbo la Chonga  |
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali          | - Jimbo la Mkoani  |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo            | - Jimbo la Matemwe   |
| 31. Mhe. Ali Mzee Ali              | - Kuteuliwa na Rais  |
| 32.Mhe. Ali Abdalla Ali            | - Jimbo la Mfenesini   |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji            | - Jimbo la Kwahani   |
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk         | - Nafasi za Wanawake   |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad         | - Jimbo la Wete  |

- 36.Mhe. Asha Abdu Haji - Nafasi za Wanawake
- 37.Mhe. Asha Bakari Makame - Nafasi za Wanawake
- 38.Mhe. Ashura Sharif Ali - Nafasi za Wanawake
- 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Nafasi za Wanawake
- 40.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake
- 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani
- 42.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura
- 43.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani
- 44.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani
- 45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe
- 46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni
- 47.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake
- 48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni
- 49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope
- 50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni
- 51.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake
- 52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini
- 53.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile
- 54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani
- 55.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

- 57.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini
- 59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
- 60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake
- 61.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo
- 62.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake
- 63.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
- 64.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani
- 65.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake
- 66.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbwe
- 67.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi
- 68.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe
- 69.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake
- 70.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake
- 71.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni
- 72.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu
- 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
- 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole
- 76.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni
- 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

- 78.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani
- 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
- 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
- Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

## **Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 23 Julai, 2011**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

### **DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

### **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto Zanzibar mwaka 2011. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto Zanzibar mwaka 2011. naomba kuwasilisha.

### **KAULI ZA MAWAZIRI**

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wazima wa afya.

Pili Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Ali Mzee Ali kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, nina hakika mchango wake utasaidia sana katika Serikal hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, leo ni siku adhimu kwetu sote ya kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, ambapo kila mwaka ifikapo tarehe 16 Juni nchi za Afrika huadhimisha siku hii kwa kutathmini utekelezaji wa mkataba wa haki na ustawi wa mtoto wa Afrika ulioridhiwa mwaka 2003.

Mhe. Spika, Umoja wa Afrika ulitoa tamko rasmi tarehe 16 Juni, 1976 baada ya mauaji ya watoto yaliyotokea huko Soweto, Afrika ya Kusini. Watoto hao waliouwawa kikatili walikuwa wakiandamana kwa madhumuni ya kupinga kutumia lugha ya kikaburu katika skuli na kutaka kupatiwa elimu bila ya malipo pamoja na kudai haki zao za kibinadamu.

Mhe. Spika, mwaka huu ni mwaka wa 21 wa maadhimisho haya ambapo ujumbe ni “*Sote kwa pamoja tuchukue hatua za haraka, kunusuru na kuondosha watoto wa mitaani*”

Mhe. Spika, tukisema watoto wa mitaani tuna maana watoto wanaoishi na kuzurura mitaani, hawa ni watoto wanaotoka katika familia zao na kufanya biashara ndogo ndogo au wanaojihusisha na mambo yasiofaa ambayo ni hatari kwa maisha yao.

Mhe Spika, watoto wa mitaani wanahitaji kushughulikiwa ili taifa liwe imara. Taarifa tulizonazo watoto wapatao milioni mia moja na ishirini (120 mil) hivi sasa ulimwenguni wanaishi mitaani, ambapo kati ya hao milioni thelathini (30) wamo barani Afrika. Hapa Zanzibar tatizo la watoto wa mitaani limeanza kujitokeza sababu kubwa zinazojitokeza ni kwamba wazazi au walezi wameshindwa kusimamia na kutekeleza wajibu wao wa kuwatumia vizuri watoto, upande mwingine sababu ya hali ngumu ya maisha pia husababisha watoto kukimbia nyumbani na kuingia mitaani kwa lengo la kutafuta riziki.

Mhe. Spika, pamoja na ujumbe huu naomba kutoa tathmini ya utekelezaji wa haki na ustawi wa mtoto kwa mwaka 2010/2011

Mhe. Spika, katika taarifa ambayo tumeisambaza kwenu tumezingatia maeneo manne (4) ya utekelezaji wa haki za watoto ambazo ni: **Haki ya kuishi** inayojumuisha masuala ya afya, lishe, kinga na tiba dhidi ya maradhi yanayowakumba watoto, **Haki ya kuendelezwa** inayojumuisha masuala ya malezi, elimu na utamaduni, **Haki ya kulindwa** kisheria dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na ukatili na **Haki ya kushiriki na kushirikishwa** katika masuala ya kijamii.

Mhe. Spika, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto iliandaa sheria ya watoto, sheria ambayo imepitishwa kwenye Baraza lako tukufu Mwezi Machi, 2011. Msingi mkuu wa sheria hiyo ni kuanzisha utaratibu wa mfumo wa ulinzi wa mtoto na kushughulikia masuala ya haki na ustawi wa watoto.

Mhe. Spika, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mashirikiano na shirika la *SAVE THE CHILDREN* imeanzisha kituo maalumu kitiwacho Mkono kwa Mkono, (*One Stop Centre*) katika Hospitali ya Mnazimmoja. Lengo la kituo hiki ni kuwaweka watu wote muhimu wa kushughulikia matukio ya udhalilishwaji wa watoto, ambapo wataalamu wenye fani ya udaktari, polisi, waendesha mashtaka na washauri nasaha, watatoa huduma zinazohitajika kwa waathirika wa vitendo vya



udhalilishwaji na kutunza ushahidi kwa madhumuni ya kuchukuliwa hatua za kisheria kwa wale wadhhalilishaji. Aidha, kituo kitafanya kazi kwa saa ishirini na nne (24). Kituo kama hiki kinatarajiwa kuanzishwa Pemba katika Hospitali ya Chake Chake hivi karibuni.

Mhe. Spika, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imeanzisha daftari maalum (*Register*) la kukusanya na kutunza kumbukumbu za matukio ya udhalilishwaji wa watoto Zanzibar kupitia ngazi za Shehia ili kuiwezesha serikali kujua ukubwa wa tatizo na kupanga mikakati endelevu ya kupunguza na hatimae kuondoa tatizo hilo linaloikabili jamii yetu. Ili kufanikisha suala hilo, wizara imewapatia mafunzo ya ujazaji na utunzaji wa daftari hilo maafisa wa ustawi wa jamii, wanawake na watoto, polisi, madaktari, masheha, wawakilishi wa mabaraza ya watoto na waratibu wa shughuli za wanawake na watoto wa shehia za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, matukio ya udhalilishwaji wa watoto yaliyoripotiwa katika Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja ni 150 na Pemba 189 yakijumuisha kubakwa, kulawitiwa, mimba za utotoni, kukosa huduma za matunzo na mvutano wa malezi, ambapo huduma za ushauri nasaha hutolewa na kwa yale yanayostahiki kwenda Mahakamani huwashauri wahusika wafungue kesi Mahakamani. Matukio mengine kama haya yameripotiwa katika Jumuiya ya Wanasheria Wanawake, (*ZAFELA*) kwa ajili ya kupewa ushauri wa kisheria ni 99.

Mhe. Spika, serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii inatoa huduma ya malezi na matunzo kwa watoto yatima na wale ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalea kutokana na matatizo ya kiuchumi na kijamii. Idara imewapatia mahitaji yote muhimu ya msingi watoto 47 (wanawake 25 na wanaume 22) wanaolewa katika nyumba ya watoto yatima Mazizini. Mahitaji hayo hujumuisha chakula, malazi na elimu. Watoto hao wamefunguliwa akaunti katika Benki ya Watu wa Zanzibar ambapo kila mtoto huwekewa jumla ya shilingi 7,000/- kwa mwezi. Aidha, kituo cha kulea watoto cha *SOS* kina jumla ya watoto 104 ambapo kati yao wanawake ni 39 na wanaume ni 65. Katika kituo hicho watoto watoto hupatiwa huduma zote muhimu zikiwemo malazi, chakula, nguo, elimu na huduma za matunzo kwa jumla.

Mhe. Spika, Idara ya Ustawi pia inatoa msaada wa shilingi 15,000/=, kwa ajili ya maziwa kwa mama wanaojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mimba moja na wote wakiwa hai. Idadi ya kinamama waliopatiwa msaada huo ni 12 kutoka katika wilaya za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Idara ya Ustawi wa jamii kwa kushirikiana na *UNICEF* na *TUNAJALI PROGRAM* imefanya zoezi la utambuzi wa watoto wanaoishi

katika mazingira magumu zaidi wakiwemo yatima, watoto wanaojilea, watoto wenye magonjwa sugu, mimba za utotoni, wanaojiingiza katika ajira mbaya, wanaolelewa na walezi wakongwe wasiojiweza na wenye maradhi sugu katika shehia 21 za Unguja na Pemba. Jumla ya watoto 4,237 walitambuliwa kwa lengo la kujua matatizo yao na kisha kupanga mipango endelevu ya kuwasaidia watoto hao.

Mhe. Spika, katika kuwashirikisha watoto ili kuwajengea uwezo wa kutambua haki na wajibu wao, wizara kwa kushirikiana na jumuiya isiyokuwa ya kiserikali ZACA imeongeza mabaraza ya watoto 30 na kufanya idadi ya mabaraza hayo kuwa 130 Unguja na Pemba. Mabaraza haya yanawapa fursa watoto kukaa pamoja na kubadilishana mawazo juu ya mambo yanayowahusu na kuwajenga kimaadili. Wizara katika kuhakikisha kuwa watoto wanashiriki na kushirikishwa katika mambo yanayowahusu, imewashirikisha watoto katika uandishi wa ripoti hii ambapo waliweza kueleza shughuli walizofanya katika kusimamia haki na wajibu wa watoto katika maeneo yao.

Mhe. Spika, huduma za chanjo za mama na watoto zimeendelea kutolewa katika vituo 145 vya serikali na katika vituo binafsi vyenye huduma za afya ya uzazi, huduma hizi zimesaidia sana kupunguza vifo vya mama watoto vinavyotokana na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo kwa mfano, kifua kikuu, kifaduro, dondakoo, pepopunda, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo, kichomi, polio, na surua .

Mhe Spika, katika kipindi hiki jumla ya wagonjwa 35 wenye dalili za surua, wagonjwa 4 wa pepopunda ya watoto wachanga na wagonjwa 6 wa kupooza ghafla waliripotiwa na kuendelea na matibabu ya kawaida.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuwakinga mama wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano Wizara ya afya imegawa jumla ya vyandarua 45,000 kati ya hivyo 30,000 vimegawiwa kwa mama wajawazito kupitia kiliniki zao. Unguja wamepata 19,276 na Pemba 10,724. Vyandarua 15,000 viligawiwa kwa wananchi wa Wilaya ya Mjini ambapo Shehia 17 zilipata vyandarua, 2 kwa kila familia.

Mhe. Spika, katika kudhibiti maradhi yanayowapata watoto, jumla ya wafanyakazi 40 (20 Unguja na 20 Pemba) wakiwemo madaktari wasaidizi “*Clinical Officer*”, madaktari “*Assistant Medical Officer*” na wauguzi walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya muongozo mpya wa udhibiti wa maradhi ya watoto “*Integrated Management of Childhood Illness – IMCI*” ili kuweza kudhibiti na kupunguza magonjwa yanayowapata hasa watoto. Aidha, jumla ya wafanyakazi 40 wa afya walipatiwa mafunzo maalum ya kuokoa

maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua (*Life Saving Skills*) katika utekelezaji wa Mkakati wa kupunguza vifo vya Akina mama na watoto (*Road Map to Accelerate Reduction of Maternal Child Mortality*), ili waweze kufanya kazi katika vituo vya afya vinavyotoa huduma za uzazi.

Mhe. Spika, huduma za kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (*PMTCT Services*) zimetolewa katika vituo 39 vya kliniki za mama wajawazito. Jumla ya mama wajawazito 134 wenye VVU walijifungulia hospitali. Katika kipindi cha Januari –Machi 2011 tathmini ya vituo vya afya vipya 21 (Unguja 13 na Pemba 8) ilifanyika kwa ajili ya utowaji wa huduma hizo. Vituo 10 kati ya hivyo 21 tayari vimeshaanza kutoa huduma. Hii inafanya kuwa na jumla ya idadi ya vituo kufikia 49 vinavyotoa huduma hizi kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, huduma rafiki kwa vijana zimetolewa kwa nia ya kuwalenga watoto na vijana walio na umri kati ya miaka 10 mpaka 24. Huduma hizi zinatolewa katika vituo 20 (10 Unguja 10 Pemba). Lengo la kutoa huduma hizi ni kuwawezesha vijana kupata elimu juu ya masuala ya afya ya uzazi, kujikinga na mimba katika umri mdogo, kujikinga na maambukizi ya VVU na magonjwa mengine ya zinaa.

Mhe. Spika, jumla televisheni 5 zilinunuliwa, kati ya hizo 4 zilisambazwa katika vituo vya Muembeladu, M/Mmoja, Fuoni, Kitengo cha Afya ya Uzazi (*RCH*). DVD 10 zimesambazwa katika vituo vinavyotoa huduma rafiki kwa madhumuni ya kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana, 5 Unguja (M/Mmoja, Muembeladu, JKU, Chumbuni na Fuoni) na 5 Pemba (Vitongoji, Wesha, Micheweni, Mkoani na Konde)

Mhe. Spika, maji ni muhimu sana katika ukuaji, hifadhi na maendeleo ya mama na mtoto. Jukumu la upatikanaji wa maji safi na salama lipo chini ya Mamlaka ya Maji ambayo ndio yenye dhamana ya kuhakikisha huduma hiyo inapatikana kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba. Mwaka 2010/2011 Mamlaka ya Maji imetekeleza miradi 6 ya Maji kwa kushirikiana na *TASAF*, *ACCRA* na *JP5* yenye lengo la kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la maji nchini.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali idadi ya wanafunzi katika skuli za maandalizi imefikia 6,876 kwa skuli za serikali ambapo wanafunzi wa kiume ni 3,376 na wa kike ni 3,500. Kwa upande wa skuli za binafsi jumla ya wanafunzi ni 26,724 ambapo wa kiume ni 12,857 na wakike ni 13,867.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina kitengo maalum kwa elimu mjumuisho ili kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa inawafikia watoto wote wakiwemo wenye ulemavu. Kwa kufanikisha hili mwaka 2009/2010 walimu 2,390, wakiwemo wanaume 808 na wanawake 1,582 walipatiwa mafunzo ya lugha ya (*Braille*) Alama za herufi nundu. Aidha, katika mwaka huo huo 2009/2010, walimu 51 wamejiunga na mafunzo hayo ngazi ya cheti katika Chuo cha Kiisilam Mazizini isitoshe walimu wengine 8 wamejiunga na mafunzo kama hayo katika ngazi ya stahhada na shahada katika vyuo vya Tanzania Bara na Uganda.

Mhe. Spika, Umoja wa Watu wenye Ulemavu, katika kuhakikisha kwamba haki za watoto wenye ulemavu zinaimarishwa, waliwatembelea watoto hao kwa lengo la kuwafanyia uchunguzi na kujua mahitaji yao. Ambapo jumla ya watoto 614 walitembelewa (315 kutoka Unguja na 299 kutoka Pemba) kati ya hao wanawake ni 357 na wanaume 257. Watoto 60 kati yao (wanawake 48 na wanaume 12) walipatiwa huduma zinazolingana na mahitaji yao.

Mhe. Spika, vyombo vya habari vimeshiriki kikamilifu katika kuelimisha jamii kwa kuwahusisha watoto wenyewe kwenye programu na vipindi vipatavyo 344 ikijumuisha maigizo, mijadala inayohusu haki na wajibu wao, kuchangia kwa kutoa maoni juu ya sheria ya watoto na uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 ambapo waliwahoji wagombea na kuwataka watekeleze wajibu wao endapo watachaguliwa na walitoa ujumbe usemao “tuwape nafasi viongozi wanaojali watoto kwa kutetea haki zao,”

Mhe. Spika, wizara inaunga mkono suala la kuwa na siku ya Mtoto wa Afrika ili tuweze kujitathmini na kujiwekea malengo kwa ajili ya kuwahifadhi na kuwaendeleza watoto. Nakuombeni Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa pamoja tushirikiane katika kuwalea na kuwajengea uwezo watoto wetu ili tuwe na taifa bora la baadae.

Ahsanteni sana Mhe. Spika, kwa kunisikiliza.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa katika hali ya uzima na afya na kuweza kuendelea kutekeleza wajibu na majukumu ya Baraza lako tukufu kwa niaba na kwa ajili ya maendeleo ya wazanzibar wote.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuungana na wizara yetu muhimu inayosimamia mambo yote yanayohusu ustawi wa watu wetu, Maendeleo ya

Wanawake na Watoto kwa kutoa maoni ya kamati juu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Mhe. Spika, Siku ya Mtoto wa Afrika ni siku muhimu katika kushajihisha jamii ya Waafrika hususan Zanzibar katika kuhakikisha kuwa haki za watoto zinalindwa na kusimamiwa ipasavyo. Ni siku ya kumbukumbu ya mauwaji ya watoto katika harakati za kupinga ubaguzi dhidi ya kupatiwa haki zao nchini Afrika ya Kusini 1976. Mwaka 1991 Umoja wa Afrika uliona umuhimu wa kuwepo kwa siku hii. Kielelezo cha umuhimu huo kinatokana na historia hiyo katika maendeleo ya kudai haki za watoto katika ngazi ya Kimataifa na Kitaifa.

Mhe. Spika, watoto wengi katika nchi za Afrika bado wanakabiliwa na matatizo mbali mbali ikiwemo kutopatiwa huduma hizo bora ambapo pamoja na mambo mengine hali hiyo hutokana na hali ya umasikini unaozikabili nchi nyingi za Afrika.

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaipongeza sana wizara kwa hatua iliyofikia katika kuratibu na kusimamia shughuli zote za utekelezaji wa haki, wajibu na maendeleo ya watoto Zanzibar.

Kamati yangu inaisisitiza jamii wakati huu kutafakari njia bora na zenye manufaa katika kumlinda mtoto pamoja na kumpatia yale yote muhimu anayostahili ikiwemo elimu, huduma za afya, chakula pamoja na matunzo bora kwa ujumla.

Mhe. Spika, taarifa za afya zinaeleza kuwa, vifo vya watoto wachanga na watoto chini ya miaka mitano vimepungua kwa kiasi kikubwa hata hivyo, vifo vitokanavyo na uzazi bado ni tatizo kwa kinamama wajawazito Zanzibar. Kamati inaisisitiza Wizara ya Afya kuendelea kuielimisha jamii umuhimu wa chanjo, kinga dhidi ya malaria, utoaji wa vitamin 'A' na dawa za minyoo, kinga dhidi ya ukimwi pamoja na huduma za afya ya uzazi.

Kamati ya Ustawi wa Jamii inaipongeza juhudi za serikali katika utekelezaji wa kuwaendeleza watoto kielimu. Jumla ya watoto 36,875 wameweza kuandikishwa na kupatiwa nafasi ya kuanza masomo ya darasa la kwanza. Tunaiomba wizara husika iendelee kuimarisha juhudi za kuwapatia elimu watoto wetu. Miongoni mwa changamoto inazozikabili sekta ya elimu ni pamoja na watoto wenye mahitaji maalum bado huandikishwa kwa kiwango kidogo, kukatisha masomo watoto kutokana na utoro na ndoa za mapema kunakosababishwa na hali duni ya maisha pamoja na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto wa kike na wa kiume.

Mhe.Spika, hivi sasa kumejitokeza matukio ya kutisha na kusikitisha dhidi ya watoto hapa Zanzibar. Watoto waliowengi wanaendelea kuathirika kutokana na kukosa usalama, kutendewa ukatili, kukandamizwa, kunyanyapaliwa, kubaguliwa na hata kutelekezwa. Tujiulize je! Kulikoni? Sheria zipo, zinafanyiwa mapitio siku hadi siku,Vyombo vya Sheria vipo, serikali ipo, lakini iweje matukio hayo dhidi ya watoto wetu yanazidi kuendelea kushamiri siku hadi siku?

Mhe. Spika , taarifa mbali mbali zimekuwa zikitolewa kupitia vyombo vya habari kwa jamii juu ya ongezeko la matukio ya ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto wetu pamoja na ripoti zinazothibitisha matukio hayo. La kusikitisha ni kuona watuhumiwa wanavyotiwa hatiani na baada ya siku kadhaa huonekana mitaani na kurejea kuwadhaliisha watoto wetu.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaiomba serikali kuwasilisha ripoti rasmi ya Kamati iliyoundwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Moh'd Shein kufuatilia masuala ya udhalilishaji wa watoto mbele ya Baraza lako tukufu ili baraza liweze kuelewa kiini cha matatizo hayo na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Spika, pili kamati yangu inaishauri wizara husika kusambaza taarifa mbali mbali za udhalilishaji wa watoto kwa wadau wengi wakiwemo Wajumbe wa Baraza la wawakilishi ili kila mmoja wetu aweze kuanza kuchukua hatua pale alipo badala ya kuziachia pekee familia za waathirika na matukio haya yanapotokea.

Mhe. Spika, tatizo la ajira mbaya kwawatoto pia bado ni sugu hapa Zanzibar. Tafiti ndogo zilizofanywa zimeyataja baadhi ya maeneo ambayo huendeshwa ajira hizo yakiwemo Soko la Mwanakwerekwe, Bandari ya Malindi na Chumbuni, kwa upande wa Unguja na Wilaya ya Micheweni Pemba. Tatizo hili limeelezwa kuwa limekosa msukumo na kupata mafanikio kutokana na wazee wenyewe wengi wao kutoona umuhimu wa kuhakikisha watoto wanapata elimu ya lazima. Mhe. Spika ni lazima tukubali kwamba suala la ajira mbaya kwa watoto ni tatizo kubwa la kila taifa, hivyo hatuana budi sote tuungane na kupiga vita tatizo hilo .

Mhe.Spika, kamati yangu inaipongeza wizara kufikia hatua ya kuanzisha mpango wa kitaifa unaolenga kuwatambua na hatimae kuhakikisha kuwa wanapata haki zao za msingi watoto wetu wanaoishi katika mazingira hatarishi. Mhe. Spika kamati yetu imevutiwa sana na mpango huu ambao hatua zake za awali za utekelezaji zinaleta matumaini. Ni mpango mzuri, ingawa umeonyesha kuwa ni wa gharama kubwa. Hivyo tunaishauri serikali kuunga mkono Mpango

huu ili tuweze kukabiliana na matatizo yanayowakabili watoto wetu ambao ni taifa la kesho.

Mhe.Spika,Kamati ya Ustawi wa Jamii inaikumbusha serikali kuwa bado ina changamoto kubwa katika utekelezaji wa haki ya kulindwa watoto wetu. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa fedha za kuendeshea huduma za kitaifa za watoto.

Mwisho Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaungana na ujumbe wa mwaka huu wa 21 wa maadhimisho ya Mtoto wa Afrika, kuwa “Sote kwa pamoja tuchukue hatua za haraka kunusuru watoto wa mitaani”.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii, lakini pia nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe hii ni Kauli ya Mawaziri, kama tunavyoelewa chini ya Kanuni ya 43 ni kwamba kauli hii huwa haijadiliwi, lakini bado tunayo nafasi ya kuweza kuuliza maswali kama kuna jambo bado halikufafanuka vizuri, Mhe. Waziri anaweza kuulizwa na baadae akatoa majibu. Waheshimiwa Wajumbe karibuni.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kupata ufafanuzi wa baadhi ya mambo yanayohusiana na taarifa hii ya vijana wetu ambao ndio taifa letu tegemezi la kesho tukijaaliwa.

Kwanza nilitegemea siku ya kuwasilisha taarifa hii Mhe. Waziri, miongoni mwa watu ambao watakuja kusikiliza taarifa hii ni watoto wenyewe ama Baraza lao la Wawakilishi sijui kama lipo. Kama lipo nashukuru ahsante sana katika hili nakupongeza sana kwa sababu taarifa hii inawahusu.

Lakini suala jengine Mhe. Spika, ni kwamba kama alivyotueleza Mhe. Waziri kuna vitendo ambavyo vinaongezeka kila uchao vya kuwadhalilisha watoto na hali ambayo inaonekana inakatisha tamaa.

Sasa licha ya Mhe. Waziri kuturipotia ni kesi ngapi zimetokea lakini kitu ambacho tungelitaka kukifahamu kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kesi ngapi zimehukumiwa katika hili.

Katika hili inaonekana kuongezeka kwa vitendo kama hivi inawezekana na uregevu wa sheria tulizonazo. Sasa nimuulize Mhe. Waziri serikali ina mpango gani.

**Mhe. Spika:** Mhe. Omar Ali Shehe samahani, uliuliza kama wadau wapo. Maafisa wangu walikawia kidogo kuleta taarifa ya kwamba kuna wadau wa jambo hili la leo asubuhi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe kuna vijana ambao wamekuja kuona shughuli zetu na kwa taarifa hii iliyowasilishwa hivi punde asubuhi inaonekana kwamba inawahusu sana. Vijana hao ni Mabaraza ya Watoto hapa Zanzibar ikiwemo Bodi ya Ushauri na Wajumbe wa Mabaraza hayo ya Watoto. Naomba basi niwatambulishwe kwenu kwa kuwaomba wasimame. Wale pale tunakushukuruni sana karibuni. Ahsante sana.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kutambulishwa ilikuwa ni muhimu kufahamu. Kwa hivyo, nilitaka kujua serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya sheria hizi ili kuona kwamba kunakuwa na adhabu za kutosha zinazoweza baadae zikakomesha vitendo kama hivi.

Suala la pili Mhe. Spika, kumekuwa na tabia ya watu wazima kuwatumia watoto wadogo wadogo katika shughuli za kuomba barabarani. Kama sasa hivi ukitembea maeneo ya Darajani kesi kama hizi kwa kweli ni za kawaida. Sasa ukweli kitendo cha mtoto kumtumilia katika kuomba ni kitendo ambacho kinamuathiri kisaikolojia mtoto na usitegemee mtoto kama yule akikua katika mazingira kama yale hatima yake itakuwa ni nini. Sasa nataka tujue kwamba serikali hili imeliona na kama imeliona serikali kama serikali inalichukulia hatua gani katika kuwanusuru watoto wale.

Mhe. Spika, la tatu kuna tabia siku hizi ya kuwashirikisha watoto katika mambo ya usanii na ngoma, hii tunachukulia kama ni sehemu za ajira zao. Mathalan utamuona mtoto mchanga kashirikishwa katika mambo ya maigizo, naamini kwamba mtoto mchanga hakuwa na hiari. Lakini je, kutumiliwa kwake katika vitendo kama vile vya kuwashirikisha katika ngoma kitu ambacho serikali inaendele kupiga marufuku mambo ya kuwaajiri watoto. Serikali ina mtazamo gani katika hilo.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa naomba niishauri serikali suala la watoto ni suala mtambuka na kwa kuwa ni suala la mtambuka linahusu Wizara ya Afya kwa mambo ya afya, linahusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mambo ya elimu, linahusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo katika sekta ya michezo, vile vile hata Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Naomba basi na Mhe. Waziri wakati atakapokuja angalau atueleze ni namna gani wanashirikiana ofisi yake na wizara hizo katika kuandaa kuona kwamba mtoto



wetu anabakia katika mazingira salama na anapata makuzi mema katika taifa lake. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kupata ufafanuzi juu ya maelezo ya Mhe. Waziri kuhusu taarifa hii ambayo ameiwasilisha hivi punde.

Mhe. Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza na kuipongeza taarifa hii na kupongeza juu ya hatua mbali mbali zile ambazo amezeleza. Mhe. Spika, mimi nitamuuliza Mhe. Waziri mambo mawili.

Katika taarifa hii ametueleza mambo mbali mbali kuhusiana na hali ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Sasa nimuulize tu Mhe. Waziri, ametwambia hapa kwamba wamepanga mikakati juu ya kuondokana na hali hiyo. Sasa tulitaka tu kwa muhtasari Mhe. Waziri alieleze Baraza lako tukufu ni mipango gani ambayo wizara imejipangia katika kuhakikisha kwamba tunapunguza au tunaondoa kabisa hali hii ya watoto wa mitaani ambao amewazungumza wanaoishi katika hali ngumu au hali hatarishi kwa lugha ya kileo.

Mhe. Spika, la pili Mhe. Waziri ametueleza kwamba tayari Baraza letu hili la Wawakilishi limeshapitisha Sheria ya Mtoto na ambayo tunaamini kwamba imeshatiwa saine na Mhe. Waziri. Sheria ambayo tunaamini kwamba kama itasimamiwa vizuri basi itaondosha kabisa au itapunguza hali hii ya unyanyasaji wa kijinsia ambapo humu mna takwimu nyingi tu ambazo kwa kweli ni za kutisha.

Sasa nimuulize Mhe. Waziri wizara yake imejipanga vipi katika kusimamia hii sheria mpya ambayo tayari imepitishwa. Kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba Baraza lako Mhe. Spika, huwa linatunga sheria nyingi lakini tatizo lipo katika usimamizi na utekelezaji wa sheria zenyewe. Sasa wizara yake kama ni mdau wa sheria hii imejipanga vipi kuhakikisha kwamba sheria hii inatekelezwa kikamilifu. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa taarifa yake. Mimi naomba kwenda ukurasa wa 39 pale pale Waheshimiwa Wajumbe wengi walipoulizia maswali ya ubakaji na udhalilishaji. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia kwamba jumla ya malalamiko 99 ya udhalilishwaji wa watoto katika mikoa yote ya Unguja na Pemba yalipokelewa na kushughulikiwa. Naomba kufahamu tu, hawa wanaofanya haya ni vijana wa miaka mingapi, au wazee, au wa umri

gani, nataka ile rika ya wale wanaoyafanya. Sijui Mhe. Waziri umefanya utafiti huo. Ahsante.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri. Katika maelezo yake Mhe. Waziri alitaja idadi ya watoto mayatima waliopo katika nyumba ya Mazizini, kama sikosei alitaja idadi kama ya watoto 47 hivi. Sasa idadi hii nahisi kwamba ni ndogo sana kwa sababu Zanzibar ina watoto wengi mayatima na wazee wao wakiwa katika hali ngumu sana.

Lakini pia nimuulize Mhe. Waziri ni vigezo gani hasa wanavyotumia vya kupokea hawa watoto mayatima. Lakini suala la pili ni muda gani Pemba kitafunguliwa kituo cha kulelea watoto mayatima. Ahsante.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mhe. Spika, kwa kuwa leo ni Siku ya Watoto wa Afrika Duniani wizara yake imejipanga vipi kutokomeza tatizo hili la unyanyasaji na ubakaji wa watoto Zanzibar.

**Mhe. Saleh Nasser Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitambua uwezo wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu tangu mwaka 1966 na ikawapatia nyumba Forodhani. Lakini sasa nilitarajia kwamba serikali itaendeleza juhudi zile kwa makusudi mazima ili kuendelea kuwaenzi watoto walioko katika mazingira magumu. Lakini kwa taarifa niliyonayo ni kwamba ile nyumba ya Forodhani ambayo waasisi wetu wa nchi hii waliwaweka watoto wenye mazingira magumu wameondoshwa na wamepelekwa katika nyumba ya *ZAYEDESA*.

- (a) Je, serikali ina mpango gani wa kuendeleza kwa makusudi juhudi zilizoanzishwa na viongozi wetu za kuwaenzi watoto wanaoishi katika mazingira magumu kama iliyofanywa mwaka 1966 kuwawekea jengo lile la Forodhani.
- (b) Je, ile nyumba iliopo pale *ZAYEDESA* imeshapewa serikali au bado ni yao wenyewe.
- (c) Ikiwa *ZAYEDESA* watahitaji nyumba yao. Je, watoto wale tutawaweka wapi. Ahsante.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Siku za nyuma kulikuwa na mtindo endelevu na mzuri sana wa kuwasaidia watoto wetu lishe kwa kupita sehemu za vijiji ambavyo watoto walikuwa wakionekana kama lishe zao zimepungua na ili kupunguza ule

utapiamlo. Kwa hivyo, walikuwa wanapitiwa majumbani wakisaidiwa kupewa lishe lakini sasa hivi mtindo ule umeondoka.

Je, ile taasisi iliyokuwa ikiendesha utaratibu ule ni serikali au ni kampuni. Kama ni kampuni au taasisi je, mradi huo umemalizika na lini utanza tena kuwasaidia watoto lishe.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa Mkoa wa Kaskazini Unguja ndio mkoa ambao unaongoza kwa vitendo hivi vya kudhalilisha watoto. Je, wizara yake ina mkakati mahsusi kwa mkoa huo ili kukomesha vitendo hivi.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri katika suala zima la hawa watoto wanaolelewa *SOS* ambao idadi yao ni kubwa sana. Nini utaratibu wa kutoa huduma ya afya kwa watoto hawa walio wengi.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu. Kwa kuwa tuna udhalilishaji sana wa watoto kutokana na takwimu tulizopewa na Mhe. Waziri. Je, atakuwa na mpango gani kuweza kuyatokomeza masuala haya wakiwemo watoto wa aina zote. Kwa sababu mitaani sasa hivi watoto tunawakuta wanazurura na takwimu tuliyopewa pengine itakuwa hawa wengine hawajaripotiwa. Je, tutakuwa na mpango gani wa kuweza kuwatafuta watoto hawa na kuwajua.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja tu. Mhe. Spika, kwa makusudi kabisa serikali imeweka kuwa watoto wote wapate elimu bila ya malipo, isipokuwa kuna kuchangia tu elimu lakini sio elimu bila ya malipo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri siku zote hapa anafafanua kuwa mtoto yeyote asirejeshwe nyumbani kwa sababu ya wazazi wake kushindwa kumlipia hiyo fedha ya kuchangia. Wizara kwa maana ya serikali imeshatoa tamko hilo lakini kuna walimu kwa utashi wao bado wanaendeleza kuwarejesha watoto majumbani na kuwakosesha haki zao. Tuseme leo haiwezekani kutoa tamko rasmi hasa likaenea katika maskuli yote ili utaratibu ukafuata na mtoto akapata haki yake ya kusoma.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri kuhusiana na haki ya mtoto. Mhe. Spika, ni muda mrefu tunapata taarifa katika vyombo vya habari kuhusiana na matukio ya watoto wanavyodhalilishwa. Lakini kesi zao hazifiki mwisho wala hupati kujua

hasa kwamba kuna mhalifu yeyote ambaye ametangazwa amehukumiwa miaka 10 au zaidi. Hizi kesi zinakuwa hazipatikani ushahidi au hazipo.

Kwa sababu mimi mwenyewe nipo kwenye Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala tumepita katika magereza yote sikumkuta mhalifu hata mmoja ambaye ana kesi kubwa kama hii ya kudhalilisha watoto. Je, hakuna hata mtu mmoja ambaye amehakikishwa kwamba amefanya kosa kama hili.

**Mhe. Spika:** Nafikiri maswali hayatoshi kwa sababu na wakati wa hotuba ya wizara hii mtapata nafasi kubwa sana ya kuweza kuchangia mambo mengi yakiwemo mambo haya haya yanayohusu watoto.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kufafanua kwa baadhi ya maswali niliyoulizwa. Kwanza kabisa Mhe. Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kesho Mwenyezi Mungu akipenda nitaisoma bajeti yangu na nitakapoisoma itafafanua mambo yote ya ubakaji, udhalilishaji na hatua mbali mbali tutakazozichukua sisi katika kuona kwamba mambo haya yanaondoka kabisa.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe ameuliza kesi ngapi zimehukumiwa. Mhe. Spika, sisi Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto katika kuona kwamba kesi hizi za udhalilishaji hazihukumiwi ndipo tukahangaika kuleta mbele yenu Sheria hii ya Mtoto. Kwa sababu inawezekana sheria zilikuwa zipo lakini kesi hazihukumiwi. Sasa hii Sheria ya Mtoto ina mambo mengi ambayo kwa vyovyote hukumu zitapatikana.

Kwa mfano, sasa hivi kazi kubwa ya mwanzo tunayoifanya ili sheria ifanye kazi tunaandaa mpango wa utekelezaji wa sheria hii. Tutakuwa na mafunzo maalum kwa hawa mahakimu. Lakini na kazi kubwa nyengine tutakuwa na uhamasishaji mkubwa katika mikoa, wilaya, shehia na vijiji, ili jambo lolote likija likitokea mtu awe hana pakupita, asije akasema mimi siyajui, mimi sina hili.

Lakini jengine katika kuona kwamba kesi hizi hazihukumiwi tumeweka vituo hivi vya *One Stop Centre* (Mkono kwa Mkono), kituo hichi sasa hivi kipo Mnazi Mmoja kinafanya kazi saa 24 watu hawaondoki pale. Kuna sehemu ya kwanza ya kufika aliyebakwa au aliyedhalilishwa akaingia akapewa ushauri nasaha, kuna sehemu ya pili ambapo pale utamkuta polisi, daktari, mwanasheria na kadhalika. Halafu kuna sehemu ya tatu ambayo hiyo ndio unakwenda kuangaliwa hasa kweli wewe umeumia. Sasa atakayetajwa hapo na njia zote hizo zimeshapitiwa atakuwa hana vya kujitetea.

Lakini pia tuna mpango na tunahangaika na wahisani wameonesha nia ya kukubali kwamba hichi chombo cha *DNA* kitapatikana, basi kikipatikana hicho ukweli unajitokeza hapo. Kwa hivyo, inawezekana kwamba kesi zetu zilikuwa hazihukumiwi lakini inshaallah zitahukumiwa. Sheria ya Mtoto iko wazi tunamshukuru Mhe. Rais ameshaiwekea saina na tutaifanyia kazi kwa hali na mali na sasa hivi tunaifanyia kazi.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Omar Ali Shehe amesema watoto wanatumiliwa katika kuombaomba mabarabarani. Mhe. Spika, hilo linawezekana kwa sababu sisi hatwendi sana barabarani, lakini Waswahili wanasema “Lisemwalo lipo na kama halipo liko njiani linakuja.”

Sasa Mhe. Spika, mimi natoa wito kwa wazee maana wao ndio wanaowatuma hao watoto nenda barabarani ukaombe tupate chochote angalau tujisaidie. Naomba jambo hili tuliache mara moja jamani kama lipo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Omar Ali Shehe anasema watoto hawa wanashirikishwa katika ngoma na mambo mengine ambayo si mazuri. Kwa nini tabia hizi wazee hatuziachi mara moja. Watoto tuwe nao, watoto tuwaangalie nyendo zao, tusikubali watoto kutokatoka usiku ovyo. Lakini sheria itakapofanya kazi yake basi kuna mambo pale ambayo yatakuwa hayamruhusu mtoto kuonekana zaidi ya saa moja hata itakapofika wakati wa hizi sherehe kama za sikukuu na kadhalika.

Mhe. Spika, anasema sheria inajieleza vizuri na kweli sheria inajieleza vizuri, kuna mambo mengi ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi na mimi nina nia ya kuwashirikisha Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kadri nitakavyokuwa naifanyia kazi hii sheria, ili tusaaidiane kuwaelimisha wenzetu juu ya sheria hii na iweze kutekelezeka.

Mhe. Spika, sasa nije kwa Mhe. Salmin Awadh Salmin, yeye anauliza hawa watoto wenye mazingira magumu tutawasaidia vipi, tutawajuaje. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi asubiri tutakavyoeleza kuhusu suala zima la watoto wenye mazingira magumu katika bajeti yetu tutakayoileta hapo mbele yenu.

Mhe. Spika, wizara imejipanga vizuri sana katika kutekeleza jambo hili la watoto wenye mazingira magumu. Moja nataka nimkumbushe Mhe. Salmin Awadh Salmin ni juzi tu tulikuwa kwenye semina ambayo tuliandaa kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi mbali mbali wa wizara

kuhusu watoto hawa wenye mazingira magumu. Nadhani Mhe. Mwakilishi bado anakumbuka.

Mhe. Spika, Mhe. Mwinyihaji Makame ni mwenzangu sana katika serikali hii. Naomba astahamili kesho tuje tumfafanulie namna ya utafiti tuliofanya katika mambo yote ya watoto wanaodhalilishwa, wasiodhalilishwa na kadhalika.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad anauliza kwamba kipindi gani kituo cha kulelea watoto Pemba kitafunguliwa maana yake hapa tuna nyumba kama hiyo Mazizini pale. Mhe. Spika, serikali imo katika jitihada za kuona kwamba kila linalofanyika Uguja na Pemba litafanyika. Kwa hivyo, tutakwenda kwa utaratibu kuona kwamba na Pemba nako lazima tuwe na nyumba ya kulelea watoto wadogo.

Mhe. Spika, pia kuna swali limeulizwa kuhusu vigezo gani vinavyotumika kwa kupokea hawa watoto yatima. Mhe. Spika, watoto ambao wazazi wao ni maskini sana ndio kigezo cha mwanzo hicho, wazee ambao hawawezi kuwatumia watoto wao, watoto wenye kuokotwa na hawatambuliwi wazazi wao, yaani tunaokota watoto wachanga, tunaokota watoto ambao wamefikia umri wa miezi minane. Mama anakwenda kumtupa mtoto wake sasa mtoto yule lazima tumhifadhi katika nyumba ya watoto.

Mhe. Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki anasema zamani kulikuwa na utaratibu watoto walikuwa wakipewa lishe. Mhe. Spika, mimi nataka niseme wakati wowote serikali yetu ya awamu hii ya saba ya kitaifa itakapokuwa tayari suala hili litafanyika. Lakini kwa sasa hivi nguvu yetu ni ndogo kidogo. Hata hivyo, misaada mbali mbali ikitokea basi huwa tunawapelekea watoto.

Kwa mfano, hivi karibuni tulikwenda Micheweni sisi katika jimbo lake hasa Mhe. Subeit Khamis Faki, tukagawa chakula cha watoto, nguo za watoto, viatu vya watoto. Nadhani ni moja katika kuwasaidia watoto waliokuwa hali zao ni ngumu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir amesema kwamba Mkoa wa Kaskazini una matatizo, watoto wanabakwa sana, vitendo vya kiudhalilishaji vimekuwa vikubwa sana na kwa bahati tunao hapa viongozi wa Mkoa wa Kaskazini. Naomba tujitahidini sana kuwaelimisha wazee wa Mkoa wa Kaskazini kwamba hili jambo sio zuri na limeshaanza kuwavumia sana wenzetu wa Kaskazini. Tujitahidi sana juu ya jambo hili.

**Mhe. Spika:** Wanasema inatosha Mhe. Waziri, kama kuna jambo kubwa unaweza kuwajibu.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Raya Suleiman Hamad amesema tutafanyaje zaidi ili pamoja na hesabu tuliyotoa hapa ya watoto wa mitaani, lakini tutafanyaje zaidi ili kuwaelewa hawa watoto.

Mhe. Raya Suleiman, tutajitahidi na hili kama atulivyokwisha kujitahidi katika sehemu nyengine na tutaendelea na Mikao mingine tuone hasa tunapiga vita kabisa watoto wa mitaani. Jambo hili sio zuri halituwekei heshima katika serikali yetu.

Mhe. Mussa amesema kwa nini watoto wanaodhalilishwa hatupati ripoti zao. Mhe. Spika, baada tu sheria yetu tukishaanza kuifanyia kazi basi tutakuwa tunajitahidi kutoa katika kikao chako hiki kitukufu taarifa kamili za udhalilishaji wa watoto katika Mikoa baada ya Mikoa tutakuwa tunatoa. Mkoa wa Kaskazini tutauleta habari, Mkoa wa Kusini Pemba tutauleta habari, Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa Kusini Unguja na mikoa yote mingine tutatoa habari zao.

Kwa bahari nzuri tuna mashirikiano mazuri, makubwa sana na Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya. Kwa hivyo, tutajitahidi kutafuta habari zao ili tuzilete hapa na nyinyi wenyewe nina hakika mtayaona mabadiliko. Tutatoa habari na tutawachukulia watu hatua. Mahakimu kwa sababu watakuwa wameshapata mafunzo maalum, naamini kwamba kesi hizi za udhalilishaji na ubakaji zitahukumiwa. Kwa kweli kesi zilikuwa hazihukumiwi, hatuna haja ya kuficha, kesi zilikuwa hazihukumiwi. Unapokwenda mahakamani watu wanashughulika na watu waliokamatwa kwa kuiba nazi na kuiba mambo mengine, lakini kesi ya udhalilishaji kabisa ilikuwa haihukumiwi.

Mhe. Spika, mimi naomba Waheshimiwa Wajumbe, kama sikuwajibu vizuri basi wastahamili kesho watapata habari katika bajeti yetu na tutaweza kufafanua vifungu baada ya vifungu. Naomba sana Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa tuone kama taarifa hii imepokelewa vizuri na Baraza. Wale wanaopokea taarifa ya utekelezaji wa haki ya mtoto wanyanyuwe mkono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Taarifa imepokelewa na Mhe. Waziri mwendeleo kuifanyia kazi. Mhe. Waziri pale ameahidi kwamba Mwenyezi Mungu akipenda kesho akiwasilisha hotuba ya wizara hii, basi mambo mengi yatafafanuliwa kwenye hotuba hiyo. Mimi nataka niseme kwamba na mwenyekiti wa Baraza Mhe. Mgeni atakuwepo hapa. Kwa hivyo, kesho tunaondoa kabisa mfumo dume.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukuwe nafasi hii nitowe taarifa ndogo pamoja na kuishukuru serikali. Baada ya umeme kukatika hivi punde na ikawa tayari tutoke nje, kumbe mafundi wetu walikuwa wanajitahidi kurekebisha mitambo ili kutumia jenereta mpya iliopo.

Kwa hivyo, naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru sana serikali kwa kushirikiana na Afisi yetu ya Baraza kwa kununua jenereta mpaya ambayo tayari inafanyakazi. (*Makofi*).

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tuondowe wasi wasi umeme unapokatika ni baada ya muda mfupi tu tutapata umeme wa jenereta yetu tena kikamilifu mambo yote pamoja na viyoyozvi vitakuwa vinafanyakazi.

Kwa kupitia kwako Mhe. Waziri Mohammed Aboud Mohammed Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, naishukuru sana serikali kwa msaada huu. Baada ya hapo sasa tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

#### UTANGULIZI

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe Spika, Kwanza naomba nichukuwe fursa hii na mimi kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Zainabu Omar Mohammed, Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa kuwasilisha ripoti ile muhimu sana ya mustakabali wa nchi yetu kupitia vijana wan chi yetu.

Pili Mhe. Spika, hotuba yangu ni kubwa sana na nimehitaji kuwa hivyo, kutokana na muelekeo mpya na thabiti wa uhakika wa serikali ya Dk. Ali Mohammed Shein. Mhe. Spika, lakini mengi ya maeneo hayo yanaonesha mahusiano na nitaarifa zaidi kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuonesha mahusiano baina ya wizara zetu na sekta mbali mbali zilizokuwemo kwenye wizara hii ya kilimo na maliasili. Mimi nitajikita zaidi katika kusoma maeneo



ambayo naamini ni muhimu ambayo naamini mwananchi wa nchi hii hasa wakulima watakuwa wanahitaji kuyasikia na kupata ufafanuzi wa kina.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Hali hii imeimarika zaidi katika awamu hii ya saba ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na wananchi wa Jimbo la Kiembe Samaki nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, leo Zanzibar ina Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Serikali ambayo imeasisiwa na Wazanzibari wenyewe kupitia kura ya maoni. Nchi yetu ikiwa miongoni mwa nchi chache duniani kufanya mageuzi makubwa ya utawala wake kwa salama na kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, umoja huu unahitaji kutunzwa, kulelewa na kuenziwa kwa maslahi ya Wazanzibari wa leo na vizazi vyetu vijavyo. Kwa kipindi hichi cha Historia ya nchi yetu, Wazanzibari tulihitaji Rais mwenye busara, makini, mkweli, mtaratibu, mchapa kazi, muungwana, mzalendo, mpole, mtenda na mpenda haki, jasiri na mwenye kujali maslahi ya watu na muhimu zaidi awe muumini wa kweli wa Umoja wa Wazanzibari. Dr. Ali Mohamed Shein ni Rais mwenye sifa hizo. Tunamuomba kwa Mwenyezi Muungu afya njema yeye na familia yake, na Inshaallah Mwenyezi Muungu atamjalilia uwezo mkubwa wa kutimiza ahadi na wajibu wake kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, nampongeza kwa dhati Maalim Seif Sharrif Hamad kwa mchango na uzalendo wake katika kuasisi maridhiano ya Kisiasa Nchini. Maridhiano ambayo yameandika Historia mpya ya Nchi yetu na kuweka misingi imara ya umoja, upendo na mshikamano. Maamuzi ya kufikia maridhiano kwa upande wa Mheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad yalihitaji ujasiri na ukweli wa dhati. Tunamuomba afya njema yeye na familia yake, pia tunampongeza kwa

michango na maelekezo mazuri anayotupa katika kuimarisha Sekta ya Kilimo Nchini mwetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balazi Seif Ali Iddi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Kitope na kuteuliwa kwake kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Tunamshukuru na kumpongeza kwa maelekezo na michango yake kwetu, Inshaallah Mwenyezi Muungu amjalie afya njema yeye na familia yake na mafanikio katika utendaji wa kazi zake.

Mhe. Spika, nina heshima kubwa kumshukuru na kumpongeza Makamu Mwenyekiti wa CCM na Rais Mstaafu wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume kwa mchango wake mkubwa katika kuasisi maridhiano ya Kisiasa Nchini, na mchango wake mkubwa katika kuiletea Nchi yetu maendeleo na hatimae kukabidhi madaraka ya Nchi yetu ikiwa salama na Nchi yenye amani, mshikamano na matumaini makubwa. Tunamuomba yeye na familia yake afya njema, furaha na mafanikio.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Spika wetu mpendwa, kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena kuwa Spika wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar. Hii imetokana na busara, juhudi na uzoefu wako na imani niliyokuwa nayo mimi na wenzangu wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar.

Aidha, pongezi za dhati zimuendee Mhe. Salmin Awadh Salmin Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara kwa kuwa pamoja nasi katika kusimamia majukumu ya Wizara hii, pamoja na kupewa imani kubwa na wajumbe wa sehemu ya Chama cha Mapinduzi wa Baraza lako katika kumchagua kushika nafasi hiyo ya Unadhimu na kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi.

Vile vile, napenda kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Baraza kwa michango yao, ushauri, maelekezo na mashirikiano yao mazuri kwa Wizara yetu. Pia nichukuwe nafasi hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kuchaguliwa kwake kwa nafasi hiyo. Pamoja na Wenyeviti wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa imani yao kwangu na kunichagua kwa kura nyingi kwa mara nyengine tena, ili niendeele kuwa Mwakilishi wao, pamoja na kunipa mashirikiano mazuri katika kuleta maendeleo ya Jimbo la Kiembesamaki. Mwenyezi Mungu atujaalie afya njema kheri na mafanikio.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, natoa mkono wa rambirambi kwa Mhe. Waziri na wafanyakazi wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto pamoja na familia ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Nd. Rahma Mohamed Mshangama aliefariki tarehe 15/04/2011. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi AMIN. Familia yake Mwenyezi Mungu Inshaallah atawajaalia subira. AMINA.

Mhe. Spika, kutokana na kipindi kirefu cha kiangazi na kukosekana kwa mvua za vuli 2010/2011 hali ya kilimo nchini iliathirika. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na kukauka kwa mazao, miti na mripuko wa viwavi jeshi. Matukio haya yaliwaathiri wakulima katika uzalishaji na kipato. Kutokana na athari hiyo Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili ilichukua hatua za kufanya tathmini ili kujua ukubwa wa athari hiyo pamoja na kugawa mbegu kwa wakulima walioathirika. Jumla ya tani 24.43 za mbegu ya mpunga zilitolewa kwa wakulima katika maeneo yalioathirika kwa jua kali. Pamoja na jitihada hizi napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wakulima wasivunjike moyo na waendeele na juhudi za kuendeleza kilimo na Wizara yangu iko pamoja nao katika kukabiliana na majanga kama haya.

Mhe. Spika, sote tunakubaliana kuwa kilimo bado kinaendelea kuwa mhimili mkuu wa maisha kwa wananchi wa Zanzibar. Inakadiriwa kuwa asilimia 70 ya watu wa visiwa hivi kwa njia moja au nyengine, wanategemea sekta ya kilimo katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kiuchumi, sekta ya kilimo inakadiriwa kuchangia wastani wa asilimia 32.8 katika pato la taifa na asilimia 75 ya mapato ya fedha za kigeni (OCGS 2010). Ni dhahiri kuwa sekta ya kilimo ina mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha, kuwa na uhakika wa chakula na lische, afya za wananchi na kwa hivyo ina athari kubwa katika maisha yetu.

Mhe. Spika, Ukweli huu unaaminisha kuwa tukikiendeleza kilimo na kikawa cha ufanisi na tija zaidi, ipo fursa kubwa kwa wananchi kupunguza ukali wa maisha, kuondokana na umasikini na nchi yetu kupiga hatua zaidi za ukuaji wa uchumi. Kinyume chake, kilimo kikiendelea kuwa duni, juhudi zetu za kupunguza umasikini zitazorota kwani wananchi waliowengi wanaoshiriki katika sekta hii watakoswa uwezo wa kujikomboa na watabaki katika dimbwi la umasikini.

## **MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MIKAKATI YA KITAIFA KATIKA SEKTA YA KILIMO**

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imeendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2010 – 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA), Malengo ya Milenia (MDGs), Mipango na Mikakati ya Kisekta na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (ATI) na Mpango wa Muda Mrefu wa Usimamizi wa Rasilmali za Misitu.

## **MUELEKEO WA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI KWA MWAKA 2011/2012**

Mhe. Spika, “Mapinduzi Daima“ ndio kauli mbiu ya Nchi yetu na watu wake. Mapinduzi ndio yaliyotukomboha na kutuletea umoja na mshikamano wetu, amani na utulivu, ustawi na maendeleo tunayojivunia hivi sasa.

Kauli mbiu ya “Mapinduzi ya Kilimo” ndio mwelekeo wa Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya saba na maana yake ni kutekeleza kwa vitendo dhamira ya kuwakomboa wakulima wa Zanzibar kutoka katika hali ya kilimo duni kisichokuwa na tija na kuweka mazingira na fursa za kuwawezesha kuongeza ufanisi na tija katika kilimo ili waongeze uzalishaji, wainue kipato, wawe na uhakika wa chakula na lishe bora na hatimae wapunguze umasikini.

Huu ndio mwelekeo wa sekta ya kilimo na maliasili na ndio malengo ya Dira ya 2020, maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya CCM 2010-2015, Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini (MKUZA II-2010), na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (ATI).

Aidha, dhamira hii ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo imefafanuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba zake za uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi aliyoitoa tarehe 5 Novemba, 2010 na sherehe za miaka 47 ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2011, na

ameisisitiza na kuitolea maelekezo katika ziara zake za mikoa mitano ya Zanzibar alizozifanya mwezi wa Mei na Juni, 2011.

Mhe. Spika, Mapinduzi ya Kilimo yataendelezwa kwa lengo la kujijengea uwezo wa kuwa na uhakika wa chakula katika nchi na kupunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa chakula kutoka nje. Ni vyema tukaelewa kuwa dunia hivi sasa imekabiliwa na hali ya upungufu mkubwa wa chakula na tishio la njaa. Sababu kuu za hali hiyo ni pamoja na upungufu mkubwa wa uzalishaji wa nafaka kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa, gharama kubwa za uzalishaji kutokana na kupanda bei za mafuta, na mahitaji makubwa ya nafaka yanayotokana na kuongezeka kwa matumizi mbadala ya nafaka. Hali hii imepelekea ushindani mkubwa katika masoko ya nafaka ya kimataifa na hivyo upandaji wa bei za vyakula hivi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar, hali hii pamoja na ongezeko la gharama za usafirishaji wa chakula kutoka nchi za Asia ya Kusini kunakosababishwa na uwepo wa maharamia wa kisomali katika mwambao wa bahari ya Afrika Mashariki, imepelekea upandaji mkubwa wa bei za vyakula muhimu ambavyo kwa kiasi kikubwa tunategemea kuagiza kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, bei ya mchele kwa mfano imepanda kwa asilimia mia moja (100%) kutoka shilingi 600 kwa kilo mwaka 2006 hadi shilingi 1200 kwa kilo mwaka 2011. Kutokana na hali nilioeleza hapo juu, mwelekeo kwa kipindi cha muda mfupi na wa kati ni upandaji wa bei za vyakula hivi hali ambayo si nzuri katika kuhakikisha usalama wa chakula nchini hasa kutokana na ukweli kwamba wananchi wanategemea kwa kiasi kikubwa mchele unaoagizwa kutoka nchi za nje kwa mahitaji yao ya chakula cha kila siku.

Aidha, mahitaji yetu ya mchele kwa mwaka ni wastani wa tani 80,000 ambapo wastani wa uzalishaji wa ndani kwa mwaka hivi sasa ni tani 25,000 za mpunga sawa na tani 16,000 tu za mchele ikiwa ni asilimia 20 ya mahitaji yetu ya kila mwaka na wastani huu huwa inapanda na kushuka baina ya asilimia 16 hadi 20 kutokana na mavuno yetu ya mpunga.

Mhe. Spika, Mkombozi wetu ni Mapinduzi ya Kilimo. Mhe. Rais, Dkt Ali Mohamed Shein ndie aliyeasisi na kuinadi kauli mbiu hii. Maelezo zaidi yamo katika kitabu cha ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015. Ninawaomba mukupitie ili muweze kupata muelekeo mzuri zaidi, ukiwemo Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Waheshimiwa viongozi wote wa Serikali na taasisi zisizo za kiserikali na Waheshimiwa wananchi wote wa Zanzibar tukubaliane na kauli

mbiu hii na sote tuinadi na tujihimize kuitekeleza ili yapatikane mabadiliko ya kweli yatayoweza kutukomboza kiuchumi na kuondokana na umasikini.

Kwa upande wetu, Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari tumejiandaa kwa kutayarisha Mpango maalum wa kuendeleza kilimo cha mpunga kwa miaka mitano ijayo ambao unaelekeza kuimarisha upatikanaji na matumizi ya mbegu bora kwa kilimo cha juu na mabondeni, kurahisisha upatikanaji na matumizi ya mbolea, kuimarisha ujenzi na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji, kurahisisha matumizi ya matrekta na zana bora za kisasa na kuimarisha utoaji wa huduma za elimu kwa wakulima. Matarajio ya mpango huu ni kuongeza uzalishaji wa mchele hapa nchini na hivyo kupunguza utegemezi wa mchele kutoka nje kutoka asilimia 84 ya mahitaji yetu mwaka 2010/11 na kuagizia kiasi cha asilimia 35 tu ya mahitaji yetu ya mchele ifikapo mwaka 2015/16. Mpango huu utekelezaji wake unaanza katika bajeti ya mwaka huu wa 2011/12.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa zao la karafuu kwa Zanzibar, Wizara yangu imekusudia kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko katika utekelezaji wa mkakati wa kufufua mikarafuu ambao kisheria na kiutawala utasimamiwa na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC). Wizara itachukua jukumu la kutoa utaalamu juu ya uzalishaji wa miche, uendelezaji mashamba na utafiti wa mashamba yote ya mikarafuu ili kuanzisha “*database*” ambayo itatupatia taarifa muhimu za uzalishaji wa karafuu, idadi ya mikarafuu katika umri tafauti, na tathmini ya mavuno ya karafuu yanayotarajiwa kila mwaka ili kutoa taarifa rasmi kwa Serikali juu na hali halisi ya mikarafuu na mkakati wa uimarishaji wake.

Aidha Wizara, kwa kushirikiana na taasisi husika, itaratibu suala la branding ya karafuu zetu ikiwa ni mkakati wa kutengeneza na kusajili haki miliki kwa karafuu za Zanzibar ambazo zinatambulika kwa ubora wake duniani, ili kuzilinda kisheria dhidi ya magendo na kupata sehemu kubwa zaidi ya thamani ya zao hili katika masoko ya kimataifa na hivyo kuwapa wakulima bei itayovutia uimarishaji wa zao hili muhimu kwa lengo la kuinua mapatao yao na ya nchi kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri sana utekelezaji wa mpango, namshukuru sana Mhe. Nassor Ahmed Mazrui tayari ameshauanza.

Mhe. Spika, hali ya vyanzo vikuu vya maji hapa Zanzibar ni mbaya kutokana na uvamizi mkubwa hasa kwenye maeneo yaliyoko nje ya mashamba ya Misitu ya Serikali kama vile Mwanyanya na Masingini. Kutokana na hali hiyo Wizara yangu inaendelea na usimamizi wa maeneo ya misitu yenye vyanzo vikuu vya maji pamoja na kufanya tathmini ya misitu yote iliyopo katika maeneo mengine

yenye vyanzo vya maji ili kuandaa mpango mahsusi kwa ajili ya upandaji miti na uhifadhi wa maeneo hayo.

Aidha, wizara yangu pia itaendeleza kampeni za upandaji miti kitaifa katika maeneo yenye vyanzo vya maji, fukwe za bahari na maeneo mengine yaliyoathirika. Wizara itaendelea na juhudi za kushajiisha wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa miti, maliasili na mazingira na kufafanua majukumu ya kila mmoja wetu katika kulinda, kuhifadhi na kusimamia utunzaji na matumizi endelevu ya maliasili zetu. Kutokana na umuhimu wa suala hili wizara yangu imeamua kwamba suala la upandaji miti kitaifa sasa litafanyika kila mwezi badala ilivyozeleka kwa kila mwaka. Mpango maalum umeandaliwa ili kuhakikisha wananchi wanashirikishwa katika kazi ya upandaji miti.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha miaka mitano ijayo Wizara itatekeleza dhamira ya Mapinduzi ya kilimo yatayopelekea sekta hii kutoa mchango zaidi katika uchumi wa taifa na kupunguza umaskini. Miongoni mwa mikakati ya Wizara iliyoungwa kufikia mafanikio haya kwa mwaka 2011/2012 ni:

- Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji na kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua (*Irrigation Master Plan*);
- Kuanzisha Mfuko Maalum wa Huduma za Kilimo (*Agricultural Development Fund*) kwa madhumuni ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na huduma za ufundi na matengenezo ya matrekta kwa kilimo cha mpunga ili kukidhi mahitaji tuliyojipangia;
- Kuendeleza programu za utafiti wa kilimo na maliasili kwa kuwashirikisha wakulima na washirika wengine;
- Kuhimiza na kushajiisha matumizi ya pembejeo na mbinu bora za kilimo na matumizi ya bora ya maliasili;
- Kuibua fursa na kujenga uwezo wa wajasiriamali katika kusarifu mazao ya kilimo na maliasili ili kukidhi mahitaji ya soko;
- Kutilia mkazo hifadhi ya mazingira na kuendeleza kilimo hai;
- Kupunguza uharibifu wa mimea unaotokana na maradhi, wadudu na ndege;
- Kuangamiza nzi wa matunda ili kuongeza fursa za kusafirisha matunda nje ya nchi;
- Kutekeleza mpango wa muda mrefu wa usimamizi wa rasilimali za misitu na maliasili zisizorejesheka;

- Kutekeleza mkakati wa uimarishaji wa zao la karafuu ikiwemo utafiti, uzalishaji, usarifu na *branding*; kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko;
- Kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na makaa kwa kutumia nishati mbadala
- Kutekeleza mkakati wa kudhibiti wizi wa mazao ya kilimo na maliasili kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika;
- Kutekeleza mkakati wa kudhibiti matumizi mabaya ya msumeno wa moto;
  - Kutekeleza mkakati wa kilimo cha juu, viungo, matunda na mboga mboga;
  - Kuimarisha utowaji wa huduma za elimu kwa wakulima kupitia mabwana/mabibishamba, skuli za wakulima, maofisa kilimo Wilaya na chuo cha kilimo Kizimbani;
  - Kutekeleza mkakati wa kuanzisha Akiba ya Chakula Zanzibar (*Zanzibar National Food Reserve*);
  - Kutekeleza mkakati wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri uzalishaji katika kilimo.
  - Kupitia Sheria na Kanuni zinazoongoza usimamizi wa KARANTINI na kuzifanyia marekebisho pale itakapo jitokeza haja ya kufanya hivyo, pamoja na kuimarisha kitengo cha KARANTINI.

Mhe. Spika, mbali na mikakati hiyo, wizara yangu inaendelea kufanya mazungumzo na washirika mbali mbali wa maendeleo kwa lengo la kupata mashirikiano ya kiufundi na fedha zaidi kwa maendeleo ya kilimo na maliasili. Miongoni ya Mashirika hayo ni *EXIM Bank* ya Korea, *USAID* ya Marekani na Washirika wengine wa Maendeleo kwenye Sekta ya Kilimo kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*Agricultural Donor Working Group*). Lengo la mazungumzo hayo ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inazipata na kuzitumia kikamilifu fursa zilizopo kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ili kuimarisha uzalishaji na tija na kukabiliana na changamoto za sekta ya kilimo na maliasili.

Aidha serikali imeandaa mkakati wa kuliendeleza zao la mpunga hapa nchini kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa mchele kutoka nchi za nje. Wizara pia inaendelea na matayarisho ya mikakati ya mazao mengine yakiwemo matunda, viungo, kilimo cha juu, kilimo cha maweni na mboga mboga kwa kutumia uzoefu uliopatikana kutokana na miradi ya huduma za kilimo (*PADEP, ASSP/ASDP-L*).



Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari imekamilisha tathmini yakinifu ya Mradi wa Umwagilaji kwa kushirikiana na *EXIM Bank* ya Korea ambao ndio watakaoufadhili mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji hekta 2000 ikiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Umwagiliaji maji. Taratibu za kukamilisha makubaliano ya mradi huu zinaendelea na tunatarajia mradi utaanza rasmi katika mwaka huu wa fedha wa 2011/12.

Aidha Wizara yangu imefanya mazungumzo na Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (*USAID*) kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika Programu ya *Feed The Future*, ambayo itasaidia katika maendeleo ya kilimo kwa mazao ya mpunga hasa katika umwagiliaji, na mbogamboga ambapo imekubalika kuwa Zanzibar ni moja katika maeneo matatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambako Programu hii itatekelezwa.

Tunatarajia kuwa programu hii itaanza utekelezaji wake mwaka huu wa fedha 2011/12 ambapo matayarisho ya kufungua ofisi hapa Zanzibar yanaendelea. Ni matumaini yetu kuwa utekelezaji wa programu ya *Feed the Future* utasaidia ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji maji na kutoa matumaini makubwa ya ongezeko la uzalishaji wa mpunga hapa nchini.

Mhe. Spika, wizara yangu pia imeshiriki kikamilifu katika mazungumzo ya pamoja baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Marekani chini ya uongozi wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Bibi Hilary Clinton, pia Zanzibar imepata fursa ya kutoa maelezo ya utayari wake kisera na kisheria katika kukabiliana na hali ya uhakika wa chakula na lishe na hatimae tumefanikiwa kushiriki katika utekelezaji wa programu ya Lishe ya *"The first thousand days of the child"* chini ya ufadhili wa *USAID* na Ireland.

Programu hii inatarajiwa kusaidia katika utekelezaji wa Sera na Programu yetu ya Uhakika wa Chakula na Lishe hasa katika kuimarisha lishe kwa makundi hatarishi ya watoto chini ya umri wa miaka mitano na kinamama wawawazito.

## **HALI YA UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO NCHINI**

Mhe. Spika, kwa ujumla uzalishaji wa mazao muhimu ya chakula umeongezeka katika msimu wa kilimo wa mwaka 2010 ukilinganisha na miaka kadhaa iliyopita hususan kwa mazao ya muhogo na ndizi. Hata hivyo,

ongezeko la uzalishaji wa mazao ya mpunga, mahindi, viazi vikuu na viazi vitamu umekuwa mdogo (Kiambatisho Nam. 1).

Mafanikio ya uzalishaji wa muhogo na ndizi yametokana na matumizi ya mbegu bora za muhogo na uwezeshaji wa kitaalamu wa miradi ya maendeleo ya kijamii (*PADEP/ASSP*) kupitia skuli za wakulima. Ongezeko hili la uzalishaji wa mazao hayo umesaidia katika uhakika wa chakula nchini ambapo pamoja na kiangazi kirefu cha mwaka 2010 hatukupata taarifa za upungufu wa chakula.

Mhe. Spika, uzalishaji wa mazao ya mpunga, mahindi, viazi vikuu na viazi vitamu umekuwa mdogo kutokana na wakulima wengi kutumia mbegu duni zenye uzazi mdogo na zisizostahamili maradhi, wadudu na ukame. Aidha, bado zipo changamoto zinazoendelea kukikabili kilimo cha mazao haya ikiwemo utegemezi mkubwa wa mvua, matumizi madogo ya pembejeo hasa mbegu bora na mbolea katika mpunga na uhamasishaji mdogo na ukosefu wa mbegu bora za viazi vikuu na vitamu.

Hata hivyo, juhudi za utafiti wa mbegu zimeanza kuzaa matunda kwa kupatikana mbegu bora za kilimo cha juu kwa mpunga aina ya *NERICA* ambayo inastawi maeneo yote ya juu, inastahamili ukame na maradhi na ina uzazi wa kuridhisha. Mbegu hii ambayo ni chachu ya Mapinduzi ya Kilimo itaanza kusambazwa kwa wakulima kuanzia msimu wa kilimo wa mwaka huu wa fedha 2011/12. Utafiti wa mbegu kwa mazao mengine bado unaendelea. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa upande wa maliasili kwa mwaka wa fedha 2010/2011 bado tulikabiliwa na changamoto ya mahitaji makubwa ya matumizi ya maliasili ambayo yanapelekea ukataji wa misitu, miti, uchimbaji wa mchanga, matofali na mawe. Aidha, matumizi makubwa ya nishati ya kuni na makaa yanachangia katika kuharibu mazingira ya visiwa vyetu kwa kumaliza misitu na miti ya matunda na mikarafuu.

Mhe. Spika, suala la matumizi ya msumeno wa moto, uchimbaji wa mchanga pamoja na rasilimali zisizorejesheka, bado limekuwa ni tishio katika jamii zetu kwa uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa na wananchi.

Katika kukabiliana na tatizo hili wizara tayari imeshatengeneza kanuni juu ya udhibiti wa msumeno wa moto, uchimbaji na usafirishaji wa mchanga na rasilimali nyengine zisizorejesheka pamoja na kuyarejeshea hadhi maeneo yaliyoathirika. Matumaini yangu kuwa iwapo sote tutashirikiana katika

utekelezaji wake basi tatizo hili litapungua sana. Wafanyakazi wa wizara yangu wataongoza katika utekelezaji wake

Mhe. Spika, wizi wa mazao ya kilimo, mifugo na rasilimali za maliasili nalo pia ni tatizo kubwa linaloendelea kuongezeka kwa kasi na kushamiri katika maeneo yote Unguja na Pemba. Tatizo hili linasababisha uharibifu mkubwa na limepelekea wakulima kuvunjika moyo, kukata tamaa na kupoteza imani kwa serikali na kuzidi kujiona wanyonge dhidi ya Wavunjaji na Wasimamizi wa sheria.

Hali hii pia inaathiri juhudi za serikali za kuongeza tija na uzalishaji kupitia programu mbali mbali ambapo baadhi ya mazao yanayoibiwa huvunwa machanga na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa matarajio ya ongezeko la tija na uzalishaji kama ilivyokusudiwa katika programu hizo.

Wizara yangu katika kukabiliana na tatizo hili imeunda kamati maalum kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, ili kufanya tathmini ya kina kuhusiana na wizi wa mazao, mifugo na rasilimali za maliasili, ambapo kukamilika kwa utafiti huu tutaweza kupata ripoti kamili itakayoweza kutupa muongozo na njia mbadala za kupambana na kupunguza tatizo hili kwa kushirikiana na wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama.

## **MUUNDO WA WIZARA, UTEKELEZAJI (2010/2011) NA MALENGO (2011/2012)**

Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeundwa na idara sita (6), taasisi mbili (2) na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
- Idara ya Kilimo,
- Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka,
- Idara ya Umwagiliaji Maji;
- Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe
- Chuo cha Kilimo Kizimbani na
- Taasisi ya Utafiti wa Kilimo

Mhe. Spika, utekelezaji katika Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2010/2011 ulilenga katika kuongeza uzalishaji wa mazao yenye ubora na tija,

kuongeza ufanisi katika udhibiti wa matumizi ya maliasili na kupunguza uharibifu wa mazingira. Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo kupitia taasisi zake kwa mwaka 2010/2011 pamoja na malengo ya mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:

## **IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Mhe. Spika, idara hii inasimamia uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati na Mipango ya Maendeleo pamoja na kazi za utafiti. Aidha, idara inaratibu mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya Wizara, taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jumuiya za Kikanda, Sekta Binafsi, Jumuiya na Asasi zisisizo za kiserikali pamoja na Washirika wa Maendeleo. Idara pia inasimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi.

## **UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Idara iliendelea kukusanya Takwimu za mazao ya kilimo kwa lengo la kuziwasilisha kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, pamoja na watumiaji wengine kwa utafiti;
- Ukamilishaji wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe na kupitiwa na Baraza hili tukufu;
- Kutoa toleo la pili la tafiti za kilimo na maliasili (2<sup>nd</sup> *Annual Research Review Proceeding*, 2011);
- Kukamilisha na kutumika Mpango Mkakati wa Wizara utakaotumika kwa kipindi cha miaka (2011 – 2014); sambamba na hilo utayarishaji wa Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo umekamilika katika ngazi ya Wizara;
- Wizara imeendelea kuratibu mashirikiano na taasisi za kitaifa na kimataifa sambamba na utayarishaji wa miradi;
- Jumla ya nakala 2,000 za Jarida la Mkulima zimetolewa na kusambazwa kwa wadau wa sekta ya kilimo na maliasili;
- Hadi kufikia mwezi wa Aprili jumla ya shilingi 212,013,950/= zimekusanywa sawa na asilimia 86.57 ya lengo lililowekwa;

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara ilisimamia na kuratibu utekelezaji wa programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo, taarifa za utekelezaji kama ilivyoambatanishwa:

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo–ASSP, (Kiambatisho Nam. 3)

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Mifugo-*ASDP-L*, Program hii inatekelezwa pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Kiambatisho Nam 4)
- Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe *FSNP* (Kiambatisho Nam. 5)
- Mradi wa Usarifu Mazao ya Kilimo (Kiambatisho Nam. 6)

Mhe. Spika, utekelezaji wa programu za Kuimarisha Huduma za Kilimo na Mifugo (*ASSP/ASDP-L*) umeleta mafanikio makubwa hasa kupitia utoaji wa taaluma na uwezeshaji kwa mfumo wa shamba darasa (*Farmer Field Schools*), ambapo wakulima na wafugaji hupata fursa ya kujifunza kwa vitendo mbinu bora za uzalishaji na hivyo kuongeza tija na ubora wa mazao yao. Jumla ya Shamba darasa 720 zenye kaya 12,600 tayari vimeshapatiwa mafunzo katika Wilaya 9 za Unguja na Pemba.

Kutokana na matokeo mazuri ya mafanikio ya mfumo huu wa shamba darasa, Wizara inakusudia kuongeza idadi ya shamba darasa kufikia 1200 mwaka huu wa fedha na kuziwezesha kuwa na ufanisi zaidi kama njia muhimu ya usambazaji wa taaluma ya uzalishaji ili kufanikisha malengo ya Mapinduzi ya Kilimo.

## **MALENGO YA MWAKA 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 idara inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kutayarisha na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango na Miradi ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Maliasili;
- Kufanya mapitio ya Sera ya Kilimo, Sera ya Misitu, Sera ya Mbegu na Haki miliki za wavumbuzi wa mbegu;
- Kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na maliasili;
- Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Utafiti na Dira ya Elimu kwa Wakulima (*Research Master Plan and Extension Vision*);
- Kuendelea kusimamia programu na miradi mipya na inayoendelea;
- Kuendeleza mashirikiano na taasisi za utafiti ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (*SUZA*) katika kufanya tafiti na utoaji wa matokeo;

- Kuendelea kuratibu mashirikiano kati ya Wizara na taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi;
- Kuandaa warsha na kutoa toleo la tatu la utafiti (3<sup>rd</sup> *Annual Agricultural Research Proceeding*);
- Kutayarisha na kutoa jumla ya nakala 2,000 za Jarida la Mkulima na kusambaza kwa wadau wa sekta ya kilimo na
- Kukusanya mapato yanayokadiriwa kufikia shilingi 1,293,774,000/= kutoka vyanzo vilivyo chini ya wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 idara itaendelea kusimamia programu tatu na mradi mmoja ambapo malengo yake yameoneshwa katika viambatisho namba 3,4 na 5. Aidha, katika mwaka huu wa fedha Idara itasimamia programu moja mpya inayohusu Uimarishaji Miundombinu ya Masoko ya Kilimo na Kuongeza Thamani ya Mazao (*Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance – MIVARF*)

**PROGRAMU YA UIMARISHAJI MUINDOMBINU YA MASOKO, UONGEZAJI THAMANI YA MAZAO NA HUDUMA YA FEDHA VIJIJINI (*Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance – MIVARF*)**

Mhe. Spika, program hii inatarajiwa kutekelezwa katika mikoa yote ya Bara na ya Zanzibar. Program hii itapatiwa jumla ya fedha USD 160.4 milioni sawa na Shilingi 247.1 bilioni ikiwa ni fedha za mkopo kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*IFAD*) USD 90.6 million sawa na Shilingi 139.5 bilioni ikiwa ni asilimia 56.4, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) USD 62.9 million sawa na Shilingi 96.9 bilioni ikiwa ni asilimia 39.2 na ruzuku kutoka Mtandao wa Kushajiisha Mapinduzi ya Kijani Afrika (*Alliance for Green Revolution in Africa - AGRA*) USD 6.9 million sawa na Shilingi 10.7 bilioni ikiwa ni asilimia 4.4

Mhe. Spika, Lengo la Programu hii ni kuimarisha miundombinu ya masoko ya kilimo, kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha vijijini (*microfinance*). Program hii itatekeleza kazi zake katika maeneo matatu yafuatayo:-

- a. Ujenzi wa mfumo na miundo mbinu ya masoko. Programu itasaidia
  - i. Ujenzi wa masoko wilayani yatakayokuwa na huduma za uhifadhi wa bidhaa zinazoharibika (*cold storage facilities*)
  - ii. Ujenzi wa viwanda viwili vya kuzalisha barafu (*ice plants*) kimoja kwa Unguja na Pemba.

- iii. Ujenzi wa barabara za mashambani ili kuunganisha maeneo yote ya uzalishaji na barabara kuu kwa lengo la kurahisisha kuyafikia masoko na utoaji wa huduma za kilimo.
- b. Utoaji mafunzo na uwezesaji katika usarifu wa bidhaa za kilimo. Programu itasaidia
  - i. Kuimarisha vikundi vya wajasiriamali katika usindikaji na usarifu wa bidhaa za kilimo
  - ii. Kutoa mafunzo ya usarifu na usindikaji bidhaa za kilimo kwa wakulima, wajasiriamali na watoaji huduma (*service providers*) za usarifu na usindikaji bidhaa za kilimo
- c. Kuanzisha mfumo wa utoaji wa huduma za kifedha vijijini (*Microfinance Systems and Institutions*). Programu itasaidia
  - i. Kutayarisha sera ya upatikanaji wa huduma za fedha kwa wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo (*Microfinance Policy*), ambapo tutafanya kwa mashirikiano na wizara inayoongozwa na Mhe. Omar Yussuf Mzee akiwa Waziri wetu wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. (*Mkofi*)
  - ii. Kuanzisha na kuwezesha taasisi za kijamii za utoaji huduma za fedha vijijini (*Community Microfinance Institutions*)

Mhe. Spika, hatua hii ya kuanzisha mfumo wa utoaji wa huduma za kifedha Vijijini na kutayarisha Sera ya upatikanaji wa huduma za fedha kwa wakulima (*Microfinance Policy*) ni hatua ya mwanzo ya kuelekea kwetu katika kuanzisha BENKI YA WAKULIMA. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wa Zanzibar, kwamba hii ni sehemu ya ahadi ya Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein. (*Makofi*)

Kwa hatua hii ya mwanzo, wakulima wa nchi yetu wataweza kupata fedha za kuanzisha shughuli za kilimo bila ya dhamana na riba ndogo sana. Kufanikiwa kwa suala hili, itakuwa ni hatua kubwa na ya msingi katika kuleta mageuzi ya Kilimo nchini na mpango huu unatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, programu hii itawawezesha wananchi kifedha na kimiundombinu ikiwa ni muendelezo wa programu na miradi iliyotanguliya ya kuwawezesha

wananchi kitaalamu kama vile *PADEP* na *ASSP/ASDP-L* ambazo zimejenga matumaini makubwa kwa wananchi ya uwezekano wa kuongeza tija na kipato chao kupitia shughuli za kilimo. Programu hii inatarajiwa kuanza utekelezaji wake mwanzoni mwa mwezi wa Julai, 2011.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba hapa nitoe msisitizo kidogo, kwamba *program* hii inajibu changamoto na kiu ya wananchi waliowengi kuwa ni wakulima. Moja katika ujenzi wa masoko, kwa sababu wakulima wetu wanapiga kelele sana kuhusu masoko na masoko, nakusudia nini? Masoko ambayo ni miundombinu wenyewe, ambapo wataweza kunadi mazao kila wilaya, masoko yatakuwa na hifadhi ya maghala pamoja na *facilities* kwa maana ya miundombinu ya kuhifadhi bidhaa zinazoweza kuharibika na yatawekwa maeneo ambayo masoko ya wakulima yako karibu. (*Makofi*)

Vile vile wakulima wetu watapa taaluma, yaani *Technology Exchange* juu ya usarifu wa mazao, kwa sababu wakulima hupiga kelele mazao yanapokuwa mengi mengi yao huharibika, basi watapata taaluma juu ya usarifu na usindikaji wa mazao hayo.

Jengine muhimu ambalo ni kujibu changamoto ya wakulima katika mabonde yao, maeneo yao wanayovuna na kulima barabara hazipitiki, hivyo mradi huu utaunganisha maeneo yote hayo na barabara kuu za nchi yetu, ili kuwapata nafunuu ya wakulima wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, muhimu zaidi au kiu kubwa ya wakulima wetu ni kukosa mitaji. Hatua tunayoiendeleza Mhe. Spika, kwamba wakulima wetu sasa hawatakuwa na haja ya kwenda kwenye mabonki makubwa ambako watadaiwa dhamana na wala hawana na kujazishwa mafumo yasiyokwisha. Hivyo, mpango huu utakuwa utaundwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mhe. Omar Yussuf Mzee kama nilivyosema na taasisi hizo nilizozitaja kwa wakulima wetu kupata mikopo bila ya dhamana, riba ndogo na kwa utaratibu ambao utakuwa na maslahi ya wakulima wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na hapa niwakumbushe haya yote ni miongoni mwa ahadi za Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein na muungwana anapoahidi basi hutekeleza. (*Makofi*)

## **MPANGO WA UWEKEZAJI KATIKA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA**

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaendelea kutayarisha Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na



Uhakika wa Chakula (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan - TAFSIP*), kutokana na makubaliano ya viongozi wakuu wa Bara la Afrika kupitia Mpango Mkuu wa Kuimarisha Kilimo Barani Afrika (*Comprehensive African Agriculture Development Programme - CAADP*) yaliyofikiwa Maputo Msumbiji mwaka 2003. Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizoridhia na kutia saini mkataba maalum (*CAADP Compact*) tarehe 8 Julai, 2010). Aidha, Mpango wa Uwekezaji (*TAFSIP*) unatarajiwa kutekelezwa katika maeneo makuu manne ambayo ni:

- Uzalishaji na Tija ya Kilimo (*Agricultural Production and Productivity*);
- Uhakika wa Chakula na Lishe (*Food Security and Nutrition*);
- Kuimarisha Biashara ya Kilimo Vijijini (*Rural Commercialization*); na
- Kuimarisha Taasisi za Kilimo (*Institution Strengthening*).

Programme hii inatarajiwa kuanza rasmi baada ya Mkutano Mkuu wa Biashara (*Business Meeting*) utakaowakutanisha washirika wa maendeleo katika sekta ya kilimo kama hatua ya kuupitia na kuukamilisha mpango huu. Mkutano Mkuu wa Biashara unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2011. Zanzibar itafaidaika na Programme hii kwa kuwasilisha programu zake za maendeleo ya kilimo moja kwa moja kwa washirika wa maendeleo ili kupatiwa ufadhili. Programe hizi tayari zimeshaandaliwa.

## **IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Mhe. Spika, idara hii ina jukumu la kusimamia masuala ya utawala, maslahi ya wafanyakazi, mafunzo na uwekaji kumbukumbu za wizara. Idara pia inasimamia rasilimali watu, ajira na sheria za kazi pamoja na kusimamia mali za serikali.

## **UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 kazi za idara hii zilisimamiwa na iliyokuwa Idara ya Sera na Mipango. Utekelezaji wa kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

- Jumla ya wafanyakazi 152 wameajiriwa katika mwaka fedha 2010/2011 kati ya hao 110 Mabwana na Mabibishamba ambao wamemaliza mafunzo kutoka Chuo cha Kilimo Kizimbani na wafanyakazi 42 (wanawake 4 na wanaume 38) wameajiriwa kama madereva wa matrekta na kada nyengine tofauti;

- Jumla ya wafanyakazi 59 (wanawake 33 na wanaume 26) wa wizara wamepatiwa mafunzo;

Wizara kupitia Idara hii na Chuo cha Kilimo Kizimbani inalifanyia kazi suala la upatikanaji wa hati miliki ya Shamba la Makurunge lililoko Bagamoyo, Tanzania Bara.

Shamba hili lilikuwa na ukubwa wa hekta 31,065 lilipoanzishwa rasmi mwaka 1977, lakini baada ya kukaa bila matumizi rasmi yaliyokusudiwa kwa muda mrefu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikubaliana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba eneo la hekta 6217 litengwe kwa matumizi ya Chuo cha Kilimo Kizimbani ambao watapatiwa hati miliki, na sehemu iliyobaki irudishwe kwa matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maombi rasmi ya kupatiwa Hati miliki yamefikishwa katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, Dar es Salaam baada ya kupitiwa na kukubaliwa na taasisi husika ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

## **MALENGO YA MWAKA 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2011/2012 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kutayarisha mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi (*Training Master Plan*) itayoonesha maeneo ya vipaumbele katika fani za Wizara;
- Kuimarisha utendaji katika uhifadhi wa kumbukumbu zikiwemo taarifa za wafanyakazi na rasilimali za wizara (*DataBase*);
- Kutayarisha mpango mkakati (*Strategic Plan*) wa miaka mitatu wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa kazi;
- Kuhakikisha rasilimali za Serikali zilizomo ndani ya Wizara zinatunzwa na kupatiwa hatimiliki;

## **IDARA YA KILIMO**

Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa Wakulima, Uhifadhi na Ukaguzi wa Mazao na kutoa elimu, mafunzo na ushauri kwa wazalishaji.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 malengo ya idara yalitekelezwa na Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima ambapo huduma za elimu kwa wakulima zilitolewa kama ifuatavyo: -

- Vipindi 32 vya redio (sawa na asilimia 80) na 20 vya TV (sawa na asilimia 66) vilitayarishwa na kurushwa hewani;
- Wakulima 1,600 walipatiwa mafunzo ya ukulima bora wa mazao;
- Mabwana/mabibishamba 120 sawa na asilimia 80 wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za kilimo;

Mhe. Spika, idara ilitoa huduma za utibabu wa mimea, udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu pamoja na kufanya utafiti. Katika juhudi za kukabiliana na tatizo la nzi wa matunda, jumla ya mitego 21,718 imesambazwa kwa wakulima 4,442 katika wilaya za Unguja na Pemba; jitihada hizi zimepelekea kupungua kwa athari ya kuharibika matunda kwa wastani wa asilimia 43.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na juhudi za kupambana na nzi wa matunda tungeweza kufanikiwa zaidi iwapo wakulima wangepatiwa wito wa Wizara wa kufukia matunda yote yaliyoathiriwa kama njia muhimu ya kudhibiti uenezi wa wadudu hao. Nachukua fursa hii kuwaomba waheshimiwa wawakilishi kusaidiana na wizara katika kuhamasisha wananchi kuitikia wito wa kuangamiza wadudu hao. Kazi nyengine zilizofanywa ni kama ifuatavyo:-

- Uangamizaji wa viwavijeshi vilivyojitokeza katika msimu wa kilimo 2010/2011 kwenye mashamba ya mpunga na mahindi ulifanikiwa kwa kupiga dawa bila ya malipo kwa wakulima;
- Utafiti wa kudhibiti nzi weupe (*Spiral whiteflies*) katika mazao ya mboga mboga unaendelea kwa kutumia madawa ya miti shamba na “*effective micro organisms*”;

Mhe. Spika, idara imeendelea kutilia mkazo upatikanaji na kushajiisha matumizi ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea, madawa ya kilimo na huduma za matrekta. Kazi zilizofanyika kwa msimu huu ni kama ifuatavyo:

- Jumla ya ekari 29, 677 za mpunga wa kutegemea mvua zililimwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 98.92 ya lengo;
- Jumla ya tani 124 za mbegu bora za mpunga (sawa na asilimia 124 ya lengo) na tani 10 za mbegu ya mahindi zililishwa na kusambazwa kwa wakulima wa Unguja na Pemba. Kati ya hizo tani 22 zilitolewa bure kwa wakulima ambao walipata athari ya

viwavi jeshi. Mbegu iliyosalia iliuzwa kwa bei ya ruzuku ya shilingi 500 sawa na asilimia 50 ya bei kwa kilo;

- Tani 442.5 za mbolea zimenunuliwa na kuuziwa wakulima kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50 ya bei;
- Jumla ya lita 18,000 za dawa ya magugu ziliuzwa kwa wakulima kwa ajili ya kuua magugu katika mashamba ya mpunga.

## **MALENGO YA MWAKA 2011/2012**

### **MPANGO MAALUM WA KUENDELEZA ZAO LA MPUNGA**

Mhe. Spika; kama tulivyotangulia kusema, serikali kupitia wizara yangu imeandaa Mpango Maalum wa kuimarisha uzalishaji wa zao la mpunga ambao utekelezaji wake unaanza katika bajeti hii. Mpango huu ni miongoni mwa hatua zinazochukuliwa na Wizara yangu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II) ulioidhinishwa rasmi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2010 ambao kwa upande wa Kilimo cha mpunga umeweka wazi malengo yafuatayo:-

- Kuongeza eneo la miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kutoka hekta 700 sawa na asilimia 8.2 ya Mpango Mkuu wa Umwagiliaji mwaka 2010 hadi hekta 5805 sawa na asilimia 68.1 ifikapo mwaka 2015
- Kuongeza tija kwa kilimo cha mpunga wa juu kutoka wastani wa tani moja kwa hekta mwaka 2010 hadi tani tatu kwa hekta mwaka 2015
- Kuongeza tija kwa kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji kutoka wastani wa tani 3.5 kwa hekta hadi tani 7 kwa hekta mwaka 2015
- Kuongeza mchele unaozalishwa ndani katika soko letu kutoka asilimia 15 mwaka 2010 hadi asilimia 65 mwaka 2015 (Kupunguza utegemezi wa mchele wa kuagiza kutoka asilimia 85 ya mahitaji yetu mwaka 2010 hadi asilimia 35 ya mahitaji yetu ya mchele ifikapo mwaka 2015)

Mhe. Spika, Mpango Maalum wa Kilimo cha mpunga umelenga kuongeza eneo litalopandwa mbegu bora kwa ajili ya Kilimo cha juu (*Upland*) na Mabondeni (*Lowland*) ili kuongeza tija na uzalishaji.

Kwa upande wa maeneo ya umwagiliaji maji, wizara itahakikisha kwamba wakulima katika maeneo yote yaliyojengwa miundombinu ya umwagiliaji na makinga maji wanatumia mbegu bora na mbolea kwa kutoa elimu juu ya umuhimu wa matumizi ya pembejeo hizo. Wizara inakusudia kuweka kanuni ndogo ndogo za kushajihisha matumizi bora ya pembejeo katika maeneo hayo kupitia usimamizi wa jumuiya zao za wakulima.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sensa ya kilimo ya mwaka 2007/08 takwimu zinaonesha kwamba hivi sasa Zanzibar ina eneo lenye ukubwa wa ekari 66,500 zinazoweza kutumika kwa kilimo cha mpunga. Kati ya hizo ekari 21,300 ndizo zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji kwa mujibu wa uhakiki na tathmini ya Mpango Mkuu wa Umwagiliaji maji (*Irrigation Master Plan*, 2004) na zilizosalia ekari 45,200 zinatumiwa kwa kilimo cha mpunga wa juu. Hadi sasa eneo lililojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji ni ekari 1,750 sawa na asilimia nane (8%) tu ya eneo lote linalofaa kwa kilimo hicho.

#### **Mfumo wa Ukulima wa Mpunga na ukubwa wa maeneo husika**

<b>Mfumo wa Ukulima wa Mpunga</b>	<b>Ukubwa wa Eneo (Ekari)</b>
Umwagiliaji maji	1,750
Makinga maji	200
Kutegemea mvua - Mabondeni	19,350
Kutegemea mvua - Kilimo cha juu	45,200
<b>JUMLA</b>	<b>66,500</b>

Mhe. Spika, Mpango Maalum wa Kilimo cha Mpunga umedhamiria kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mpunga kukidhi mahitaji ya Kilimo cha juu na mabondeni ambapo wakulima kwa kiasi kikubwa bado wanaendelea kutumia mbegu zao za asili kama vile Ringa, Kiya la Ngawa, Madevu, Kidunari, Kibata Ngoto, Mpakulie Bwana, Kibawa, Arishe, Baraza Hailigwa, Mvivu Hali, Usintupe, Kijicho, Moshi na nyingi nyenginezo zenye uzazi mdogo. (*Makofi*)

Matumizi ya mbegu hizi za asili kwa wakulima wetu wa mpunga hivi sasa ni zaidi ya asilimia 80. Kwa vile tumekamilisha utafiti wa mbegu mpya ya mpunga wa juu aina ya *NERICA*, Wizara ya Kilimo na Maliasili imepanga kuanzisha uzalishaji na usambazaji wa mbegu hizi kutoka zero mwaka 2010/11 hadi kufikia tani 140 za *NERICA* mwaka 2011/12.

Mhe. Spika, aidha wizara inaendelea na uzalishaji wa mbegu bora kwa Kilimo cha mabondeni ikiwemo *BKN Super, Super India, TXD 88* na *TXD 306* na inadhamira ya kuongeza upatikanaji wa mbegu hizi kutoka tani 124 mwaka 2010/11 na kufikia tani 215 mwaka 2011/12.

Suala hili la uzalishaji mbegu bora litatekelezwa kwa mashirikiano ya karibu baina ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na Shamba la Pamoja la Kilimo la JKU – Bambi pamoja na mikataba ya uzalishaji mbegu kwa wakulima, ambapo mbegu hizo zitasambazwa kwa wakulima kuanzia msimu wa kilimo wa mwaka 2011/12. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika utoaji wa huduma za zana za kisasa za Kilimo, Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia mpango huu imekusudia kukibadilisha Kilimo cha Mpunga kutoka katika matumizi ya zana duni za jembe la mkono na kiwe cha kisasa, ili kuvutia nguvu kazi ya vijana ambayo kwa kiasi kikubwa hajahamasika vya kutosha katika shughuli za kilimo.

Wizara inakusudia kuongeza upatikanaji wa matrekta makubwa na madogo ya 50HP ambayo yatumika kwa kilimo cha umwagiliaji maji na hasa kutoa huduma katika maeneo ya Pemba, ambapo matrekta makubwa hayawezi kufanyakazi kutokana na muinuko wa ardhi yake.

Aidha wizara imelenga kuingiza nchini zana nyengine za Kilimo cha mpunga ikiwemo zana za kupandia (*planters*), kuvunia (*harvesters, rippers na threshers*) na za kutwanga (*milling machines*) kwa lengo la kurahishisha kazi, kupunguza upotevu kabla na baada ya mavuno na kuhamasisha Kilimo cha Mpunga kuwa cha kibiashara. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu wanisikilize vizuri kwa maana asilimia kubwa waliwachagua ni wakulima na hata wa Kikwajuni, pengine hawana ardhi ya kulimai wanalima sehemu nyengine. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa mnasaba wa utekelezaji wa mpango huu, katika mwaka wa 2011/12 Wizara ya Kilimo na Maliasili inakusudia kuongeza utoaji ruzuku katika huduma za kilimo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitoe msisitizo katika eneo hili, utoaji wa ruzuku unahitaji serikali makini inayojiamini na yenye muelekeo na dhamira ya dhati na nia njema kwa wananchi wake. Utoaji wa ruzuku kwa wakulima wa nchi maskini zinazoendelea haupendezi na haukubaliki na baadhi ya Nchi Wahisani na wengine kutishia hata kuondosha misaada yao. *(Makofi)*

Pamoja na yote hayo, Serikali inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, baada kuzingatia yote hayo, bado imeona kuna haja kubwa sio tu kuendeleza utoaji ruzuku kwa wakulima wa nchi yetu bali kuurasimisha utaratibu wa utowaji ruzuku, ili uwe sehemu ya Sera na Mipango ya Serikali yetu. Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umakini na ujasiri wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali yetu inaongeza viwango vya ruzuku, ili kuwajengea misingi imara wakulima wa nchi yetu na hatimaye kuondokanana na kilimo duni na kuelekea kwenye kilimo cha kisasa chenye tija na kilimo endelevu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kutangaza bei mpya za huduma za kilimo kwa mwaka wa fedha wa 2011/12 kama ifuatavyo:

HUDUMA	BEI SASA KWA KILO (Shilingi)	BEI YA SASA KWA POLO (Shilingi)	BEI MPYA KWA KILO (Shilingi)	BEI MPYA KWA POLO (Shilingi)	GHARAMA HALISI KWA KILO (Shilingi)
Mbolea TSP	600	30,000	300	15,000	60,000
Mbolea UREA	400	20,000	200	10,000	40,000
Mbegu ya Mpunga	500	25,000	200	10,000	60,000
<b>HUDUMA ZA MATREKTA</b>					
HUDUMA	BEI SASA KWA EKA (Shilingi)	BEI MPYA KWA EKA (Shilingi)	GHARAMA HALISI KWA EKA (Shilingi)		
Kuchimbua	32,000	16,000	64,000		
Kuburuga	32,000	16,000	64,000		

## DAWA YA MAGUGU

HUDUMA	BEI SASA KWA LITA(Shilingi)	BEI MPYA KWA LITA (Shilingi)	GHARAMA HALISI KWA LITA (Shilingi)
Dawa ya Magugu	12,500	6,000	12,500

Mhe. Spika, kabla kutangaza bei hizi nilisema kwamba mpango huu unahitaji serikali iliyokuwa makini yenye nia njema, nia thabiri na inayojiamini wakubwa hawapendi jambo hili lakini Rais wetu ameahidi ametekeleza. Kipimo cha muungwana ni utekelezaji wa ahadi zake nikiwa Waziri wake wa Kilimo na Maliasili nachukua nafasi hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Moh'd Shein kwa uweli wake na uungwana wake.

Mhe. Spika, Ili kuhakikisha kuwa pembejeo hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa, ruzuku zilizoanishwa katika jadwali ya hapo juu watapatiwa wakulima chini ya utaratibu maalum ulioandaliwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia kwenye jumuiya zao. Wizara ya Mhe. Haroun Ali Suleiman imeshaelekezwa kuwasaidia wakulima wetu ikiwa wa mpunga, mananasi Donge kule, ndimu, ndizi Makunduchi kule, ikiwa wa mihogo Tumbatu wote hao ruzuku hizi watapatiwa na watasaidiwa kujiunga kwenye vikundi tutaomba uongozi wenu wawakilishi nyinyi wa wananchi.

## KILIMO CHA MATUNDA NA VIUNGO

Mhe. Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa mazao ya matunda na viungo kwa wakulima wadogo wadogo hasa katika kujipatia ajira, kipato na katika kukimu mahitaji yao ya chakula. Wizara kupitia programu za huduma za kilimo na utafiti inaendelea kushajiisha matumizi ya miche bora na utaalamu katika uzalishaji wa mazao haya na hasa katika kuongeza thamani ili kupata mazao yaliyobora kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na pia kwa usafirishaji. Aidha, Wizara inakusudia kurejesha haiba ya Zanzibar kuwa visiwa vya viungo (*Spice Islands*) kwa kutayarisha mkakati maalum wa uendelezaji wa kilimo cha viungo (*Spice Development Strategy*).

Mhe. Spika, Viungo muhimu ambavyo baada ya utafiti wa kina vimeonesha mwelekeo wa uzalishaji wa kibiashara na vitakavyoingizwa katika mkakati huo ni pamoja na karafuu, pilipili kichaa, manjano, mdalasini, vanilla, pilipili manga na mchaichai. Viungo vyengine kama tangawizi, hiliki, kungumanga,



mvuje, mrehani, hina, zingifuri na vyenginevyo vitaimarishwa kwa ajili ya utafiti, mafunzo na matumizi ya ndani ikiwemo maonyesho ya watalii.

Mhe. Spika, kwa upande wa kilimo cha matunda na viungo, Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kutoa elimu ya uzalishaji kupitia skuli za wakulima (FFS) zitakazoanzishwa maalum kwa ajili ya matunda na viungo muhimu hasa mikarafuu, minanasi, miembe, midimu na viungo ambavyo vimeonyesha mwelekeo wa uzalishaji wa kibiashara. Aidha kupitia programu ya Miundombinu ya masoko, Usarifu wa Mazao na Huduma za fedha vijijini, Wizara yangu itashajiisha uundwaji wa vikundi vya wajasiriamali wa kusarifu mazao haya ili kuongeza thamani na kuyafikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

## **KILIMO CHA MAZAO MENGINE YA JUU**

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imepata uzoefu mkubwa katika utafiti na uendelezaji wa kilimo cha juu hasa kwa mazao ya muhogo, viazi vikuu, viazi vitamu na migomba. Kupitia tafiti mbali mbali zilizofanywa katika vituo vyetu vya utafiti wa kilimo, Wizara imefanikiwa kuondosha baadhi ya vikwazo vya uzalishaji kwa mazao haya hasa katika kupata mbegu zinazostahamili maradhi na zenye uzazi mkubwa. Aidha, Wizara imefanikiwa kuzifanyia utafiti na kuzihakiki mbinu bora za uzalishaji wa mazao haya kwa kushirikiana na wakulima wenyewe ambao sasa wameanza kupata mavuno makubwa wanapotumia mbegu bora na utaalamu uliozalishwa kutoka vituo vya utafiti.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka wakulima wa muhogo walivyohangaika wakati wakitumia mbegu zao za asili kama Kibiriti, Jawa, Kigoma, Ndege, Rikunde, Majoka, Msheli, Mtayata, Mfodoa, Boma, Chane, Matemwe, Mbega na nyenginezo ambazo ziliathiriwa sana na matatizo ya maradhi na kupunguza uzazi. Kupitia utafiti uliofanywa na wataalamu wetu, kwa kuchanganya mbegu za asili na za kigeni, tumeweza kugundua na kuzindua mbegu bora nne za muhogo ambazo zinastahamili maradhi na zina uzazi mkubwa. Mbegu hizo ni Kizimbani, Machui, Mahonda na Kama ambazo tayari zimesambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba kwa ajili ya uzalishaji.

Mhe. Spika, Mbegu hizi nne zinaendelea kuzalishwa katika vituo vyetu vya kilimo vya Kizimbani, Mahonda, Matangatuani na Weshu na pia kwa wakulima maarufu Unguja walioko Mahonda, Kinduni, Kama, Machui, Dunga, Kilombero, Bumbwini, Chaani Masingini, Kinyasini, Mgambo, Muyuni, Kiboje Ghana, Kombeni na Nyamanzi. Kwa upande wa Pemba wakulima wazalishaji wa mbegu hizi wako Matangatuani, Konde, Vikunguni, Chakechake, Pujini, Makombeni, Gando, Junguni, Kinyasini, Mtakata,

Vitongoji, Kangani, Mjimbini, Mtambile, MizeMiyumbi na Kichunguu. Aidha mbegu mbili za kienyeji, Mwari kwa hapa Unguja na Sepide kwa Pemba zimeonyesha mwelekeo mzuri wa uzazi na ustahamilivu wa maradhi na zinaendelea kutumiwa na wakulima wengi.

Mhe. Spika, Kwa mnasaba wa kilimo cha juu, Wizara inakusudia kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kutanua matumizi ya mbegu bora na utaalamu huu kwa wakulima wengi zaidi kupitia skuli za wakulima (*FFS*) ili yapatikane mabadiliko ya kudumu na endelevu ya uzalishaji na tija katika shughuli za kilimo. Aidha, Wizara imedhamiria kuziunganisha juhudi za utafiti wa mazao haya na programu zinazotoa elimu na huduma za kilimo kama *PADEP*, *ASSP/ASDP-L*, *MIVARF* na nyenginezo ili matokeo ya utafiti yatafsiriwe kwa vitendo na yasaidie kukibadilisha kilimo chetu kutoka katika hali duni iliyopo sasa na kuwa kilimo chenye tija na cha kibiashara kwa manufaa ya wakulima na nchi yetu..

### **KILIMO CHA MAWENI**

Mhe. Spika, Kilimo cha Maweni ni sehemu muhimu ya shughuli za kilimo Zanzibar hasa kwa wakaazi wa ukanda wa maweni ambao wanakitegemea sana katika kukimu maisha yao. Wakulima wengi wa ukanda huu wanauzoefu mkubwa katika uzalishaji wa mbaazi, mtama, uwele, fiwi, viazi vikuu na pilipili hoho, lakini kwa kipindi kirefu kilimo chao hicho kimeachwa bila ya mfumo imara wa usaidizi wa kitaalamu. Kwa kulitambua hilo, Wizara yangu imejipanga kuwaendeleza wakulima wa maweni kwa kuwapatia utaalamu kupitia skuli za wakulima na itaendelea kushajiisha matumizi endelevu ya rasilimali za ardhi na maji katika kuendeleza kilimo hiki bila ya kuathiri mazingira na maliasili zilizowazunguka.

Mhe. Spika, Kilimo cha mboga mboga ni tegemeo kubwa kwa wazalishaji wadogo wadogo wa maeneo ya Maweni na katika maeneo yaliyokaribu na mjini na yanayozunguka shughuli za utalii. Wizara yangu inatambua umuhimu wa mbogamboga katika kuhakikisha lishe bora na katika kuinua kipato cha wananchi, na hivyo imeandaa mpango wa kuinua uzalishaji kupitia programu ya “*Feed the Future*” inayofadhiliwa na *USAID*. Utekelezaji wa mpango huu utasaidia kuongeza uzalishaji wa ndani wa mboga mboga na hivyo kulitumia kwa ukamilifu soko letu la utalii linaloongezeka kwa bidhaa hizi ambapo hivi sasa zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji ya mboga mboga yanatoka nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika; juhudi hizi zitakwenda sambamba na uimarishaji wa utoaji huduma za Elimu kwa Wakulima kwa kuajiri na kutoa mafunzo kwa

Mabwana/Mabibishamba watakaopangwa katika Shehia, pamoja na kuwapatia usafiri maofisa wa Elimu kwa Wakulima katika ngazi za Shehia, Wilaya na Mkoa ili kuimarisha utendaji kazi utakaoleta ufanisi na usimamizi makini wa Mapinduzi ya kilimo tunayoyakusudia.

Mhe. Spika, Mapinduzi ya kilimo yataenda sambamba na matumizi ya pembejeo na zana za kisasa za kilimo. Kwa upande wa pembejeo, Idara kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 inakusudia kuzalisha na kusambaza tani 140 za aina mpya ya mbegu ya mpunga wa juu *NERICA* na tani 215 ya mbegu bora za mabondeni ili kuongeza utumiaji wa mbegu bora kutoka asilimia 0 kwa kilimo cha juu mwaka 2010/11 hadi asilimia 10.3 mwaka 2011/12, na kutoka asilimia 19.4 mwaka 2010/11 hadi asilimia 33.6 mwaka 2011/12.

Mhe. Spika, matumizi ya matrekta na zana za kisasa za kilimo yataimarishwa kwa kuagizia matrekta mapya makubwa (*Hp 80*) nane, matrekta madogo (*Hp 50*) 16, majembe ya kulimia 24, majembe ya kuburugia 24, *power tillers 50, seed drillers 50, mini combine harvestors 30, rice reappers 30, na threshers 30*. Zana hizi zitarahisisha kazi za matayarisho ya ardhi ili kuwahi msimu wa kilimo na zitapunguza upotevu wa mpunga kabla na baada ya mavuno. Aidha zana hizi zinatarajiwa kuvutia nguvu kazi ya vijana ambayo inahitajika sana katika kufikia malengo ya Mapinduzi ya Kilimo.

## **UDHIBITI WA INZI WA MATUNDA**

Mhe. Spika, suala la kuwadhibiti inzi wa matunda litapewa umuhimu unaostahili ili kuwatokomeza kabisa inzi hawa na kurudisha hadhi ya matunda yetu na fursa ya kuyasafirisha nje ya nchi kama ilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya 90 kabla ya mashambulizi ya inzi hawa. Katika mkakati wa muda mrefu, Wizara inashiriki katika matayarisho ya Mradi wa kikanda (*Regional Programme*) kwa nchi za Afrika ya Mashariki wa kuangamiza inzi wa matunda kwa kutumia mionzi chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*). Katika utekelezaji wa mwaka 2011/12, Idara inakusudia kusambaza mitego 43,000 ya kunasia nzi dume wa matunda kwa kukamilisha Wilaya ya Mkoani kwa Pemba na Wilaya ya Kaskazini kwa Unguja. Aidha Idara inaendelea kuwahamasisha wakulima kudhibiti ongezeko la wadudu hawa kwa kufanya usafi wa mashamba na kuyazika matunda yote yanayoanguka chini ya miti.

Mhe. Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kupambana na inzi wa matunda, Wizara tayari imeshatoa mitego kwa vipindi tafauti Unguja na Pemba kama ifuatavyo:

**JADUELI: USAMBAZAJI WA MITEGO YA KUNASIA NZI  
WA MATUNDA**

<b>AWAMU</b>	<b>UNGUJA</b>	<b>PEMBA</b>	<b>JUMLA</b>
YA KWANZA (2009-2010)	17,020	5,000	22,020
YA PILI (2010-2011)	11,325	10,000	21,325
<b>JUMLA</b>	<b>28,345</b>	<b>15,000</b>	<b>43,345</b>

Mhe. Spika, pamoja utowaji huo wa mitego, Wizara hivi sasa inayo akiba ya mitego 21,675 ambayo inaendelea kusambazwa katika visiwa vya Unguja na Pemba hasa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkoa wa Kusini Pemba. Pamoja na hayo, Wizara inategemea kuagizia mitego mengine 35,000 ili kufikisha idadi ya mitego 100,000 ikiwa ni hatua ya kitaifa ya kupambana na kuangamiza kabisa nzi wa matunda nchini.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Idara pia imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuwaelimisha wakulima 1,500 juu ya mbinu za kilimo bora;
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabibishamba/mabwanashamba 120 juu ya mbinu bora za kilimo na Utafiti wa mazao ya chakula, biashara, usarifu wa mazao;
- Kuandaa ziara 12 za wakulima na mabibi/mabwanashamba ili kuweza kubadilishana utaalumu ikiwemo kuwapeleka katika maonyesho ya nane nane Tanzania Bara;
- Kutayarisha Makala 15 na vipeperushi 600 na kupatiwa wakulima;
- Kutayarisha vipindi 60 vya redio na 37 vya TV na kuvirusha hewani;
- Kununua gari tano kwa lengo la kufanikisha utoaji wa huduma za elimu kwa wakulima;
- Kuendeleza kazi za karantini na ukaguzi wa mazao;
- Kuzalisha na kusambaza tani 12 za mbegu za mahindi na mtama tani 5 na jamii ya kunde tani 8;
- Kununua na kusambaza mbolea tani 1,090 (545 TSP na 545 Urea);
- Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kushirikiana na wenye matrekta binafsi pamoja na kutengeneza matrekta mabovu 29 na zana zake;

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara iliendelea kusimamia mradi wa *PADEP* ambao umemaliza kupata mchango wa wahisani na kwa sasa unatekelezwa kwa fedha za SMZ pekee. (Kiambatisho. Na 10).

## **CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI**

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani ni taasisi yenye jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo na mifugo kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari na kufaulu masomo katika fani ya sayansi. Hivi sasa Chuo kimeanza kutumia mitaala ambayo imetayarishwa kwa mashirikiano na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi - *NACTE*. Mitaala hii itawawezesha wanafunzi kuhitimu mafunzo ya ngazi ya Diploma.

## **UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, Chuo cha Kilimo Kizimbani kilitekeleza yafuatayo:

- Mafunzo kwa wanafunzi 70 wa mwaka wa pili (wanawake 44 na wanaume 26) katika ngazi ya cheti "*General Agriculture Certificate*"
- Wanafunzi 74 wa ngazi ya cheti walisajiliwa;
- Wakufunzi wawili (2) walimaliza mafunzo ya shahada ya kwanza, fani za "*Rural Development*" na "*Development Studies*" katika Chuo Kikuu cha Sokoine na (*MSc –Training Centre for Development Cooperation*) Tanzania, Arusha;
- Wafanyakazi wa maktaba wawili (2) walipatiwa mafunzo ya ukutubi ngazi ya stahada (*Diploma in Record Management*) na cheti (*Certificate in Library*) katika vyuo vilioko Tanzania Bara;
- Chuo kilitekeleza mradi wa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga katika mabonde matatu (3) ya umwagiliaji maji kwa kushirikiana na Idara ya Umwagiliaji Maji pamoja na Mradi wa *TANRICE*;

## **MALENGO YA MWAKA 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo kimepanga kutekeleza yafuatayo:

- Kutoa mafunzo ya cheti kwa wanafunzi 140 wa mwaka wa kwanza;
- Ujenzi wa bweni la wanafunzi ambao unafadhiliwa chini ya Programu za *ASSP/ASDP-L* uko katika hatua za awali;

- Kutoa mafunzo kwa wakulima 500 katika mabonde matatu ya mpunga wa umwagiliaji;
- Kukamilisha usajili wa Chuo kwa Baraza la Vyuo vya Ufundi Tanzania (*NACTE*).

Mhe. Spika, Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa Chuo cha Kilimo Kizimbani tayari kimekamilisha taratibu zote za kuanzisha mafunzo katika ngazi ya Diploma na kuanzia mwaka wa fedha wa 2011/12 tunaanza kuchukuwa wanafunzi ambao watapatiwa mafunzo katika ngazi hiyo. Aidha kwa kuwa Serikali imedhamiria kukipandisha daraja chuo hiki na kuwa kitivo cha Kilimo cha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Wizara yangu tayari imeanza matayarisho ya kukijengea uwezo Chuo hiki hasa kwa kuwapatia walimu nafasi za Elimu ya juu ili waweze kuwa rasilimali watu inayohitajika kutoa mafunzo katika daraja hilo.

## **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO**

Mhe. Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kupanga na kutekeleza kazi za utafiti wa Kilimo na Maliasili kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi hii inajumuisha vituo vyote vya utafiti vilivyo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

## **UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, malengo ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo yalitekelezwa kupitia iliyokuwa Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima kama ifuatavyo:

- Jumla ya wakulima 135 katika wilaya tisa za Unguja na Pemba wamepatiwa aina 3 (*NERICA* 1, 10 na 12) za mbegu hizi kwa uzalishaji;
- Jengo la kufanyia uchunguzi wa maradhi ya mpunga limekamilika na limeanza kutumika;
- Utafiti wa kitaalam wa kutumia mionzi (*gamma rays*) umefanyika na mbegu aina tatu za mpunga zilizozimuliwa kwa mionzi hiyo zilipandwa kwa hatua ya mwanzo na hatua ya pili inaendelea;

- Tafiti za mbegu za mpunga aina 55 kutoka China zilifanyika pamoja na mbegu zetu za kienyeji, kati ya hizo mbegu 12 zimeonyesha kuzaa zaidi kuliko mbegu 3 za kienyeji.
- Uzalishaji na usambazaji wa aina 4 nne za mbegu mpya za muhogo zinazostahamili ukame uliendelea. Mbegu hizo ni *Kizimbani, Mahonda, Machui na Kama*;
- Jumla ya aina 34 za migomba ya kienyeji na ya kigeni zimefanyiwa uchunguzi;
- Mbegu aina 19 za viazi vikuu za kigeni na kienyeji zimekusanywa na kuhifadhiwa;
- Utafiti wa mbegu za mtama, ulezi, mahindi na zile za jamii ya kunde kutoka Tanzania bara zimefanyiwa ukaguzi kuangalia ustawi wake katika mazingira ya Zanzibar, utafiti huu bado unaendelea;
- Jumla ya miche 7,085 ya misitu, viungo na matunda imezalishwa na kuuzwa kwa wakulima;
- Jumla ya miche 9,913 ya minazi imezalishwa na kuuzwa kwa ajili ya kupandwa kwa msimu wa Vuli 2010 na Masika ya 2011;
- Mafunzo ya matumizi bora ya udongo na hifadhi ya mazingira kwa wakulima na wanafunzi wa skuli za msingi, sekondari na vyo vikuu pamoja na wakulima na wanafunzi 412 wa ndani na nje ya nchi yalitolewa.

## MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo;
- Kuzalisha mbegu mama za muhogo katika eneo la hekta 25 katika vituo vya utafiti;
- Kuchapisha makala za utafiti;
- Kufanya utafiti wa mbegu bora za mpunga, mazao ya mizizi na mbogamboga ili kupata mbegu mpya zitakazotoa mazao mengi zaidi.
- Kukarabati majengo, barabara na miundombinu mengine ya vituo vya Kizimbani Unguja na Matangatuani Pemba zikiwemo maabara ili kurudisha haiba ya vituo hivi na kuimarisha kazi za utafiti.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, taasisi hii itatekeleza programu ya kuendeleza utafiti wa kilimo na maliasili yenye malengo yafuatayo:

- Kujenga maabara za tafiti za mazao;
- Kujenga uwezo wa wataalamu wa tafiti;
- Kuongeza tafiti za mazao ya kilimo na maliasili;

## **IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE**

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kuratibu kazi za uhakika wa chakula na lishe ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa juu ya matukio yanayohusiana na hali ya uhakika wa chakula na lishe hapa nchini.

### **UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 kazi za uhakika wa chakula na lishe zilikuwa zikisimamiwa na Idara ya Sera na Mipango na kutekelezwa chini ya Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012 yameoneshwa katika **(Kiambatisho Na. 5)**

### **MALENGO KWA MWAKA 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuratibu masuala ya uhakika wa chakula na lishe.
- Kufanya upembuzi yakinifu (*feasibility study*) juu ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*National Food Reserve*);
- Kukamilisha Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo na kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sera
- Kuweka na kutekeleza mfumo wa kukusanya na kutoa taarifa ya Uhakika wa chakula nchini na tahadhari ya mapema (*Early Warning*);
- Kukarabati maghala ya akiba manne ikiwa ni matayarisho ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa.

Mhe. Spika, Hali ya lishe na utapiamlo hapa Zanzibar si ya kuridhisha hasa kwa watoto waliochini ya umri wa miaka mitano. Ingawa tathmini ya Hali ya Afya na Lishe Tanzania (*DHS, 2010*) imeonyesha unafuu kwa viashiria vya ukondefu (*wasting*) ambao umepungua kutoka asilimia 6.0 (2004/2005) hadi asilimia 3.7 (2010) na wepesi (*under weight*) umepungua kutoka asilimia 19 (2004/2005) hadi kufikia asilimia 12.1 (2010). Kiashiria cha kudumaa (*stunting*) kwa Zanzibar kimeongezeka kutoka asilimia 23 mwaka (2004/05) hadi asilimia 30.2 mwaka (2010). Hali hii inatokana na ukosefu wa lishe bora



kwa kipindi cha muda mrefu. Kwa kuzingatia hali hio, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeshaandaa na kuwasilisha rasmi maombi ya mradi wa Lishe bora unaotarajiwa kutekelezwa chini ya programu ya lishe ya *“Scaling Up Nutrition for First one thousand days of child”* inayofadhiliwa kwa pamoja Serikali ya Marekani na Ireland kupitia mpango mkuu wa *“Feed the Future”*

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara itaendelea kusimamia Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe ambayo malengo yake yameonyeshwa katika Kiambatisho Na. 5

## **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA**

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu ya asili, kuratibu upatikanaji wa maliasili zisizorejeshika kama vile mchanga, mawe na udongo na kuratibu upatikanaji wa mbegu na miche bora ya miti ya mazao ya biashara, matunda, misitu na mapambo. Idara pia inaratibu upatikanaji na kusimamia ustawi wa wanyama pori pamoja na makaazi yao.

## **UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:

- Jumla ya miche 830,300 ya matunda, viungo, mapambo na misitu iliotesywa na kusambazwa;
- Uhamasishaji wananchi katika kazi za upandaji miti umefanyika katika wilaya zote za Unguja na Pemba na upandaji miti kitaifa ulifanyika Bumbwini Mafufuni. Jumla ya miche 21,000 ilipandwa siku hiyo katika eneo la hekta tisa na asilimia 80 ya mbegu zilizopandwa zimeoota zote vizuri;
- Tathmini ya sera ya Taifa ya misitu ya mwaka 1995 imefanyika ambapo imependekezwa kwamba ifanyiwe mapitio;
- Jumla ya hekta 12 za misitu zimevunwa katika mashamba ya misitu ya serikali na jumla ya hekta 81.2 zimepandwa;
- Mafunzo ya kuwajenga uwezo wa uhifadhi wa misitu ya mikoko yametolewa kwa wanajamii 30 kwa kila Wilaya za Unguja na Pemba;
- Jumla ya wanafunzi 563 kutoka Skuli 29 za Zanzibar walitembelea katika hifadhi ya msitu wa akiba wa Kiwengwa-Pongwe;
- Wananchi 1,026 wameanza kutumia gesi kwa kupikia baada ya kupata gesi bila ya malipo yenye thamani ya Tsh. 119,617,000;

- Jumla ya vikundi 52 vya ufugaji wa nyuki na wafugaji 1,481 wamepatiwa mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki kwa Unguja na Pemba.

## **MALENGO YA MWAKA 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara imepanga kutekeleza yafuatayo:

- Kuzalisha miche 1,000,000 ya matunda, viungo, misitu na mapambo;
- Kuanza utaratibu wa kupandisha hadhi ya Msitu wa Hifadhi ya Masingini na Msitu wa Muyuni – Jambiani;
- Kupeleka huduma za gesi ya kupikia Pemba;
- Kuanza kuhifadhi vianzio vya maji vilivyomo nje ya misitu ya hifadhi;
- Kupanda miti ya misitu katika eneo la hekta 80 na kuvuna mita za ujazo 3,000 kwenye mashamba ya Serikali;
- Kuandaa na kutekeleza mipango ya misitu ya vijiji;
- Kufanya mapitio ya Sera na Sheria ya Misitu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Mradi wa HIMA kwa ufadhili wa Norway unaendeleza kazi ya kuhamasisha matumizi ya gesi. Hali halisi ni kwamba wastani wa asilimia tisini (90%) ya watu wa Zanzibar wanatumia kuni na makaa kwa kupikia. Mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi milioni mia tatu kwa mwaka kwa ajili ya kununulia gesi ambayo hutolewa bure kwa watumiaji wanaoanza ili kunusuru na kupunguza utumiaji wa misitu michache iliyobaki hapa Zanzibar. Katika kipindi cha mwaka mmoja wa majaribio ya mradi huo, wananchi 1,026 wa Unguja tayari wamehamasika kwa kuanza kutumia gesi badala ya makaa na kuni.

Aidha, mradi tayari umepeleka gesi Pemba na umeanza kuhamasisha matumizi ya majiko ya gesi kuanzia mwezi wa Julai 2011. Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili katika kuihami misitu yetu, Serikali imeanza kuchukua hatua za awali za kuangalia uwezekano wa kuondosha kodi katika majiko ya gesi na vifaa vyake ili kushajiisha matumizi ya nishati mbadala. Nachukua fursa hii kuwataka wananchi wote kuanza kuacha kupikia kuni na makaa na kutumia nishati mbadala kama ilivyo agizwa katika *MKUZA II*.

## **MIRADI NA PROGRAMU**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara itasimamia miradi mikuu mitatu ambayo ni :

- Mradi wa Mpango wa Taifa wa Uimarishaji Mikarafuu  
(**Kiambatisho Na. 7**)
- Mradi wa Hifadhi Misitu ya Asili (*HIMA*) (**Kiambatisho Na. 8**)
- Mradi wa Hifadhi wa Misitu ya Ukanda wa Pwani(**Kiambatisho Na.9**)

## **IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI**

Mhe. Spika, naamini Wajumbe wa Baraza hili watakubaliana nami kwamba kilimo cha umwagiliaji maji ndio mkombozi wetu kwa kilimo cha mpunga na umuhimu wake umezidi kuwa mkubwa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa yanayotokea duniani kote na kukifanya kilimo cha kutegemea mvua kutokuwa cha uhakika na cha kutegemewa. Ni ukweli uliowazi kuwa tunahitaji kujipanga vyema na kukiimarisha kilimo hiki ili nchi yetu iweze kujihakikishia uhakika wa chakula na kupunguza uagizaji. Hapa ndipo ulipo mwelekeo wa Mapinduzi ya Kilimo. Hapa ndipo uwekezaji mkubwa wa Serikali, sekta binafsi na wakulima unapohitajika.

Mhe. Spika, Idara ya Umwagiliaji maji ina majukumu ya kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kiufundi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji katika utekelezaji wa kazi za kila siku za utunzaji wa vianzio vya maji, uendeshaji wa kilimo cha umwagiliaji na katika utoaji wa huduma za elimu na pembejeo za kilimo kwa wakulima.

## **UTEKELEZAJI WA MALENGO 2010/2011**

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi za umwagiliaji maji Idara ilitekeleza mambo yafuatayo:

- Kazi ya uwekaji Umeme katika mabonde ya Bumbwisudi na Cheju imekamilika;
- Visima viwili vimechimbwa katika bonde la Mtwango;
- Ujenzi wa matuta ya msingi wa kumwagilia maji mita 500 Kibokwa na mita 480 Mtwango umekamilika;
- Transfoma imenunuliwa kwa matumizi ya bonde la Makombeni;

- Ujenzi wa mita 500 za mitaro Cheju, Bumbwisudi mita 445 na Kibokwa mita 500 umekamilika.
- Ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji maji umefanyika kwa eneo lenye ukubwa wa ekari 205, ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima, mitaro ya kutolea maji, ununuzi wa pampu na transfoma: Tunduni ekari 40, Bumbwisudi ekari 45, Kianga ekari 35, Jendele ekari 45, Machigini ekari 20, Tungamaa ekari 20;
- Vishamba vya maonesho ya umwagiliaji maji wa matone vimetayarishwa Mpapa, Kitogani, Jendele na Bumbwini kwa Unguja na Micheweni na Pujini kwa Pemba, ambapo jumla ya ekari 2.5 zimetumika;
- Ujenzi wa bwawa na mtaro 100m umefanyika katika kituo cha Kinyakuzi na ujenzi wa tuta la msingi mkuu 500m Koani.

## **MALENGO KWA KIPINDI CHA 2011/2012**

Mhe. Spika, Wizara yangu imekusudia kuutekeleza kwa ukamilifu Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji ambao unajibu hoja na changamoto zote za kilimo hicho. Nachukua fursa hii kuliarifu Baraza hili kwamba tayari tumeshafanya mazungumzo na washirika wa maendeleo ambao wameonyesha nia ya kutusaidia hasa katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji wakiwemo *EXIM BANK* – Korea (hekta 2105), *USAID* (hekta 2000), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (*TASAF* – hekta 280) na miradi ya *JICA* (hekta 720). Ni Matarajio ya Wizara yangu kwamba kupitia miradi hii tutakuwa tumekamilisha ujenzi wa miundombinu hekta 5,805 ifikapo mwaka 2016 ambazo ni sawa na asilimia 68 ya maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji kama yalivyohakikiwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Umwagiliaji maji imelenga kutekeleza Mpango Maalum wa kuimarisha zao la mpunga kwa upande wa miundombinu ya umwagiliaji kama ifuatavyo:

- Kusimamia ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji kwa ekari 237 ili kufikisha jumla ya eneo la kilimo cha umwagiliaji la ekari 1987 Unguja na Pemba; Miundombinu hii itajengwa kupitia miradi ya *TASAF* katika mabonde ya Bumbwisudi, Kisima Mchanga, Kilombero na Kikobweni; na kupitia miradi ya *JICA* katika mabonde ya Koani, Ubago, Kwajibwa na Kiboje Mwembeshauri.
- Kujenga mtaro mkuu wa mita 500, kujenga matuta katika ekari 25 bonde la Koani;

- Kukamilisha uwekaji wa umeme katika kituo cha Saninga, Mtwango na Makombeni;
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabwana/mabibishamba 40 Unguja na Pemba;
- Kusomesha wafanyakazi wawili Msc na wanane kwa kiwango cha Diploma;
- Kutoa mafunzo kwa wakulima 120 wa bonde la Kibokwa;
- Kutayarisha vishamba 10 vya maonesho ili kuongeza taaluma kwa wakulima wa mpunga na mbogamboga katika mabonde ya umwagiliaji maji;
- Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika maeneo mawili ya vituo vya uzalishaji mbegu ekari 65 ambapo Kibonde Mzungu ekari 40 na Ole ekari 25.

## **AFISI KUU PEMBA**

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na Idara zilizomo katika wizara hii. Mwaka 2010/2011, kazi zilizotekelezwa na Afisi Kuu Pemba ni miongoni mwa kazi zilizokwishwa elezwa na kila idara.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi Kuu Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya Sh. 1, 458, 374,710 na hadi kufikia mwezi Aprili, 2011, jumla ya Sh. 1,256,516,085 zilikwishatolewa na Serikali, sawa na asilimia 86.16 ya lengo. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi Kuu Pemba imepangiwa kutumia jumla ya Sh. 1, 388, 302,000

## **CHANGAMOTO ZA WIZARA**

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Wizara ya Kilimo na Maliasili bado tunakabiliwa na changamoto ambazo zinadhoofisha utendaji wa wizara katika kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kuondoka/kuhama kwa wataalamu kutokana na maslahi duni;
- Uhaba wa matumizi ya teknolojia bora na za kisasa katika kuendeleza kilimo
- Mabadiliko ya tabia nchi duniani;
- Kuongezeka kwa wadudu waharibifu na maradhi ya mimea;
- Uvamizi wa maeneo ya kilimo na misitu;

- Ongezeko kubwa la mahitaji ya mazao ya maliasili kuliko uwezo wa uzalishaji;
- Gharama ya nishati mbadala ya kupikia bado ni kubwa kutokana na kodi.
- Upungufu wa nguvu kazi ya vijana katika sekta ya kilimo;
- Kuongezeka kwa wizi wa mazao mashambani;
- Gharama kubwa za pembejeo za kilimo.

Mhe. Spika, pamoja na changamoto hizi wizara inaendelea kutafuta mbinu za kukabiliana nazo.

## **MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2010/2011**

### **Makusanyo ya Mapato 2010/2011**

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ilikadiriwa kukusanya jumla ya Sh. 244,900,000. Hadi kufikia Aprili, 2011 wizara imekusanya jumla ya Sh. 212,013,950 sawa na asilimia 86.57 ya makadirio ya lengo (**Kiambatisho 11**).

### **MATUMIZI YA FEDHA 2010/2011**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya Sh. 5,837,781,710 kwa kazi za kawaida na Sh. 271, 560,000 ikiwa ni ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2011. Kwa kazi za kawaida wizara imepata Sh. 4,805,227,581 ambayo ni sawa na asilimia 82.3 ya fedha zilizoombwa na Chuo cha Kilimo kimepata Sh. 163,500,000 sawa na asilimia 60.1 (**Kiambatisho 12**).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya Sh. 8,578,132,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh. 1,391,000,000 kutoka SMZ na Sh. 7,187,132,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo na kufanya jumla ya Sh. 14,687,473,710. Fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2011 jumla ya Sh.1,059,000,000 zimepatikana ikiwa ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 76.13. Mchango wa washirika wa maendeleo kufikia Aprili, 2011 wizara imepokea jumla ya Sh. 2,296,067,287 ambazo ni sawa na asilimia 31.95 ya fedha zilizo idhinishwa. (**Kiambatisho 13**).

## **MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Kilimo na Maliasili inakadiriwa kukusanya Sh. 238,500,000. Aidha, wizara kwa mwaka wa 2011/2012 inakadiriwa kutumia Sh. 15,306,631,000 kati ya hizo Sh. 6,623,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na Sh. 500,000,000 ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani na Sh. 3,600,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali na kwa upande wa washirika wa maendeleo Sh. 4,583,631,000.

Mhe. Spika, bajeti niliyoisoma imetoa mchanganuo wa mambo ambayo wizara yangu inakusudia kuyatekeleza kwa mwaka huu wa fedha ili kuondoa vikwazo vingi vinavyo wakabili wakulima na kuelekea kwenye mafanikio ya sekta hii. Nawaomba wakulima wazitumie kikamilifu fursa nilizozieleza katika bajeti hii ili kuleta mabadiliko makubwa katika tija na uzalishaji wa kilimo na katika utunzaji na usimamizi wa maliasili zetu kwa manufaa ya wakulima na nchi yetu.

## **SHUKRANI**

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar napenda kutoa shukurani za dhati kwa Serikali, Mashirika ya nchi zifuatazo: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Korea Kusini, Jamhuri ya Kiislamu ya Irani, Japan, Misri, China, Finland, Ujerumani, Norway, Uholanzi, Austria, Marekani, Uingereza. Aidha, napenda kuzishukuru Taasisi na Washirika wa Maendeleo wakiwemo:- *AGRA, FAO, Benki ya Dunia, FFI, IFAD, AfDB, KOICA, JICA, USAID, UNDP, WFP, IAEA, WCS, GEF, IITA, ACTION-AID, GLOBAL FUND, UNICEF, DANIDA*, Pia tunazishukuru Jumuiya za *EAC, EU, SADC* pamoja na Wizara za *SMZ* na Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazosaidia katika maendeleo ya sekta hii.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na upendo naomba kuchukua fursa hii, kuwapongeza: Katibu Mkuu wa wizara yangu ndugu Afani Othman, Manaibu Makatibu Wakuu ndugu Juma na Dk. Aseid, Ofisa Mdhamini – Pemba Dk. Suleiman, Wakurugenzi, Wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara Unguja na Pemba kwa kazi nzuri wanaozifanya kwa ufanisi wa hali ya juu pamoja na mazingira magumu wanayofanyia kazi. Pia, nawapongeza Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Wawakilishi, Wakuu wa Wilaya, Masheha, wakulima na jumuiya zao kwa kazi zao nzuri za kuleta maendeleo katika Sekta ya Kilimo na Maliasili. Aidha, navipongeza vyombo vyote vya habari kwa utoaji wa habari

za Sekta ya Kilimo. Matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana katika kufanikisha maendeleo ya kilimo na hifadhi ya maliasili hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, shukurani za pekee zimwendee Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali pamoja na wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Upiga Chapa kwa kufanikisha uchapaji wa hotuba hii, na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za wizara yetu. Mwisho napenda kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu.


## **HITIMISHO**

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, waijadili na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na kutupatia maoni, maelekezo na ushauri wao juu ya kuiendeleza sekta hii kwa manufaa ya taifa letu, wakulima na washirika wengine wa sekta hii. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinisha jumla ya Sh. 15,306,631,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2011/2012. Kati ya fedha hizo, Sh. 6,623,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Sh. 500,000,000 ni ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani na Sh. 8,183,631,000 kwa matumizi ya kazi za miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

## **KIAMBATISHO 1: UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA MWAKA 2006 - 2010**





**Kiambatisho 2: Idadi ya Wafanyakazi Waliokamilisha Mafunzo kwa Mwaka 2010/2011**

Nam	AINA YA MAFUNZO	JINSIA		JUMLA
		MUME	MKE	
1.	PhD	1	0	1
2.	Shahada ya Pili (MSc)	5	2	7
3.	Shahada ya Kwanza (Bsc)	5	4	9
4.	PGD	2	0	2
5.	Diploma	4	14	18
6.	Cheti	9	13	22

	<b>JUMLA</b>	<b>26</b>	<b>33</b>	<b>59</b>
--	--------------	-----------	-----------	-----------

**N.B.** Jumla ya wafanyakazi 31 wamepatiwa nafasi za masomo ya muda mfupi.

### **Kiambatisho 3: Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo (ASSP)**

#### **Maelezo Mafupi ya Programu:**

Programu hii imeanza Januari 2007 ikiwa na madhumuni ya kuwawezesha wakulima kupata na kutumia utaalamu na teknolojia za kilimo ambazo zitaongeze uzalishaji, kipato na uhakika wa chakula. Programu hii inatekelezwa katika Wilaya tisa za Unguja na Pemba.

**Gharama:** USD 5.9 milioni

**Wachangiaji:** SMZ 22%, IFAD 77.1 %, Walengwa 0.7%

**Lengo Kuu:** Kuinua hali ya maisha ya wakulima kwa kuongeza uzalishaji wenye tija, kuongeza kipato, uhakika wa chakula na kupunguza umaskini

**Gharama kwa mwaka 2010/2011: Programme** IFAD US Dola 664,845.48, SMZ Tshs. Tshs.200,000,000 na Walengwa Tshs.8,985,516

#### **Utekelezaji wa Malengo 2010/2011:**

- Vikundi 360 vya skuli za wakulima, kaya 6,300 viliendelea kupewa taaluma ya uzalishaji na kuhitimu na vikundi 20 vilivyoibuka nje ya skuli za wakulima vilipewa mafunzo. Programu pia imeanzisha vikundi vipya 260 na kuvihudumia;
- Ziara za kimafunzo zilifanyika Mkoa wa Pwani ambapo wakulima 13 wa muhogo kutoka Unguja na Pemba (8 wanaume na 5 wanawake) walitembelea wenzao kwa madhumuni ya kujifunza na kubadilishana mawazo juu ya mbinu za kilimo bora cha muhogo na namna ya usarifu. Pia wakulima watano (5) kutoka Pemba walifanya ziara ya kuja Unguja kutembelea wakulima wenzao wa maeneo ya maweni;
- Utafiti wa zao la muhogo umefanyika kwa kushirikisha vikundi vinane (8) vya wakulima wa muhogo kwenye maeneo yao;
- Mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wawili (2) katika ngazi ya shahada yamefanyika;
- Mpango Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Mifugo kwa shehia 3 za Unguja na 2 Pemba umeandaliwa.

**Gharama kwa mwaka 2011/2012:** SMZ: Tshs 126,083,000, IFAD. USD 314,628.63, walengwa Tshs.4,830,652.

**Malengo ya Mwaka 2011/2012:**

- Kuendelea kuwapatia mafunzo wakulima katika fani za SACCOS na usarifu wa mazao;
- Kujenga Bweni katika Chuo cha Kilimo Kizimbani;
- Kupeleka wakulima 180 katika ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara;
- Kuimarisha shughuli za utafiti katika vituo vya Utafiti na mashamba ya wakulima;
- Kuwapa mafunzo 26 ya muda mfupi wafanyakazi wa Programu;
- Kuwahamasisa wakulima kujiunga katika vikundi vya uzalishaji na masoko.

**Kiambatisho 4: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo- Mifugo (ASDP-L)****Maelezo Mafupi ya Program:**

Programu hii imeanza Januari 2007 ikiwa na madhumuni ya kuwawezesha na kuwaendeleza wafugaji ili kuinua kipato na kupunguza umaskini. Programu inatekelezwa katika wilaya tisa za Unguja na Pemba ikianzia na Shehia kumi kwa kila wilaya.

**Gharama za mradi:** USD 3.76 milioni

**Wachangiaji:** SMZ (6.1%), IFAD (93 %) WALENGWA (0.9%)

**Lengo Kuu:** Kupunguza umaskini, kuongeza uhakika wa chakula na kuongeza kipato cha wafugaji.

**Gharama kwa mwaka 2010/2011:**

*IFAD* US DOLA 725,777.67, *SMZ* Tshs. 95,000,000, walengwa shilingi 13,072,540

### **Utekelezaji 2010/2011**

- Vikundi 174 vya skuli za wafugaji vilipatiwa taaluma ya ufugaji, pamoja na vikundi 10 vilivyoibuka nje ya skuli za wafugaji;
- Dozi 3,000 ya chanjo dhidi ya magonjwa ya mahepe zimenunuliwa na kuku katika Shehia zote zinazofanya kazi na Programu wamepatiwa chanjo;
- Ukarabati wa vituo 3 na maabara 2 za mifugo umeanza;
- Jumla ya wafugaji wa ng'ombe 33 walipata mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na maziwa na wafugaji wanane (8) walipatiwa ziara za kimafunzo Mkoa wa Kilimanjaro kujifunza usarifu wa maziwa;
- Mashine 10 za kusarifia maziwa zimenunuliwa kwa na kukabidhiwa wafugaji;
- Uchunguzi wa kina juu ya maradhi ya kuku na vifo vya vifaranga ulifanyika Pemba kwa kusaidiana na mtaalamu wa mifugo kutoka Kenya;
- Watoa huduma za msingi kwa wafugaji wamepatiwa mafunzo, vifaa pamoja na mbegu ili waweze kuwasaidia wafugaji vijijini juu ya uchunguzi wa maradhi ya mifugo.

**Gharama ya mwaka 2011/2012:** SMZ 50,957,000; *IFAD:* USD 476,489.82  
na Walengwa: TShs. 20,083,274

### **Malengo ya mwaka 2011/2012**

- Kuendelea kuvipa taaluma vikundi 360 vya skuli za wakulima/wafugaji pamoja na vikundi 30 vilivyoibuka venyewe;
- Kuvipatia mafunzo ya *SACCOS*, vikundi 360 vya skuli za wakulima/wafugaji;
- Kuendeleza mabaraza ya wakulima na vituo vya upashanaji habari katika Wilaya tisa (9) kwa kuwapatia taaluma na nyezo,
- Kuanzisha skuli 360 nyengine za wakulima katika Wilaya zote za Unguja na Pemba;
- Kuwapatia mafunzo wawezeshaji 180 wakulima/mifugo;
- Kutoa mafunzo kwa wapandishaji 10 wa mbuzi;
- Kuendelea ukarabati wa vituo na maabara za mifugo na kununua vifaa vya maabara;
- Kufanya ukarabati kituo cha machinjio Kisakasaka;
- Kununua chanjo 1,500 za mahepe na kuzigawa katika Shehia 90 zinazotekeleza program;
- Kununua dozi 40 ya chanjo ya vibuma kwa ndama 1600;
- Kuwapatia wafugaji 180 ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara;

- Kusaidia kuweka mitambo mitano ya *Gas* kwa wafugaji;
- Kuwahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi vya uzalishaji na masoko.

### **Kiambatisho. 5: Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe**

**Programu:** hii ni ya miaka mitano na imeanza 2009

**Gharama:** *USD* 15 Million katika awamu ya Miaka mitano ya mwanzo

**Wachangiaji:** SMZ, *FAO*, *UNDP* na Serikali ya Ujerumani

#### **Lengo Kuu:**

Lengo kuu la Programu hii ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umasikini wa chakula na kipato, kukabiliana na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za Taifa, jamii na kaya na kushajiisha ushiriki wa jamii katika hatua za kujiongezea kipato, kuondoa njaa na kufikia hali ya kila mtu kuwa na haki ya kula na kushiba.

#### **Gharama Mwaka 2010/2011:**

Kwa mwaka 2010/2011 Pragamu iliombewa Sh. 200,000,000 kutoka SMZ, *USD* 102,000 kutoka JP5 na *USD* 50,000 kutoka Serikali ya Ujerumani. Hadi kufikia Aprili, 2011 fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Sh.200,000,000, kutoka JP5 ni *USD* 70,000 na kutoka Serikali ya Ujerumani ni *USD* 20,000.

#### **Utekelezaji 2010/2011**

- Idara ilisimamia ukamilishaji wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Aidha, rasimu hii ya sheria tayari imeshapitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;
- Katika kuendeleza uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mbegu bora ya mpunga, Programu ilinunua tani 51 za mbegu ya mpunga kutoka kwa wakulima ambao Wizara iliingia nao mkataba, jumla ya wakulima 175 walinufaika na mpango huo Unguja na Pemba (wanaume 60 na wamawake 115). Programu pia ilisaidi uzalishaji wa mbegu mama na mbegu ya msingi ya mpunga aina ya Supa na NERICA. Kazi hizi zilifanyika katika vituo vya utafiti Kizimbani na Bambi. Aidha, kwa kushirikiana na Kitengo cha Uzalishaji Mbegu, Programu ilisambaza mbegu bora ya mpunga kwa kutumia magari maalumu. Kazi hii ilifanyika kwa lengo la kumrahisishia mkulima upatikanaji wa mbegu bora na hatimaye kuongeza matumizi ya mbegu bora;
- Programu ilitoa mafunzo kwa Timu ya Uongozi za Wilaya (*DMT*) katika Wilaya za Chake Chake na Kusini, juu ya utayarishaji wa mipango kazi ya Wilaya (*District Food Security and Nutrition Action Plan*) kwa kuzingatia

dhana nzima ya uhakika wa chakula, lishe na utawala bora. Lengo kuu la mafunzo hayo ni kujenga uwezo wa watumishi wa Wilaya katika kutayarisha mipango kazi na kusimamia utekelezaji wake. Mipango kazi hiyo hivi sasa ipo katika hatua za mwisho kukamilika na hatimaye itawasilishwa na kujadiliwa katika ngazi za utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe;

- Programu ilianzisha Kamati za Uhakika wa Chakula na Lishe katika Shehia za Kizimkazi Dimbani na Jambiani Kikadini kwa Wilaya ya Kusini Unguja na Mbuzini na Pujini kwa Wilaya ya Chake Chake Pemba. Kamati hizi zitakuwa na jukumu la kusimamia miradi na kazi zinazohusiana na uhakika wa chakula na lishe katika shehia zao. Kamati tayari zimepatiwa mafunzo ya awali juu ya masuala ya uhakika wa chakula na lishe na mpango wa baadae ni kujenga uwezo wa kamati hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Aidha, baada ya kupata mafunzo ya awali, Kamati zilipata fursa ya kubuni miradi ya maendeleo katika shehia zao na tayari imeshawasilishwa *TASAF* kwa ajili ya kuombewa ufadhili;

#### **Gharama Mwaka 2011/2012:**

Programu inatarajia kupata Shilingi 721,500,000 kutoka SMZ, USD 50,000 kutoka Serikali ya Ujerumani.

#### **Malengo Mwaka 2011/2012**

- Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mashamba ya kuzalisha mbegu yaliopo Kibonde Mzungu (ekari 40) na Bambi (ekari 10) kwa Unguja na Ole (ekari 25) kwa Pemba. Mashamba haya yanatarajiwa kutumika kwa uzalishaji wa mbegu bora za mpunga ikiwemo mbegu ya NERICA iliyozalishwa hivi karibuni;
- Kusambaza na kushajiisha matumizi ya mbegu bora za mpunga kwa wakulima. Aidha, Programu inatarajia kuanzisha mfumo wa kutoa zawadi kwa wakulima watacao tumia mbegu bora na watakaoshawishi wakulima wenzao juu ya matumizi ya pembejeo bora za kilimo na wataopata mazao mengi na bora watazawadiwa;
- Kwa kushirikiana na Kitengo cha Uzalishaji Mbegu, Programu itaendeleza mpango wa kuwashirikisha wakulima katika uzalishaji wa mbegu bora ya mpunga kwa kutoa mafunzo na kufunga nao mikataba ya uzalishaji wa mbegu;
- Kuandaa warsha kwa wadau ili kuongeza uelewa juu ya Sera na Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe na dhana ya Haki ya chakula;
- Kuendeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini (M&E) wa masuala ya

uhakika wa chakula na lishe;

- Kuendeleza mafunzo kwa Kamati za Uhakika wa Chakula na Lishe katika Shehia za Kizimkazi Dimbani na Jambiani Kikadini kwa Wilaya ya Kusini Unguja na Mbuzini na Pujini kwa Wilaya ya Chake Chake Pemba. Mafunzo hayo yatalenga katika kujenga uwezo wa Kamati hizo katika kufanya uchambuzi wa hali halisi ya uhakika wa chakula na lishe, kuandaa miradi ya maendeleo, kutafuta fedha za kutekeleza miradi hiyo kutoka kwa washirika wa maendeleo wa ndani na nje na kushajiisha maendeleo ya kilimo na lishe bora katika shehia zao. Sambamba na hayo, programu pia inalenga kuanzisha kamati kama hizo katika shehia mpya za Wilaya hizo teule (*piloting districts*);
- Kutoa mafunzo kwa *DMT* juu ya masuala ya uhakika wa chakula na lishe na kutayarisha mipango kazi katika wilaya za Mkoani na Wete kwa Pemba na Wilaya za Kati na Kaskazini A kwa Unguja.

### **Kiambatisho. 6: Mradi wa Usarifu wa Mazao ya Kilimo**

**Muda wa Mradi:** Miaka mitatu, (Julai 2010/Juni 2013)

Gharama/Wachangiaji.: KOICA: US \$ 2.300 milioni SMZ TSh 600 milioni

**Lengo kuu:** Kujenga uwezo wa wakulima juu ya usarifu wa mazao na ujasiriamali pamoja na udhibiti wa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wataalamu.

Gharama kwa mwaka 2010/2011: Sh.s. 190,000,000/= SMZ

#### **Utekelezaji 2009/2010:**

- Transfoma moja kubwa imefungwa kwa ajili ya matumizi ya Kituo cha Mafunzo ya Uchumi
- Ujenzi wa Jengo la Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa Mazao umeendelea na kwa sasa uyezekaji;
- Ukarabati wa njia ya kuingilia eneo la ujenzi (*Access road*) umefanyika kwa kuelewa
- Kuingiza mambo yanayohusu usarifu na kuongeza thamani ya mazao katika miradi hizo kutekelezwa na Wizara ili kutanua wigo wa mradi uliopo sasa;

Gharama kwa mwaka 2011/2012: US\$ 800,000 KOICA na SMZ Sh. 211,700,000

**Malengo ya mwaka 2011/2012:**

- Kukamilisha ujenzi wa jengo la kituo cha kusarifia mazao;
- Kutoa mafunzo kazini kwa wafanyakazi juu ya matumizi na matengenezo ya vifaa na kuzalishia bidhaa;
- Kutoa mafunzo ya usarifu kwa wajasiriamali 100 pamoja na kuandaa ziara za kimara mradi na wazalishaji;
- Kuendelea Kuandaa miradi mipya itakayosaidia kutanua wigo (*scope*) wa mradi uliopo mradi na wazalishaji;
- Kukamilisha njia ya kuingilia eneo la ujenzi (*Access road*) kwa kiwango cha kifusi.

**Kiambatisho. 7: Mradi wa Uimarishaji Mikarafuu****Gharama:**

Uingiaji: SMZ na Shirika la ZSTC

**Malengo vya Mradi:**

- Kuotesha miche ya mikarafuu ili kutosheleza mahitaji ya wakulima
- Kutoa elimu ya kilimo mchanganyiko cha karafuu na mazao ya viungo

**Malengo ya mwaka 2010/2011:**

• Kutoa Tshs 80,000,000/- kutoka SMZ.  
• Malimizi ilizotolewa ni 30,000,000 sawa na asilimia 37.50 ya lengo

**Malengo ya mwaka 2010/2011**

- Kuzalisha miche 300,000 ya mikarafuu.
- Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mikarafuu, uvunaji na uanikaji.
- Kufanya utafiti wa vifo vya mikarafuu midogo.
- Kufahamisha wakulima kupanda mikarafuu na kuhudumia
- Kujengea uwezo wananchi kuongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na karafuu.

**Malengo ya mwaka 2010/2011**

- Kutoa miche 239,600 sawa na asilimia 80 ya lengo;
- Kufanywa matengenezo ya mabanda 5 ya miche ya vitalu yalifanyika Pemba na kuchimba kisima katika kituo cha miche ya mabanda yanyanya;
- Kutoa miche ya kilimo bora cha mikarafuu imetolewa katika vipindi viwili vya redio na TV;

**Malengo ya mwaka 2011/2012:** 300,000,000/=

**Malengo ya mwaka 2011/2012**

- Kuzalisha miche 200,000 ya mikarafuu;



fanya matengeneza ya mabanda 10 ya kuzalisha miche ya mikarafuu;  
toa elimu ya upandaji na utunzaji wa mikarafuu wilaya 7 za Unguja na Pemba;  
fanya tathmini ya mikarafuu iliyopandwa baada ya msimu;  
fanya sense ya Mikarafuu.

### **Kiambatisho. 8: Mradi wa Hifadhi Misitu ya Asili (HIMA)**

**Programa:** USD 5,539,175 na Muda wa Mradi ni miaka minne

**Changiaji:** Serikali ya Norway

**Malengo kuu:** Kupunguza Hewa Mkaa kutokana na Ukataji wa Miti ovyo na Uharibifu wa Misitu – Zanzibar na Pemba  
ngeza kipato kwa jamii ambacho kitatokana na kutunza misitu ya asili.

#### **Malengo vya Mradi:**

- Kutayarisha na Kupitia Mipango ya Usimamizi wa rasilimali za misitu;
- Kuwajenga uwezo wadau wa Uhifadhi;
- Kupunguza na kudhibiti ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa ardhi.  
Kusambaza miche 750,000 (300 ha) ya miti kwa wanajamii Unguja na Pemba ili kupunguza matumizi  
misitu ya asili.

**Malengo kwa mwaka 2010/2011:** USD 1,124,350

#### **Malengo wa malengo kwa mwaka 2010/2011:**

- Mradi umeweza kutayarisha muongozo wa kutoa mwelekeo wa utayarishaji wa mipango ya usimamizi  
rasilimali za misitu;
- Mipango ya matumizi imefanyiwa mapitio katika vijiji vya Mtende na Ukongoroni (Unguja) Mjimbiri  
Mtambwe kusini (Pemba);
- Mipango 4 mipya imeanza kutayarishwa ikiwa pamoja na Kajengwa na Uzi Ng'ambwa (Unguja) na  
Kiuyu na Mkia wa Ng'ombe (Pemba).
- Miche 957,000 (382.8 ha) ya miti ya misitu imesambazwa kwa wanavijiji wa Unguja (526,000) na Pemba  
(428,000).

**Malengo kwa mwaka 2011/2012:** USD 1,077,716

#### **Malengo kwa mwaka 2011/2012**

- Kuendelea na mapitio ya mipango ya usimamizi wa rasilimali za misitu ya jamii;
- Kuelimisha jamii kuhusu MKUHUMI hadi katika ngazi za Wilaya;
- Kusaidia jamii kuanzisha mashamba ya misitu hekta 100 ili waweze kujipatia mahitaji yao;
- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 15 wa Idara ya Misitu na Maliasili yanayohusu  
MKUHUMI na mabadiliko ya tabia ya nchi;
- Kufanya utafiti na mabadiliko ya tabia nchi hapa Zanzibar ili kutambua athari ambazo zimejitokeza  
Zanzibar;

- Kufanya utafiti wa kujua matumizi makuu ya misitu kwa jamii na upotevu wa misitu ili kuandaa mikaa ya kusaidia jamii kiuchumi ili kupunguza matumizi ya misitu ya asili;
- Utoaji wa gesi bure kwa wananchi wanaotaka kuachana na matumizi ya kuni na mikaa.

**Kiambatisho. 9: Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani**

**Ukanda:** USD 900,500 na Muda wa Mradi ni miaka minne

**Chaji:** Global Environment Fund (GEF)

**Ujumbe:** kuweka mtandao wa misitu ya Hifadhi na kupandisha hadhi misitu ya Jamii

**Ufafanuzi wa Mradi:**

kuwawezesha wanavijiji kupanga mipango shirikishi na endelevu ya matumizi ya misitu inayowazunguka kuujiunga kwa kusimamia na kuimarisha maeneo ya Misitu ya Hifadhi za Taifa

**Ukanda mwaka 2010/2011:** Tsh. 116,111,000

**Ufafanuzi kwa mwaka 2010/2011**

kuuzindua na kutambulisha mradi kwa watendaji na wadau husika  
 kuununua vifaa na vitendea kazi muhimu

**Ufafanuzi wa Malengo kwa mwaka 2010/2011**

Mradi tayari umezinduliwa  
 Inunuzi wa Komputa desk top 2, lap top 2 na printer 1 zimenunuliwa;  
 Komputa desk top 1, lap top 2 zimenunuliwa.

**Ukanda mwaka 2011/2012:** Tsh. 731,580,000

**Ufafanuzi kwa mwaka 2011/2012**

kuweka mipaka ya kudumu katika maeneo ya misitu ya Hifadhi ya Kiwengwa, Masingini, Ras Kiuyu na Mkuu;  
 kuanzisha utaratibu wa kuupandisha hadhi Msitu wa Hifadhi ya Masingini kuwa Hifadhi ya Kimaumbile na  
 kufanya matayarisho ya kuutangaza Msitu wa Muyuni-Jambiani kuwa Misitu wa Hifadhi;  
 kuimarisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka;  
 kutayarisha na kutekeleza mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Hifadhi wa Masingini na kuipitia mipango  
 usimamizi ya Hifadhi za Ngezi, Kiwengwa-Pongwe, na Jozani na Ghuba ya Chwaka.

**Kiambatisho.10: Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezesaji (PADEP)**

**MRADI WA PADEP**

**Gharama:** US \$ 9.605 milioni

**Wachangiaji:** 1. IDA: US \$ 7.942 milioni 2. SMZ na Walengwa: US \$ 1.663 milioni

**Lengo kuu:** Kujengea wakulima uwezo wa kitaaluma ili waweze kutambua matatizo yao na kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija na kushajiisha sekta binafsi kushiriki katika kutoa h

**Gharama kwa mwaka 2010/2011** SMZ Sh. 166,000,000

**Utekelezaji wa Malengo kwa mwaka 2010/2011**

- Miradi ya wanajamii katika Shehia 121 imefuatiliwa na kutolewa maendeleo utekelezaji wake.
- Uhakiki wa Ripoti ya Mwisho ya Utekelezaji wa Mradi (Implementation Completion Report) ya Tathmini ya Matokeo ya Mradi (PADEP Impact Assessment) umefanyika Serikali kuziwasilisha ripoti hizo Benki ya Dunia.
- Semina za Utayarishaji wa Taarifa Kamili ya Miradi (*Project Profile*) inayofanyika zimefanyika Unguja na Pemba kwa kuwakutanisha washiriki wapatao 25.
- Kazi ya kukusanya taarifa kwa ajili ya '*Project Profile*' imeshaanza katika Mradi wa PADEP, Unguja na Pemba.
- Mfanyakazi mmoja wa Mradi, kada ya uhasibu amepolekwa Chuo cha Elimu cha Pemba kwa masomo ya ngazi ya Stashahada (*Diploma in Accountancy*).

**Gharama kwa mwaka 2011/2012:** Sh. 175,000, 000 kutoka SMZ

**Malengo ya mwaka 2011/2012:**

- Kuendelea kufuatilia maendeleo ya miradi ya wanajamii kwenye Shehia 174.
- Kuandaa semina na mafunzo kwa wakulima na wadau wengine wa Mradi.
- Kufanya ziara za mafunzo kwa wakulima baina ya Unguja na Pemba.
- Kuwapeleka wakulima kwenye Maonyesho ya Kilimo, Nane Nane.

**KIAMBATISHO NAM. 11: TAARIFA YA MAPATO  
YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2010 - MACHI 2011  
NA MAPATO YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA KWA MWAKA  
WA FEDHA 2011 / 2012**

KIFUNGU		MAELEZO	MAKIS JULAI 10 JUNI 20
<b>03 OFISI KUU PEMBA</b>			
28001	14222 4	MAZAO YA MISITU	16,000,
28002	14222 5	ADA YA UUZAJI WA MAWE MCHANGA NA KOKOTO	13,000,
37012	14225 4	UKAGUZI WA MAZAO	4,900,0
37015	14225 7	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	1,000,0
37044	14500 2	MAPATO MENGINEYO	2,000,0
37062	14210 1	MAUZO YA MICHE	1,000,0
<b>JUMLA PEMBA</b>			<b>37,900,</b>
<b>04 IDARA YA MIPANGO NA SERA</b>			
37044	14500 2	MAPATO MENGINEYO	12,000,
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>12,000,</b>
<b>05 KAMISHENI YA KILIMO, UTAFITI NA ELIMU KA</b>			
34018		ADA YA UINGIZAJI WATALII	2,000,0
37012	14225 4	UKAGUZI WA MAZAO	10,000,
37015	14225 7	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	8,000,0
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>20,000,</b>
<b>07 IDARA YA MAZAO YA BIASHARA, MATUNDA NA MISITU</b>			
28001	14222 4	MAZAO YA MISITU	90,000,
28002	14222 5	ADA UUZAJI WA MAWE MCHANGA NA KOKOTO	80,000,
37062	14210 1	MAUZO YA MICHE	5,000,0

		<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>175,000,</b>
		<b>JUMLA YA UNGUJA</b>	<b>207,000,000</b>
		<b>JUMLA KUU</b>	<b>244,900,000</b>

**KIAMBATISHO NAM. 12:**

**MAKISIO NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2010/2011 PAMOJA NA FEDHA ZILIZOTOLEWA KUENZIA JULAI, 2010 HADI APRILI 2011 NA MAKADIRIO YA MWAKA 2011/2012**

<b>KIFUNGU</b>	<b>MAKADIRIO YA FEDHA MWAKA 2010/2011</b>	<b>FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI, 2010 APRIL, 2011</b>
AFISI KUU PEMBA	1,458,374,710	1,256,5
IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI	678,929,007	591,3
IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	-	-
IDARA YA KILIMO	2,391,709,648	1,897,9
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	-	-
IDARA YA MISITU NA RASILIMALI ZISIZOREJESHEKA	919,177,000	744,7
IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	389,591,345	314,6
IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	-	-
<b>JUMLA KUU</b>	<b>5,837,781,710</b>	<b>4,805,2</b>

**KIAMBATISHO NAM. 13: TAARIFA ZA KAZI ZA MIRADI YA  
MAENDELEO JULAI HADI MACHI, 2011**

<b>K A S M A</b>	<b>JINA LA MRADI</b>	<b>MA KISI O 2010/ 2011 SMZ</b>	<b>FE DH A ZIL IZO TO LE WA 201 0/20 11 SM Z</b>	<b>%</b>	<b>MA KIS IO 201/ 201 1 WA HIS ANI</b>	<b>FED HA ZIL IZO TO LE WA WA HIS ANI</b>	<b>%</b>	<b>MAK ADIR IO YA MWA KA 2011/2 012 SMZ</b>	<b>MA KAD IRIO YA MW AKA 2011/ 2012 WA HIS ANI</b>
61 20 5	PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO- MIFUGO	75,00 0,000	57,0 00,0 00	7 6 0 0	994, 315, 000	620, 815, 437	6 2 0 4	50,957 ,000	733,7 94,00 0
61 22 5	PROGRAMU YA KUIMARISHA HUDUMA ZA KILIMO	120,0 00,00 0	83,0 00,0 00	6 9 1 7	914, 162, 000	862, 509, 025	9 4 3 5	126,08 3,000	484,5 25,00 0
61 30 0	PROGRAMU YA KELIMISHA WADAU WA SEKTA YA KILIMO - HIV/AIDS	40,00 0,000	13,0 00,0 00	3 2 5 0	-	-		-	-
61 31 0	MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	300,0 00,00 0	270, 975, 000	9 0 3 3	208, 240, 000	151, 480, 003	7 2 7 4	721,50 0,000	77,00 0,000
61 32 0	MRADI WA KUKUZA USARIFU WA	190,0 00,00	185, 156,	9 7	1,37 0,00	164, 400,	1 2	211,70 0,000	1,232 ,000,

	MAZAO YA KILIMO	0	300	. 4 5	0,00 0	000	. 0 0		000
61 26 0	MRADI WA USHIRIKISHWA JI WA MAENDELEO YA KILIMO	166,0 00,00 0	141, 087, 000	8 4 . 9 9	-	-		175,00 0,000	-
61 24 0	MRADI WA KUIMARISHA MIKARAFUU	80,00 0,000	39,1 75,0 00	4 8 . 9 7	-	-		300,00 0,000	-
61 25 2	HIFADHI YA MISITU YA ASILI (HIMA)	-	-		2,83 1,83 5,00 0	243, 724, 944	8 . 6 1	-	1,077 ,716, 000
61 25 3	UHIFADHI WA MISITU YA PWANI	-	-		731, 580, 000	116, 137, 878	1 5 . 8 7	-	731,5 80,00 0
61 21 5	MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA KILIMO CHA U/MAJI	200,0 00,00 0.	92,5 78,7 00.0 0	4 6 . 2 9	137, 000, 000	137, 000, 000	1 0 0 . 0 0	1,400, 000,00 0	-
61 21 6	MRADI WA KILIMO CHA KISASA CHA UWENDELEZAJI WA KILIMO							-	
	CHA UMWAGILIAJI MAJI TANZANIA	220,0 00,00 0	177, 028, 000	8 0 . 4	-	-			-

				7					
	PROGRAMU YA KUIMARISHA MIUNDO MBINU YA MASOKO YA KILIMO							162,50 0,000	247,0 16,00 0
	PROGRAMUYA UTAFITI WA KILIMO NA MALIASILI							452,26 0,000	0.00
	<b>JUMLA</b>	<b>1,391 ,000, 000</b>	<b>1,05 9,00 0,00 0</b>	<b>7 6 1 3</b>	<b>7,18 7,13 2,00 0</b>	<b>2,29 6,06 7,28 7</b>	<b>3 1 9 5</b>	<b>3,600, 000,00 0</b>	<b>4,583 ,631, 000</b>

**Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kuwasilisha hotuba ya mwenyekiti wa kamati hiyo. Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sisi sote tuliyoopo hapa kuendelea kutumia neema yake ya uhai na uzima. Aidha, nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, naomba pia nichukue fursa hii kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansour Yussuf Himid kwanza kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri katika Wizara hiyo na hii ikiwa bajeti ya mwanzo kwake kuwasilisha kwenye Baraza. Kamati inaamini kabisa ni kiongozi mahiri mwenye uwezo mkubwa wa utendaji na usimamizi wa majukumu anayokabidhiwa na haya yameanza kudhihirika kwenye hotuba yake kama ambavyo ametuwasilishia hii leo. Pia pongezi zangu ziwafikie watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Kamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo mbali mbali wa wizara hii. Tunawapongeza kwa utekelezaji mzuri wa kazi, mashirikiano wanayotoa, pamoja na maelekezo yao ya kina kwa wajumbe wakati kamati hii ilipofanya kazi zake.

Mhe. Spika, naomba vile vile niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano yao ambayo leo hii yananiwezesha kuwasilisha hotuba hii kwa niaba yao.



Mhe. Spika, naomba uniruhusu niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kama ifuatavyo:

Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
Mhe. Abdalla Mohamed Ali	Makamo Mwenyekiti
Mhe. Mlinda Mabrouk Juma	Mjumbe
Mhe. Rufai Said Rufai	Mjumbe
Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa	Mjumbe
Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
Ndg. Amour Moh'd Amour	Katibu
Ndg. Asha Said Mohamed	Katibu

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imepewa majukumu ya kusimamia Sekta za Kilimo na Maliasili ili kutimiza malengo ya kuongeza uzalishaji wa tija katika kilimo, ili kuhakikisha uhakika wa chakula na lishe katika nchi na kusimamia uhifadhi na matumizi ya rasilimali zisizohamishika.

Mhe. Spika, majukumu hayo ni makubwa, kwani bado tunatambua kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa maisha yetu. Ili nchi ipige hatua kubwa ya maendeleo basi ni lazima kujitosheleza wenyewe kwa chakula ni jambo la muhimu sana. Ni ukweli usiopingika kwamba idadi ya watu inaongezeka katika ardhi tuliyonayo na hali ya kwamba ardhi ile imebaki pale pale na hivyo kuyafanya mahitaji ya watu katika matumizi ya ardhi hiyo kuwa makubwa kuliko ukubwa wa ardhi yenyewe.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba ardhi hiyo tunaihitaji siyo tu kwa matumizi ya kilimo, bali hata kwa makaazi na mambo mengine lakini ardhi ndogo bado ni ndogo tuliyonayo, tukiyapanga vyema matumizi yake, kwa kulima kitaalamu basi tunaweza kupata mavuno makubwa. Mtazamo huu ndio ambao Serikali yetu inao kupitia Wizara hii ya Kilimo na Maliasili na ndio mana Mhe. Waziri leo ametuwasilishia mikakati ya wizara katika kufikia malengo hayo. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa maamuzi hayo. Tunaamini kwamba kauli mbiu iliyopo hivi sasa ya Mapinduzi ya Kilimo itatimizwa kivitendo.

Mhe. Spika, naomba nieleze japo kwa kifupi maoni ya kamati yetu juu ya utekelezaji ulioanishwa kupitia Idara na Taasisi zilizomo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

## **Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 ya idara hii ni utayarishaji na uratibu wa Sheria, Sera, Mikakati na Mipango ya Miradi ya Sekta ya Kilimo, lakini pia kwenye Sekta ya Misitua pamoja na sheria ya hatimiliki ya wavumbuzi na watafiti wa mbeu mpya za mimea.

Mhe. Spika, kamati yetu inasisitiza kwamba sera hizo zinazohusu kilimo na misitu basi zichanganye fikra za makundi yote wakiwemo wakulima wenyewe, wataalamu wa kilimo na watu wa Utawala. Hii itasaidia sana kuona kwamba tunakuwa na sera iliyotimia ambayo itakidhi haswa yale mahitaji tuliyoyakusudia na hivyo inakua rahisi kuyafikia malengo yetu. Halikadhalika tunapochukua takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula au ya biashara au hata hizo maliasili basi tujitahidi sana kufuatilia kwa karibu mno hali halisi na ilivyo, jambo ambalo litatuwezesha kupata takwimu iliyo sahihi.

Mhe. Spika, tunaamini kwa dhati kabisa usimamizi wa miradi ya kilimo na mifugo, kama vile uhifadhi wa misitu ya pwani, na ile ya asili, programu ya umwagiliaji maji, uimarishaji wa mikarafuu, Uwezeshaji wa Maendeleo ya Kilimo, Uhakika wa Chakula na Lishe, Ukuzaji na Usarifu wa mazao ya kilimo, Programu ya kuendeleza Sekta ya kilimo na mifugo (*ASDP-L*), Programu ya kuimarisha Huduma za Kilimo (*ASSP*) Na Programu ya Utafiti wa Kilimo na Maliasili, pamoja na Mradi wa Usafiri wa Mawasiliano ambao unahusisha Programu ya Miundombinu ya soko, kuongeza thamani na misaada vijijini. Hii itasimamiwa vyema na kuleta tija inayotarajia.

Mhe. Spika, jumla ya shilingi 8,139,849,000 zinazohitajika sio kidogo, ambapo kati ya hizo shilingi 3,600,000,000 ni mchango wa serikali moja kwa moja na shilingi 3,113,296,000 ni msaada, wakati shilingi 1,426,553,000 ni mkopo. Tunaiomba Serikali ijitahidi kuweza kutoa mchango wake huo kwa wakati lakini pia wasimamizi na waendelezaji wa miradi hiyo wawe makini katika kutekeleza wajibu wao.

## **Idara ya Uendeshaji na Utumishi**

Mhe. Spika, mambo makubwa ambayo kamati yetu inayasisitiza ni suala la mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa hatimiliki wa rasilimali za Serikali zilizopo chini ya Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Kwasababu tunahitaji uzalishaji mkubwa wa mazao kupitia ardhi ndogo tuliyonayo ni dhahiri kwamba, tunahitaji kilimo cha kitaalamu ambacho kitahitaji nyenzo zake, nazo ni vifaa na wataalamu wa kuvitumia na kutoa elimu kwa wengine. Ni vyema tukawa na mpango madhubuti wa kuwaendeleza wataalamu wetu

pamoja na kwamba elimu ina gharama kubwa lakini hili tusiliogope kwani kila tutakapowafundisha wengi na tukiwatunza na kuwatumia kikamilifu basi tija itapatikana.

## **Idara ya Kilimo**

Mhe. Spika, idara hii imepewa majukumu makubwa hasa yanayohusiana na usimamiaji wa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora na mbolea, huduma za matrekta pamoja na kuratibu karantini na ukaguzi wa mazao.

Mhe. Spika, tunaipongeza sana Serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo na Maliasili kwa kutoa punguzo kubwa la mbolea, lakini pia na huduma za ukulima wa matrekta. Tunaelewa fika kwamba kundi kubwa la wakulima wetu vipato vyao ni vidogo na wanahitaji kuendelezwa. Msukumo mkubwa uwe kwa haya maeneo ya upatikanaji wa mbolea, mbegu na madawa.

Mhe. Spika, kwa mkakati huo wa Serikali tunatarajia sana unafuu ambao utawezesha wakulima wetu kuzalisha kwa wingi. Jengine ni suala la usambazaji wa mbegu kwa wakulima. Kamati inaamini kwamba usambazaji huo utazingatia mahitaji halisi ya mbegu, lakini pia wakati muafaka wa upatikanaji wake. Kwani bila ya hivyo juhudi hizo zinaweza zisikidhi haja iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la nzi wanaoharibu matunda yetu hasa maembe ambapo kwa kiasi fulani wameharibu sifa ya soko hilo hapa kwetu ambapo tayari tulikuwa tunasafirisha boribo za Muyuni nchi za nje. Mafanikio ya kuwaondoa wadudu hawa yatairudisha ile hadhi na haiba ya embe zetu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 jumla ya mitego 21,718 ya kunasia nzi hao iliwekwa na kupunguza athari ya kuharibika kwa matunda kwa asilimia 43. Ni kazi nzuri na tunatarajia kwa mwaka huu wa fedha basi tufikie lengo la angalau asilimia 70.

Mhe. Spika, ukiachilia mbali wadudu hao wa nzi wanaoharibu matunda, bado kuna wengineo kama vile viwavi jeshi wanaoharibu mazao ya mpunga na mahindi, nzi weupe wanaoharibu mazao ya mboga mboga na wengine wanaoharibu migomba na mihogo. Hao wote lazima Serikali iangalie na kuthibiti vyanzo vyao na pia iwe tayari kuwaangamiza wakati wanapojitokeza.

Mhe. Spika, tumekuwa tukihimizana sana ukulima wa mpunga na hii ni kwasababu ya kuwa ndio chakula chetu kikuu. Pamoja na ukweli huo bado tuendeleo kuhimizana sana na aina ya vilimo vyengine kama vile mtama,

mahindi, mbaazi, chooko na kunde. Halikadhalika mazao ya mihogo, viazi na ndizi ili navyo visaidie mahitaji ya chakula na hivyo kuufanya mpunga tunaozalisha uweze kutosheleza. Jambo la kufurahisha ambalo Mhe Waziri amelieleza ni suala la kufufua kilimo cha pilipili hoho kwa wakulima wa maweni. Hilo nalo litajenga matumaini makubwa kwani mazao hayo ya biashara yanaweza kuleta tija kubwa kwa wananchi wetu katika kujikwama kiuchumi.

### **Chuo cha Kilimo – Kizimbani**

Mhe. Spika, uamuzi wa kuwa na chuo kinachotoa taaluma ya kilimo hapa petu haukuwa wa bahati mbaya, ni uamuzi wa busara na wenye kukidhi haja hiyo. Tunahitaji wataalamu wanaojifunza kwenye mazingira tunayofanyia kazi na kwa maana hiyo, wanafunzi wanaosoma fani hii hapa wanapoyatafsiri mafunzo yao kivitendo basi huwa ndio uhalisia wenyewe. Kwa hiyo, kamati inaiomba Serikali ikipe kipaumbele chuo chetu kwa vifaa na nyenzo pamoja na wanafunzi kutunzwa na kuenziwa katika mazingira yaliyo mazuri ili tupate wataalamu walio bora.

### **Taasisi ya Utafiti wa Kilimo**

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba juhudi zote ambazo wizara inazipitisha katika kufikia malengo ya kuwa na mbegu bora na uzalishaji mkubwa wa mazao, hazitafanikiwa endapo hakutakuwa na utafiti wa kutosha katika maeneo yote yakiwemo utafiti wa udongo bora wa kilimo na aina ya mazao, mbegu bora katika eneo stahiki, mbolea bora kwa aina fulani ya mazao na mengi mengineyo.

Mhe. Spika, kwa kuelewa hivyo kwamba bila ya utafiti hatuwezi kufikia ufanisi, basi Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu kubwa. Tunaelewa na kwa kweli kamati inawapongeza sana watafiti wetu kwa kazi kubwa waliokwisha kuifanya na wanayoendelea nayo ya utafiti wa mbegu. Tayari tafiti zinaonesha kwamba tunaweza kuzalisha kwa wingi mpunga wa juu (ambao haulimwi kwenye mabonde) na ni wenye kutoa mazao mengi. Mbegu hizo ambazo ni *NERICA* 1, 10 na 12 zikisambazwa kwenye Wilaya zote za Unguja na Pemba tutakuwa tumepiga hatua kubwa mbele.

Mhe. Spika, kazi ya kuzifanyia utafiti mbegu nyengine za mpunga, mazao ya mizizi na mbogamboga zinaendelea. Tuna matumaini kwamba watafiti wetu watagundua mbegu nyengine nzuri zinazofaa katika mazingira ya nchi yetu.

Mhe. Spika, jambo muhimu la kuangaliwa ni namna ambavyo Serikali itakavyowawezesha wataalamu wetu kwa kuwapatia nyenzo na vifaa vya kufanyia kazi, mafunzo zaidi na malipo stahiki.

Mhe. Spika, endapo matokeo ya utafiti yatatumika vyema na wakulima wakapatiwa mafunzo ya matumizi ya tafiti hizo ni jambo litakaloturusha kutoka tulipo hadi kufikia tafsiri halisi ya mapinduzi ya kilimo. Kamati inashauri elimu kwa wakulima ni muhimu.

### **Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe**

Mhe. Spika, idara hii ni mpya ambayo imeundwa kwa madhumuni ya kuratibu masuala ya uhakika wa chakula na lishe, ndiyo yenye kufanya upembuzi yakinifu juu ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*National Food Reserve*).

Mhe. Spika, nchi kutokua na akiba ya chakula ni hatari sana. Kila siku tunasikia habari za mabadiliko ya tabia nchi, majanga mbali mbali yanatokea duniani. Mwenyezi Mungu azidi kutuepusha nayo lakini kwa sababu dunia imekuwa kijiji basi athari ya nchi moja husababisha na athari nyengine kwa nchi nyengine. Ukiachilia mbali hayo ya mabadiliko ya hali ya hewa, lakini pia mabadiliko ya tabia za watu ambayo nayo yanaziingiza nchi katika mabalaa ya migogoro na vita. Hayo yote husababisha upungufu wa mambo mengi likiwemo hili la uzalishaji wa chakula.

Mhe. Spika, tunalianzisha jambo hili la kuwa na Hifadhi ya Chakula cha Taifa kwa nia njema kabisa na kwa madhumuni ya kwamba chakula hicho kisaidie wakati wa dhiki. Jambo hili linahitaji uratibu nzuri na hivyo kamati inaomba zile kamati zilizoandaliwa kwa madhumuni haya na kwa mujibu wa sheria basi zive na mashirikiano ya hali ya juu katika kulifanikisha suala hili.

### **Idara ya Misitu na Maliasili zisizohamishika**

Mhe. Spika, katika kuinusuru nchi yetu na athari ya majangwa na mmong'onyoko wa ardhi, Idara ya Misitu na Maliasili zisizohamishika ina jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti mzuri na utaratibu muafaka wa ukataji na upandaji wa miti lakini pia uteuzi mzuri wa maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Spika, kwa kufikia malengo hayo, basi suala la uzalishaji wa miche ya misitu na matunda ni muhimu sana, sambamba na usimamizi wa sheria zinazolinda uhifadhi wa misitu hiyo. Kamati imebaini kwamba, adhabu zilizomo katika sheria za misitu ni ndogo kiasi cha kwamba haimuogopeshi

hata kidogo mtu kutenda makosa hayo ya ukataji wa miti bila ya Kigali. Hivyo basi, inaiomba wizara kuzipitia upya sheria zake hizo ili zifanyiwe marekebisho yanayofaa kwa wakati tulionao.

Aidha, suala la uchimbaji wa mchanga nalo liangaliwe kwani inaelekea kwamba Sheria yake nayo haitishi sana au haisimamiwi kikamilifu. Magari ya ng'ombe na punda yanachota mchanga hadi pembezoni mwa nyumba jambo ambalo linaweza kusababisha athari katika nyumba hizo. Jambo hili ni hatari sana na tusipokuwa makini iko siku athari yake itatuumbua. Lakini hata hayo magari ya mchanga nayo wakati mwengine baadhi yake huchukua mchanga katika maeneo yasiyuruhusiwa.

Mhe. Spika, katika kulinda misitu yetu na rasilimali zizozrejesheka pamoja na kupanda miti kwa wingi bali pia ni vyema na ile misitu yetu ya asili tuliyonayo na ambayo inahitaji kuhifadhiwa tuendelee kuitunza kwa faida yetu na vizazi vyetu vijavyo. Idara ijitahidi kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuzilinda rasilimali zetu hizi.

### **Idara ya Umwagiliaji Maji**

Mhe. Spika, bado tunaamini kabisa kwamba mkombozi wa kilimo cha mpunga basi ni kilimo cha umwagiliaji maji. Pamoja na kugundulika kwa mbegu ambayo haihitaji maji mengi lakini kwa vile tuna maeneo mengi ya mabonde basi ni vyema tukaweka mikakati madhubuti ya kukiendeleza kilimo cha aina hii.

Mhe. Spika, serikali imekuwa na mpango wa muda mrefu wa kuendeleza kilimo hiki ambapo kwa kupitia wafadhili mbali mbali wakiwemo *JICA*, *USAID* na *KOICA* jumla ya hekta 6000 za umwagiliaji maji tayari zimepata wafadhili. Ingawaje kwa sasa jumla ya hekta 700 zishafanyiwa umwagiliaji na lengo ni kufikisha hekta 8521 kwa maeneo yote ili kuhakikisha kuwa kilimo chetu kinakua endelevu.

Mhe. Spika, bila ya shaka kwa mikakati iliyopangwa ifikapo mwaka 2016 tutaweza kufikisha hekta 5,805 zilizokwisha kufanyiwa miundombinu ya maji na hivyo eneo linalofaa kulimwa kwa kilimo hicho kufikia asilimia 68. Kwa kweli tutakuwa tumefikia mbali sana.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Wizara ya Kilimo na Maliasili, Kamati yetu inashauri kuwepo kwa mikakati madhubuti itakayohakikisha ugawaji wa fedha kwa wakati katika idara zote hususan kwa upande wa Pemba ili malengo yaliyopangwa na idara hizo yawe yanafikiwa kwa wakati. Na kwa mnasaba huo, tutakuwa na mustakabali mzuri wa kuendeleza Sekta ya Kilimo na Maliasili kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa upande mwingine kuongezeka kwa wizi wa mazao mashambani, uvamizi wa maeneo ya kilimo na misitu pamoja na matumizi mabaya ya misumeno ya moto ni tatizo kwa nchi yetu kwani athari zake ni kubwa kwa jamii ya sasa na hata kwa vizazi vijavyo. Hivyo basi, kamati inashauri kuwepo kwa sheria madhubuti ambazo zitahakikisha kuwa matatizo haya yanadhibitiwa kwa nguvu zote na hivyo wakulima watakuwa na uhakika wa kuvuna mazao yao kwa muda waliojipangia na kuepuka kuvuna mazao hayo na watu wasiohusika na kuendelezwa kwa hofu ya wizi. Kamati inashauri Masheha wa vijiji washajiishe ulinzi wa Polisi Jamii ili kuondoa tatizo hilo.

### **Kuhusu Mapinduzi ya Kilimo**

Wizara ya Kilimo iendeele kuwahamasisha na kuwahimiza wananchi kilimo cha kisasa, kilimo cha kisasa ndio ufunguo wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu na ndicho kitakachoongeza tija na ziada kubwa. Kilimo cha kisasa ndicho kitakachoondosha uchumi wa kujikimu hatua kwa hatua na badala yake kujenga uchumi wa soko huria.

Mhe. Spika, ongezeko la tija la ziada ya mazao litapunguza umaskini na litaongeze mazao ya kuuza nje ili kujipatia fedha za kigeni na litachochea uanzishwaji wa Viwanda vya Kusindika Mazao hapa nchini.

Mhe. Spika, ili kufikia azma hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Ali Mohamed Shein ni lazima iwawezeshe wakulima kutekeleza kanuni za kilimo bora kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao kwa kila eka kulingana na viwango vya kisasa kwa kila zao wanalolima.

Mhe. Spika, ili kufikia malengo haya, serikali tunaishauri itenge bajeti stahiki na sio kama ilivyo sasa.

Kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo wizara imekadiria kutumia jumla ya shilingi 15,306,631,000. Kati ya hizo shilingi 6,623,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, shilingi 500,000,000 ni kwa ajili ya ruzuku ya Chuo cha Kilimo Kizimbani na shilingi 8,183,631,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, kwa kipindi hicho cha 2011/2012 wizara imekadiria kukusanya mapato jumla ya shilingi 240,000,000/-.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo haya kwa niaba yangu na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na kwa niaba ya

Wajumbe wote wa kamati hii, kwa niaba ya Waziri wa Kilito na Maliasili pamoja na watendaji wake wote na kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Kikwajuni tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Baada ya kwishakuwasilisha Hotuba ya Mwenyekiti naomba ridhaa yako ili na mimi nichangie kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya kwishakuwasilisha hotuba hii mimi naomba kama Mhe. Waziri alivyokuja hapa na kusema kwamba ametoa changamoto kwa ajili ya kilito hiki ili tuweze kuondokana na umasikini katika nchi yetu, ningelichukua fursa hii basi Mhe. Spika, kumuomba Mhe. Waziri na sisi wana Kikwajuni tumehamasika katika suala zima la kilito cha mpunga na mihogo katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama tulivyokwishakuanza juhudi zetu za mwanzo naomba lile ombi la wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kupatiwa eneo la kulima zao la muhogo na mpunga tutfanyie utaratibu kupata eneo hilo kwa haraka ili nasi tuweze kuungana na wenzetu Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla katika harakati za kuendeleza kilito ili tuweze kuondokana na tatizo la umasikini.

Lakini pia mchango wangu mwingine nirejee tu, tulipokuwa katika kamati tuliomba wizara yako Mhe. Waziri mukae na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili tuweze kutengeneza utaratibu mzuri wa kuweza kuhakikisha kwamba tunatengeneza utaratibu wa kulinda vyanzo vyetu vya maji ambavyo kwa sasa vinaendelea kupotea kwa asilimia kubwa kabisa. Mtakapokaa pamoja na kushirikiana mtaweza kutusaidia sana kuendeleza misita katika nchi yetu hii na kuhakikisha kwamba wananchi wetu vyanzo vyao vya maji vinaenziwa na kutunzwa hususan ikiwa wewe utakuwa dhamana hasa kwa sabau wewe ndio mwenye kushughulika na Idara ya Misita.

Jengine Mhe. Spika, ningeliomba kuchukua fursa hii kuomba tena Wizaa ya Kilito kupitia tena sheria zinazohusu Idara ya Misita ili ziweze kwenda na wakati na ule ukataji wa miti uweze kumalizika au kuondoka kabisa.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kikwajuni kwa mara nyengine tena naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii asubuhi ya leo ili kuweza kufungua dimba kuichangia Wizara hii ya Kilito na Maliasili.



Mhe. Spika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sote kwa kutupa pumzi na kutufikisha kwenye Baraza lako tukufu asubuhi hii ya leo kuelekea mchana na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuendeleza na pumzi zetu kuendelea kudunda.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na makamo wake wa kwanza na wa Pili nao lazima tuwashukuru viongozi wetu. Lakini niseme tu Mhe. Rais safu yake imekuwa ni nzuri sana kwa kutuletea viongozi wake waadilifu na hususan katika bajeti hii in asura mpya kabisa ya Wajumbe wako wa Baraza hili na hasa kuleta msisimko mkubwa. Wenzetu sasa hivi huko Uingereza, Marekani wanatuingalia katika Baraza lako hili tukufu na hususan kwa kitendo alichokifanya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kutuweka *open* kabisa na mtandao upo watu wanatuona. Kwa hili Mhe. Spika, nitoe pongezi Kubra sana kwa sifa hiyo.

Mhe. Spika, kama kawaida yangu nikianza kuchangia huwa nina masikitiko makubwa na hasa katika zile wizara ambazo zinawagusa wananchi. Jana nilipochangia sehemu ya uvuvi nilikaribia kutaka kutoka machozi, kwa sababu nimeona bajeti yake ni ndogo sana, sasa halikadhalika na wizara hii na hasa vile tunavyosema kuwa ni uti wa mgongo katika kilimo na bado bajeti naona ni ndogo, hata ukiwapelekea watu wa Jimbo la Kitope kwa kweli haikidhi haja.

Mhe. Spika, mimi nafikiria kwamba sasa tuwe wakweli, Mhe. Waziri nakusifu sana pamoja na watendaji wako hususan katibu na naibu katibu pamoja na wakurugenzi wote na wataalamu. Hiki kitabu chako umekieleza vizuri sana, mimi nafikiria wajumbe sijui kama atatokea wa kuweza kupiga buti. Kwa sababu ndani yake umeeleza kwa maandishi vizuri lakini tuangalie na utekelezaji wake ukoje Mheshimiwa.

Nikianza katika masuala ya umwagiliaji wa mpunga hii ni moja katika ukurasa wa 37 hapa. Katika vitabu vya nyuma vilivyopita hivyo mara nyingi sana ilikuwa tunaoneshwa mabonde yale kwa yale tu ya Bumbwisudi, Mwembemchomeke, lakini nashukuru sana kitabu hiki leo kimetuonesha kwamba sasa tuna nia ya uendeleu wa kutafuta mabonde mapya na zaidi nimefarijika kuona bonde la Kilombero. Hii ni faraja kuwaba sana na kweli naamini kwamba sasa hivi Dkt Shein anataka kuondoa umasikini kwa kupitita wiziri wake kwa njia ya umwagiliaji.

Mhe, Spika, nimkombozi asikwambie mtu mwingine, kama hatuna njia hizi basi kila situ tutakuwa masikini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba sana tena sana acha mambo yote punguza safari zako za nje uwe katika uchangiaji hili suala liwe ni la mwanzo tuone jinsi gani katika mabonde haya uliyoyaainisha ili yaweze kulimwa, tena hapa ukija mara hii sitaki nikupige buti lakini uniambie

tarehe, unambie kwamba fedha zikiingia baada ya mwezi mmoja au miwili, mitatu naanza kuchimba misingi katika Bonde la Kilombero. Kwa sababu bonde lile ni kubwa sana, lina historia kubwa lakini tumelitupa, kuna *open space* nyingi sana utazikuta kama uliwahi kutembea hazilimwi na hazilimwi kutokana na hali halisi kuwa wanaona ni yale kwa yale tu kila siku wakilima wanakuwa hawapati situ chochote.

Mhe. Spika, tunaewa kwamba hivi sasa mvua hatuipati na tunaikimbiza kwa makusudi kwa mambo tunayoyafanya. Mvua inavutika kutokana na mimea, lakini leo mime ile tunaiondoa kwa makusudi sasa mvua itakuja papi? Halafu tuseme leo tutegemee ulimaji wa mvua hiyo haiwezekani hiki kitu tukubaliane. Lakini mimi nikazanie serikali kuu, kutokana na malengo yako uliyoyataja humu serikali kuu je, itakupa fungu hili? Hapo ndio suala lilipo.

Hivi sasa wananchi wanakusikiliza vizuri huko nina imani wanakupigia kofi kutokana na mambo kila mkulima anshukuru kuwa sasa umasikini unaondoka kwa hii mipango yako. Lakini je, serikali kuu tuna tabia sisi ya kuwapa asilimia ndogo katika wizara zetu kwa mipango mizuri hatimaye tunakuja kuwalaumu hapa tunawapigia mabuti kumbe tunapiga buti kwa kuwaonea tu. Serikali Kuu ndio inayowafanya hivyo, kuwapa kasma ndogo, yale malengo yanakuwa hayafikiwi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kasema hapa ataleta matrekta, *power taller*, tena unaleta trekta kwa *grade*, ametaja kwa kila *power* yake ile. Mhe. Spika, hiyo ni sifa nzuri mimi sijapata waziri mwingine yoyote kufanya situ kama hicho ukweli tuseme tu, Mheshimiwa kuficha kwangu mimi mwiko. Lakini haya yote aliyoyakusanya akipeleka jimbo la Kitope kule kwa wakulima dakika tu yanapanguswa hakuna hata moja litakalobaki. Lakini kama tuna nia nzuri kutaka kuwaondolea umasikini wananchi wetu tuwe na mpango wa kuwakopesha vitu, hii ndio itakuwa njia moja ya ukombozi, kachukue trekta, *power taller* hizo wananchi wakopeshe, serikali ising'ang'anie tu. Hiyo ni *plan* yako nzuri Mhe. Waziri na utakuwa na uhakika wa umasikini kuondoka kawakopeshe wakulima matrekta kwa bei nafuu.

Mhe. Waziri kaeleza hapa vitu ambavyo ni muhimu, alisema mbolea na kweli mbolea ilikuwa ni ghali, watu walikuwa wanashinda kutumi ambolea. Alisema suala la ulimaji kwa trekta pia, ni kweli Mhe. Waziri kuchimbua na kuburuga ilikuwa ni ghali kabisa mkulima wa chini hawezi hana kipato hicho na hasa ukiangalia kipato chake cha ukulima kinakuwa ni kidogo. Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwamba ameweza kupunguza vitu hivi madawa ya magugu, mbolea, matrekta katika uchimbaji na kuburuga basi sidhani kama utashindwa na kuwakopesha wananchi matrekta kwa bei nafuu, hilo naamini wazi utaweza.

Mhe. Spika, waziri akifanya hivyo Zanzibar pamoja na ardhi yetu kuwa finyu kwa sababu ni ndogo sana lakini kuna ulimaji wa kisasa. Hawa utafiti niseme *Alhamdulillah* kwa kupitia mwenyewe mtaalamu Mkuregenzi Mberik, wanajitahidi sana katika kutoa taalama za ulimaji wa kisasa, wanasaidia sana na kijana wake Othman. Utakuja na kisomo kidogo lakini unapata mpunga mwingi sana, lakini kutokana na zile zana ulizozisema kuzipunguza bei basi naamini mwaka kesho wa mpunga tutakula mpunga mwingi sana.

Kusema kweli kuna bonde jengine la Pangezi. Mhe. Spika, tusifichane hivi sasa hakuna kiwanda cha sukari wala cha nini wapewe wananchi walime mpunga, tunawasumbua tu kwa nini tuwasumbue wananchi wetu. Kulikuwa na tume imeundwa ya kuja kutupa ripoti ya kiwanda kile je, kitaendelea au hakitoendelea? Kwa sababu ni moja katika kuzuia mabonde ya walimaji mpunga, kimekasimu sehemu kubwa na kuwapotezea wakulima wetu.

Mhe. Spika, hii tume sijui inangoja nini, kwa sababu naona wizara zinakwenda zinazunguruka sijasikia tume ikaeleza, lakini naingojea tume hiyo katika kiwanda. Mimi kama sikupata jibu zuri kwenye tume kuhusiana na kiwanda kile nazuia fungu la Wizara ya Biashara na Viwanda, nitazuia kabisa tena mshahara wake hasa naunyakua wapu ili niweze kupata taarifa iliyokuwa nzuri. Kwa sababu ni maeneo makubwa na ni mazuri tu, lakini mpaka leo tunaona kimya, nina *message* ndani ya simu zaidi ya tatu naulizwa Mheshimiwa vipi suala la viwanda, ninawaambia bado mwenyewe msimfanyie haraka atakuja kutujibu, waziri mzuri tu yule atatuletea manufaa yake.

Kwa hivyo, kwanza nikupe pole hiyo kuwa ardhi huna, ardhi sasa hivi inavamiwa watu wanataka kujenga, lakini tulikubaliana hapa kwenye kamati yangu na waziri kuwa kutakuwa na ardhi ya ukulima Mbale, ya kufanyia masuala ya michezo mbali na masuala ya ujengaji yatakuwa mbali. Hiyo ni moja iliyonipa faraja kubwa na hasa hii *plan* yako uliyoiweka.

Lakini niingie pia katika ukurasa wa Misita, kwa kweli Idara ya Misita hii nikwambie mwenyekiti wangu alisema hapa labda hii sheria inalegalega. Mimi pia niunge mkono, kama hatuko *serious* tukakunja uso kwa kutokumuonea mtu haya Mhe. Waziri utakuwa huna msitu, tusidanganyane kabisa. Hivi sasa msitu wa Kiwengwa na Ramadhani hiyo hapo unaanza kulia machozi, unajua sasa hatari hiyo inakuja sasa kuja kukatwa.

Mhe. Spika, msitu kwa Zanzibar iliyobakia ni miwili tu, Jozani na Kiwengwa, wenzetu Jozani tayari wame-*control* vizuri na sasa hivi si rahisi kwenda kukata. Lakini Kiwengwa bado tungali tunaoneana haya hili suala linasikitisha sana. Sheria tunaichezea mkononi hatuifanyii kazi, msitu wa Kiwengwa utaonea huruma unalia machozi na *season* hiyo hapo sasa hivi. Mimi kweli na niwe

mbaya sikufichi, Mhe. Waziri kwa hili nasema tena kwa Sauri pana kabisa na niwe mbaya katika mali yangu sitokubali kuchezeza, utanicheyaje sharubu alaa, mchezo ule utakuwa kila siku kata kata mimi nitakuwa na rasilimali gani ya kuweza kujisemea.

Mhe. Spika, ukiangalia kuna mapango mengi tu ya maji kule, lakini leo ukikata msitu ukiweka wazi maji yatakauka na yanawasaidia wananchi sasa hivi tena sana tu. Sasa Mhe. Waziri mimi nakuomba kabisa kama kuna kipengele ambacho kinalega lega katika sheria ya msitu tulettee hapa tukupitishie haraka sana, lakini msitu wa Kiwengwa upate kuepukana na kukatwa.

Mhe. Spika, mimi leo nilikuwa na sehemu chache tu, ambazo sehemu hizo mbili mimi ndio zinaniuma ndani ya roho na zinanikondesha kabisa. Kwasababu mimi tayari nafsi yangu inatokana na mifupa ya ukulima na msitu ambao umo ndani ya eneo langu naona jinsi uharibifu unavyoendelea siku hadi siku.

Kuna *community* kule Kiwengwa naomba Mhe. Waziri uiite kwa makusudi na iuisaidie, wanafanya kazi vizuri wanalala ndani ya msitu wakiongozwa na kiongozi wao, hawa lazima uwaiite na uwajenge kabisa.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa zungumza na kiti zaidi na uzingatie muda.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, samahani na kweli *shake shake* ya ku-*running* hivi ndio wakati mwengine nakosea kukuona. Nashukuru Mhe. Spika. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri badala ya kuwapa baskeli aendeleze nakuwapa tuzo nyengine za kuweza kuwalinda ili ikitokea maafa mengine waweze kunusurika. Pale walipo hawana *rain boot* za kuweza kuingia kwenye mawe, na nguo zinazokuwa madhubuti kama wenzetu kule Bara wanakuwa na nguo zile za kaki madhubuti, ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuwapatia.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilito na Maliasili hasa katika utamu wa kitabu chake alichokipamba hivi sasa tunaomba heri na ayatekeleze haya aliyoyataja humu. Kwa niaba ya Jimbo la Kitope ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** *Bismillahi Rahmani Rahym.* Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima hadi asubuhi hii tunaendelea na shughuli tulizoagizwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kumteuwa kijana mahiri na kumtwisha wizara ngumu lakini yenye

matumaini makubwa kwa Wazanzibari ndugu yangu Mhe. Mansour Yussuf Himid. Nina hakika Mhe. Rais alifanya hivyo kwa vielelezo, vielelezo vya Mhe. Waziri vilimshawishi Mhe. Rais akamuondoa huko alikoanzia akasema na hapa basi nataka kuona, naomba sana watendaji wa wizara hii wampe kila msaada kusudi yale matumaini ya Wazanzibari juu ya kijana huyu yawe endelevu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niipongeze kwa dhati kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kukiona kilio cha wakulima wetu juu ya pembejeo na wakaweza kuchukua hadi asilimia 70 mpaka asilimia 80 na zaidi imebeba serikali. Mhe. Spika, hili ni jambo kubwa na hatuna budi kuipongeza serikali yetu na kila zuri tufanye hivyo.

Mhe. Spika, pamoja na kushangilia hasa kwenye matumizi ya mbolea ya viwanda bado tuna changamoto kuendelea kutegemea mbolea hizi. Tukitilia maanani ufinyu wa ardhi yetu ya kilimo lakini na kuzingatia ongezeko la idadi ya watu. Mahitaji ya ardhi yanaongezeka siku hadi siku lakini na Mwenyezi Mungu katujaalia tunazaana siku hadi siku. Ardhi inapungua mahitaji yanakua. Wanaotutengenezea mbolea kutuletea kwa kuzalisha mazao ya kilimo wao wenyewe hawaitumii mbolea hiyo kwa mazao kwa matumizi ya binadamu. Ni changamoto kubwa kwetu, ni vizuri tufikie pahala kutokutegemea sana mbolea hizi za viwanda na tuweze kutumia mbolea zetu ambazo zinapatikana humu humu mwetu.

Mhe. Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kwamba pamoja na changamoto aliyonayo ya wataalam kuhama lakini bado nakuhakikishia una safu nzuri na itahitajika serikali kuithamini safu ile kwa kuipa jicho la karibu sana kimaslahi yao.

Mhe. Spika, nije kwenye mwelekeo wa mwaka 2011/2012 kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mhe. Spika, wizara imejikita kutilia mkazo hifadhi ya mazingira. Mhe. Spika, mazingira yetu yanazidi kuchafuka ama kuchafuliwa. Nilisema na leo naendelea kusema Mhe. Spika, kwamba hivi ni vita, kama ni vita sote tukubali kuwa ni maaskari tena askari wa mwamvuli namba moja ili tuweze kushinda vita hivi.

Mhe. Spika, miti bado inateketea, maeneo yote ya kila pembe yanachafuliwa kwa kasi kubwa. Kama tutaendelea kulidharau suala hili kama tunavyolidharau ama kutokuisimamia mikakati tunayoweka Mhe. Spika, tutabeba dhima sana kwa kizazi cha kesho na kesho kutwa.

Mhe. Spika, uharibifu wa mimea unaotokana na maradhi na wadudu bado ni tatizo kubwa na linaendelea kukua siku hadi siku. Mimea yetu inakumbwa na maradhi tofauti na uwezo wa watu wetu kupambana na maradhi hayo ya mimea ni mdogo mno.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu wana kazi kubwa kama tunavyojieleza siku zote kwamba sisi ni madaktari, ni wataalam wa kilimo, ni mainjinia barabarani na kadhalika kwa sababu wakulima hawana uwezo wa kukabiliana na dawa hizi za kuuu wadudu.

Mhe. Spika, jengine ambalo limekusudiwa kuna huyu nzi wa matunda. Nimeona kwenye jadweli usambazaji wa mitego lakini hapa nitamuomba ndugu yangu hebu aturidhishe. Katika hatua hii ya nzi huyu kudhibitiwa tumefikia wapi. Hivi tunakwenda kwa mafanikio au bado juhudi za wizara ni dhaidu kwa maana maendeleo bado ni madogo kuliko matumaini.

Kwa sababu Mhe. Spika, suala la mitego kusambazwa wapi na wapi bado tunatoka nalo Kikwajuni kwenye jengo letu la asili. Lakini hadi leo tuko hapa sijui kama tumefanikiwa kiasi gani kwa kutumia mitego hii, huku tukiona kwamba nzi sasa sio tu kwamba yupo kwenye embe, bali yupo kwenye fenesi, yupo stafeli na kadhalika. Matunda yetu yamekosa sifa na kwamba sasa kule tulikotegemea sana kuwa na soko nchi za Ghuba hatuwezi kupeleka haya matunda. Sasa juhudi zetu tunazojipanga kwa uzalishaji wa matunda hatutofanikiwa kamwe kama hatujaweza kumdhibiti huyu mdudu.

Mhe. Spika, kuna suala la karafuu bahati njema Wazanzibari wamefurahi baada ya kusikia bei mpya ya zao la karafuu. Tujipange basi kwa kuuhami mkarafuu huo uliobaki na kuendelea kupanda mipya. Katika kufanya hivi ndugu yangu Mhe. Waziri bila ya kuusahau mnazi. Mhe. Spika, leo Zanzibar tunaagiza mbata na mafuta ya nazi kutoka Msumbiji. Kwa Wazanzibari ama wenzetu walioondoka Zanzibar miaka 30 iliyopita wakisikia hili watatushangaa. Mnazi unahama kwa kasi kubwa ndani ya visiwa hivi na msumeno unacharaza asubuhi na usiku.

Mhe. Spika, tunasema kwamba msumeno wa moto ni adui lazima tutangaze vita na serikali itamke juu ya udhibiti wa msumeno huu. Mhe. Spika, miti inamalizika. Ni kweli tunatumia rasilimali za ndani lakini lazima tuwe na mipaka katika matumizi tusihamishe kama tunavyofanya.

Mhe. Spika, nazi tunaitumia kwenye chakula lakini na mnazi tunahitaji kwa kupata hiyo nazi yenyewe na mafuta yake na mambo mengine.

Mhe. Spika, umri wetu wa udogo tunakumbuka ni vipi mbata ilivyokuwa ikitumika hapa, leo tunaagiza mbata kutoka Msumbiji hii ni hatari. Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine na jitihada hizi lazima ikae pia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuhakikisha kwamba suala la mnazi kwa kupata mazao yake na mkarafuu sasa zinakwenda sambamba na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, matumizi ya nishati ni kuni na mkaa, mwananchi leo wa kijijini ukija ukimwambia usikate kuni, usipige mkaa, tegemeo lake akate kuni ama kutumia yeye mwenyewe au kuuza kupata riziki yake na mkaa ni hivyo hivyo mbadala ni nini. Hatutoweza tu kukitumia kifungu hichi kama hatujatafuta mbadala wa hili ni nini.

Sasa kuni ni lazima zitumike, mkaa ni lazima utumike, lakini tufanyeje kufidia haya, nadhani hili ndio la kujiuliza. Tufanye nini sasa kufidia kinachokatwa kwa mkaa na matumizi mengine. Mhe. Spika, mpango mzuri uliobuniwa nimekuta huku kwa misitu mpaka ya vijiji nadhani kama itasimamiwa vizuri hili litatusaidia sana. Litatusaidia sio tu kwenye suala la mazingira lakini pia kwa upatikanaji wa mvua.

Mhe. Spika, hii wizara ni nyeti kwa namna yake, hapa ndio kuna uhai wetu, tusaide tunapoweza kusaidia, tuchangie tunapoweza kuchangia kumsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kuna taarifa njema ya kwamba sasa Zanzibar tunakwenda na ile *National Food Reserve*. Kwa kweli taifa kukaa hivi hivi hakuna akiba ya chakula kama tulivyokuwa ni tishio, tukizingatia kwamba leo duniani vyakula vya nafaka tunavyovitumia hapa hususan mchele na mambo mengine dunia inatumia nafaka hizi kwa kulisha wanyama wao.

Mhe. Spika, zamani Wachina walikuwa hawatumii nyama ile ya ng'ombe kwa kiasi kikubwa, sasa wanakula sana na kusudi wapate kwa haraka hizi wanawalisha wanyama hawa kupata ukuaji wa haraka. Sasa na sisi tunategemea kutoka kwao tuna upungufu katika hili. Lakini hivi sasa nafaka hizi hizi zinatumia kusarifiwa mafuta kuendeshea mitambo ya viwanda. Tuna haja ya kujivuta kufunika pengo hili.

Mhe. Spika, ndugu yangu Mhe. Waziri kwa watu alionao tukiweza kupambana na haya yanayotukwaza hatutofunika mahitaji tutapunguza uagizaji. Mhe. Spika, lengo ni kupunguza hasa uagizaji wa mchele nje ya nchi. Lakini *irrigation* tuliyonayo ni ngumu. Mhe. Spika, ni ngumu *cost wise*, ni ngumu kwa uendelevu wake, tunategemea maji yatokanayo chini ya ardhi ni tofauti na

wenzetu wanaotegemea maziwa na mito. Hii kwetu ni changamoto nzito, wakiondoka wahisani inatuwia vigumu kuviendeleza.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe lazima tuhakikishe kwamba vyanzo vya maji vinalindwa na kuendelezwa. Mhe. Spika, hapa ndipo patakapokuwa na kimbilio letu, vyanzo vyetu lazima tuvilinde na tuviendeleze. Mtindo unaoendelea sasa huu wa kuviharibu hatutafaidika chochote kile. Vyanzo vya maji vina umuhimu wake kwa maisha yetu sote, lakini maisha ya huku tunakoelekea kupata maji, maji tutayapataje kama vyanzo vya maji vyenyewe tunaviua.

Mhe. Spika, nimshauri Mhe. Waziri kwamba miti ile inayosaidia kuhifadhi vyanzo vya maji kama miale, mianzi na kadhalika kwa makusudi hebu tufanye kwamba katika ile *plan* ya misitu ya vijiji hii iwemo kwenye program zenu.

Mhe. Spika, bahati njema pia kuna mti unaitwa mkadi na najua kwa umri wako sasa una hadithi ya mkadi na msanata. Lakini nimwambie Mhe. Waziri kwamba mkadi katika ile jumla ya miti ambayo itasaidia kuinua uchumi wetu mafuta ya mkadi leo duniani lita moja ni dola 8,000 za Kimarekani. Sasa tukichanganya na nazi, tukijitahidi na mkarafuu na *Inshaallah* hilo jengine mnalolijua nyote nadhani tutakuwa kwenye hatua nzuri. Lakini tunazungumza kilimo leo namwambia Mhe. Waziri kwamba na mkadi nao kwa sifa zake mafuta yake ni mali nzuri sana, hii iko sana kwenye vijiji vyetu inapatikana kando kando ya pwani ya Bahari ya Hindi.

Mhe. Spika, najua kwamba wengi wana nia ya kuichangia wizara hii na sitopenda kuwakatia wenzangu ili wapate fursa ya kuja kusema chochote kile. Lakini namsihi sana Mhe. Waziri aje atusaidie pia katika niliyoyasema kwenye suala la mitego na mdudu huyu tuko wapi. Lakini nataka pia kauli ya msumeno wa moto tumefika wapi na uendelezaji mzima wa miti hii niliyoitaja kwa maslahi ya vyanzo vyetu vya maji.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi niseme naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, nakushukuru asubuhi hii kunipatia nafasi na mimi kutoa mchango wangu mfupi katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Lakini kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha asubuhi hii kuja hapa kufanya kazi hii kwa lengo la kufanikisha kazi zetu.

Mhe. Spika, kadhalika nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha kwake bajeti hii kwa umakini na umahiri mkubwa. Pia nimpongeze kwa pongezi kadhaa



alizotoa kwa kuanzishwa hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama alivyoona yeye kuwa imetuletea umoja, upendo, mshikamano na maelewano katika jamii. Huu ni ukweli usiofichika wala usiokatalika. Kama si umoja uliofanywa baina ya viongozi wa vyama viwili basi uchaguzi wa 2010 usingekuwa kama ulivyokuwa kwa sababu huko nyuma ulipokuja uchaguzi wengine ilikuwa majumbani tunaaga tukirudi sawa hatukurudi watoto wenu hao. Kwa hivyo, nishukuru kwamba hilo kaliona na kalitolea pongezi.

Mhe. Spika, nije kwenye upungufu wa chakula duniani hasa mchele. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kaeleza kwamba kutokana na matatizo mbali mbali ya kidunia bidhaa hii ya chakula cha mchele ambacho kwa sisi Wazanzibari tumekifanya ndio chakula chetu kikuu kimepungua kwa sababu mbali mbali zilizotajwa na hata siku hizi wanaingizwa maharamia wa Kisomali.

Lakini Mhe. Spika, huu uharamia ni jambo lililozuka leo na jana. Mhe. Spika, serikali pia inalitia suala hili kuwa ni miongoni mwa mambo ambayo yamesababisha bidhaa hii kupanda bei duniani.

Mhe. Spika, takwimu alizotoa Mhe. Waziri hapa inaonesha bado kilimo chetu kiko nyuma sana na tuko mbali kufikia malengo na kujitosheleza kwa chakula. Lazima juhudi za makusudi tuziongeze ili kuweza kufikia lengo la kujitosheleza kwa chakula la mchele, tukiona kuwa mchele ndio chakula hasa kinachopendwa zaidi kuliko vyengine vyote hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, niseme kuwa labda hatua alizozitegemea kuchukua Mhe. Waziri kama zikichukuliwa tunaweza tukasogeza kidogo mbele. Kuna punguzo la bei ya pembejeo za kilimo, mbolea, mbegu na kadhalika. Sasa kwa kuwa punguzo hili ni kubwa na kwa kuwa katika hotuba yake kasema wakubwa duniani hawafurahi hili, sina hakika je, serikali ina uwezo wa kukabili punguzo hili na kuleta pembejeo hizi kama ilivyokusudia. Hofu yangu isijekuwa ni pambo tu la kwenye kitabu lakini kwenye utekelezaji wake ikawa mipango iko mbioni, kumbe siku zote mipango ina mbio zaidi kuliko serikali ambayo inaifukuza hiyo mipango.

Kwa hivyo, hofu yangu ni hiyo, tusije kwenda wakulima kutaka mbolea Wizara ya Kilimo na Maliasili ikatwambia mipango iko mbioni mbolea inaletwa. Ikiwa ni hivyo, ni kweli mipango ina mbio zaidi kuliko sisi wafukuzaji. Kwa sababu kama ingekuwa sisi tuna mbio kuliko mipango ingelikuwa hapa tulipo tumeshaondoka zamani. Namuomba Mhe. Waziri kuhusu suala hili mipango aivute shati, serikali iwe na mbio zaidi kuliko mipango.

Mhe. Spika, nije kwenye zao la karafuu na mkarafuu yenyewe. Mhe. Spika, msitu mkuu wa Pemba ulikuwa ni mkarafuu, siku hizi mkarafuu unatoweka

pole pole kwa njia tofauti. Inakufa kwa sababu nayo ni viumbe, tunaiua kwa kukata kuni na miti ya kujengea na kuna kipindi watu walifika pahala mikarafuu wakawa wanaiua makusudi ili wapate eneo wapande mihogo pale karafuu ilipokuwa ina bei duni. Mashamba kadhaa watu waliopewa eka na Mzee Abeid Amani Karume wameona karafuu haina maana tena na kwa sababu muhogo ndio una soko zuri wakaamua kuuu mkarafuu na hatimae kupanda muhogo.

Mhe. Spika, Pemba hivi sasa zaidi sisi tulioko Kusini na upande wa Mashariki kuna kweli mikarafuu haikubali tena pamoja na kuwa serikali ilitoa hoja kuwa haupandwi. Iliyobaki kwa Wilaya ya Mkoani labda ukanda wa Magharibi kwa wilaya yetu bado kwa kima fulani unakubali.

Sasa Mhe. Spika, bei mpya ya karafuu ilipotangazwa hivi majuzi kwa kweli imezua sokomoko katika kisiwa chetu cha Pemba. Mara nyingi kunapotokea mabadiliko ya bei kutoka ilivyokuwa na ikapanda juu wakulima wa karafuu ambao ndio tunawaita matajiri wa mikarafuu kidogo wanabadilika.

Mhe. Spika, Pemba kuna watu tofauti katika suala la karafuu, kuna wachumaji, kuna watu ambao wanaokota karafuu za chini na kuna watu pengine wanaofanya kazi ya kuanika tu. Sasa bei hii hivi sasa imeleta matatizo baada ya kuleta faraja. Kwa sababu wenye mikarafuu wengine tayari wanatembea na mapanga akimuona mtu kwenye mkarafuu wake anaokota hawako tayari watu waokote karafuu wala kuchumiwa kulingana na hii bei.

Sasa badala ya kuwa iwe faraja kwa kila Mzanzibari wanaomiliki wanataka iwe ni faida kwao peke yao kwa kweli ni tatizo. Mhe. Spika, pamoja na kuwa watu hawataki lakini tutoe onyo kuwa wasijichukulie sheria mikononi mwao. Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha kuwa neema inakuja na hatimae baada ya kutokea faraja ikawa ni matatizo kwa watu wa kawaida.

Mhe. Spika, hapo zamani tulikuwa tunahesabu kuwa Zanzibar zao lake kuu ni karafuu, mbata, nikisema neno hilo kuna watu mbata hawaijui kutokana na umri wao na pilipili hoho. Sasa mbata inatokana na nazi, karafuu inatokana na mkarafuu, mazao yote mawili haya pole pole yanaanza kupotea. Wazalishaji wakubwa wa karafuu ilikuwa ni kisiwa cha Pemba na wakubwa wanaozalisha mbata ilikuwa ni kisiwa cha Unguja.

Lakini leo maeneo ambayo ilikuwa yana minazi yanatoa mbata ndio viwanja vya kujengea majumba. Ndio maana Mhe. Assaa Othman Hamad aliyeondoka alisema kuwa Zanzibar kuagizia mafuta au mbata kutoka Msumbiji ni jambo la kusikitisha. Itakuja kuwa kama Pemba tukapanda mitende ikabidi Muscat waagizie tende kutoka Pemba pia ni jambo la ajabu vile vile.

Kwa hivyo, ni jambo la ajabu kwa Wazanzibari kuagizia mafuta ya nazi kutoka nje ya Zanzibar ambapo sisi ndio ilikuwa tunasafirisha mafuta ya nazi kwenda sehemu nyengine duniani. Kwa hivyo, mnazi ni lazima upandwe, ulindwe na uhifadhiwe, vyenginevyo tutapoteza zana zetu kuu za uchumi wetu.

Lakini Mhe. Spika, kwa vyovyote vile ku-retain mambo haya mawili kuyafanya kuwa ndio uchumi wetu tunategemea kufika. Lakini ile rasilimali ambayo bado hatujaifanyia kazi na kuitumia ningepomba serikali ivute soksi zake juu ili ipatikane kama ni moja katika uchumi wa taifa, nayo ni kuhakikisha kuwa mafuta yetu tunayachimba.

Mhe. Spika, tulifanyiwa semina hapa na tuliambiwa kuwa duniani kote hakuna nchi inayotegemea kilimo ikawa ndio ikaendelea kwa kilimo. Kwa hivyo, sisi kufanya kilimo kwanza tuendeleo, itakuwa tunakwenda kinyume na ile dhana ambayo watu wa kilimo wenyewe walipotufanyia semina, walitwambia kuwa hakuna nchi itakayoendelea kwa kutegemea kilimo. Sisi tumefanya kuwa tukwamuke kwa kutegemea kilimo, sasa sijui sisi ni vijembe kongoroka na matrekta matatu au manne ambayo Mhe. Waziri atayaagizia au kutafuta njia mbadala ya uchumi. Lakini mimi naamini kwamba kilimo hakitotutoa katika umaskini, pengine kinaweza tu kutusaidia kupunguza uagiziaji wa chakula, lakini sidhani kwamba itafika pahala tuweze kusafirisha na itusaidie kwa uchumi wetu wa nchi.

Mhe. Spika,

**Mhe. Spika:** Una dakika tano Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Tu. Nije kwenye uharibifu wa mazingira kwa uchimbaji wa mchanga, utumiaji wa misumeno ya moto, uchimbaji wa matofali. Sasa haya ni kweli Mhe. Spika, kwamba yanatuharibia mazingira. Lakini mimi nije kwenye mchanga, matofali na mawe. Haya Mhe. Spika, bado ndio nyenzo zetu za kujengea nyumba zetu. Ukikata mti unaharibu mazingira, lakini bado kuna watu wanajenga kwa kutumia miti. Ukichimba mchanga na kuchukua saruji kufanya matofali pia unaharibu mazingira. Kwa hivyo, serikali itafute nyenzo mbadala za kujengea nyumba. Kwa sababu haya yote yanayofanywa na watu wetu tukiwemo sisi, ukisikia mtu anajenga basi tunatumia vitu hivi. Lakini unapofanya hivyo ni kuwa unaharibu mazingira je, sasa tujenge nyumba zetu kwa kutumia kitu gani.

Mhe. Spika barabara zetu tunatumia fusi kwa kujenga barabara ingawaje kuna kima fulani kilichowekwa cha uchimbaji, lakini kwa sababu mahitaji yanaongezeka ya kila siku ni vyema serikali ikafikiria upya ili mazingira

yasiharibike zaidi, lakini na ujenzi uendeleo kwa sababu watu wanahitaji pahala pazuri pa kukaa.

Mhe. Spika, kwa kuwa umeniambia bado dakika tano, nafikiri bado dakika mbili hivi sasa. Nije kwenye huyu nzi anayeharibu matunda. Nashukuru kuwa katika mitego iliyotajwa imetajwa tu katika wilaya ya Mkoani na Mhe. Waziri kataja pia Wilaya ya Kaskazini. Lakini Kaskazini kuna Wilaya mbili Unguja, hakuainisha ni Kaskazini gani ni “A” au “B”. Kwa hivyo, hii mitengo ni muhimu kuletwa, lakini kasema kuwa inakamata nzi dume tu. Hivi jike naye akishapata mimba akizaa si atazaa dume pia. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nahisi kuwa hii mitego iwe inaweza kukamata nzi wote hao ili watokomee. Kama watu wa mazingira walivyoangamiza kunguru wa aina zote.

Kwa hivyo, na watu wa kilimo nao waangamize nzi wa aina zote ili haya matunda yawe salama. Kwa kweli sisi watu wa Wilaya ya Mkoani tukila embe iliyotoka katika wilaya yetu, ni lazima tule kizani, vinginevyo hutokula embe kwa mafunza yaliyo ndani ya embe.

Mhe. Spika, kwa kuwa pengine hizo dakika tano zimeshamalizika. Kwa hivyo, niseme kuwa naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia machache kuhusiana na bajeti hii. Kwanza namshukuru Allah kwa kutujaalia uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Pia namshukuru na nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa kuanza kazi katika bajeti hii ya mwanzo kihakika na kwa ari kubwa, ni jambo lisilotaka maelezo mengi. Jitihada yake aliyochukua ya kufikia maamuzi ya kuwapa nafuu wananchi katika pembejeo na bei ya trekta, ni jambo lililokuwa ni la aina yake. Tunamtakia mafanikio mema na kazi nzito aliyonayo.

Mhe. Spika, suala la kilimo ni suala la uhai, kwa hivyo tunapozungumza suala la uhai hakauna jambo lililolingana na hilo. Kwanza nije katika uzalishaji wa mazao kwa jumla ya kilimo. Mhe. Spika, mimi najua utendaji mzuri wa wizara pamoja na watendaji wote, lakini hivi sasa hali tunayokwenda nayo inahitaji ufuatiliaji mkubwa wa mazao yetu. Huko sokoni tunakokwenda kunapotezo la aina fulani au udanganyi wa aina fulani hivi unaweza kuuona. Nitatoa mfano Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hivi karibuni nilikwenda soko la Mwanakwerekwe, kiasi wiki mbili zilizopita, nilikwenda mapema sana ili niwahi na niweze kufanya na shughuli nyengine. Nilivikuta viazi vitamu vimepangwa na kwa sababu

nilizowea kula wali siku nyingi kutokana na mazingira yetu yalivyo basi nilipenda nivinunuwe siku ile. Lakini katika kuingiziwa ndani ya chombo, yule anayeua akaniambia vimekuja kutoka Iringa jana hivi. Hee! Hapo kidogo nilishtuka, nilitegemea viwe ni viazi vyetu kutoka Donge, lakini nikaambiwa kwamba vinatoka Iringa. Sasa hili ndio jambo ninalolisema kwamba linaweza kutupoteza kidogo. Tunahitaji kuingia kikweli kweli katika kilimo, ili tusipoteze yale malengo tukaona viazi vinaingia au matunda yanaingia tukafikiria ni yetu kumbe sio yetu. Sasa kwa njia hii naomba sana ile jitihada inayofanywa ya kupima mazao yetu yanayotoka basi izidishwe.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa ni mdau mkubwa wa kuchangia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Siku za nyuma ilikuwa ikiitwa Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Biashara tupate zile mizani kubwa kama wenzetu tutayapima vipi mambo yetu yanayoingia na yanayotoka. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili nalo alitilie mkazo zile mizani kubwa za magari zipatikane japo moja katika kile njia.

Mhe. Spika, hivi karibuni kuna jamaa walikuwa wakinitumia kwenye E-mail yangu. Kuna *articles* nyingi siku hizi zinatoka za kuhusiana na umuhimu wa haya mazao tuliyonayo. Hii *article* kubwa Mhe. Spika, kiasi *page* 8 hivi, umuhimu wa nazi tu na mambo yanayotokana na nazi. Halafu kuna nyengine ya ndizi na kuna nyengine ya viazi vitamu. Sasa wanasema kuwa vinachukua nafasi nzuri sana katika kilimo na hivi ndivyo vinavyotutoka. Nazi inatutoka, viazi vitamu hivyo ndio vinatoka Iringa, ndizi kwa bahati nzuri tunazo lakini tulipata magonjwa, tulipata ugonjwa ule wa sijatoka mpaka hivi leo baadhi ya migomba mingi ugonjwa ule haujatoka.

Mhe. Spika, kwa hivyo, naomba sana hiki kitengo cha utafiti kama kilivyoenezwa katika kitabu, basi vile vile kiendeleo na tafiti zake za maradhi mbali mbali ya mimea.

Mhe. Spika, nataka kumalizia hapa, lakini nasisitiza tena umuhimu wa kulima mazao manne haya. Mpunga, ndizi, viazi na kuimarisha minazi. Mhe. Spika, suala la pili nampongeza tena kwa mara nyengine waziri kwa kupunguza bei ya ukulima wa trekta. Lakini tulipotoka majimboni wananchi wetu wengi hawajui taratibu gani ili waweze kupatya hilo trekta, ndio lenye matatizo hasa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na haya irahisishwe sasa kila eneo kupangiwa siku maalum ya lile trekta kwenda kulima. Ndio hapa nampongeza tena kwa kuamua kuongeza matrekta, kwa sababu moja kati ya sababu kubwa pengine ni kuwa matrekta yenyewe hayatoshi. Lakini tunaweza kuwa na matrekta mengi, lakini hayakupangiwa ikawa yakaelema upande mmoja na wengine wakawa hawapati kwa wakati.

Mhe. Spika, moja katika tatizo kubwa liliopo katika wilaya huko ni kwamba hili trekta halina utaratibu maalum wa kwenda katika maeneo. Maeneo ya kilimo yale maafisa huwa wanayajua, kwa nini trekta lile huwa halipangiwi programu maalum. Hata kama mimi nitakwenda tu kufuatilia basi niambiwe kuwa tarehe fulani na tarehe fulani litakuwa katika jimbo au katika maeneo iwe hivyo.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri kuwe na *schedule* hasa ili tuweze kufuatilia kama *schedule* ile inafuatwa au laa. Lakini Mhe. Spika, kidogo imenisikitisha, kama itakuwa nimesahau au sikufahamu imenipita naomba radhi. Kwa sababu vitabu vyenyewe ndio kama hivyo tunapewa leo, akili ishike leo na mbao yote. Haya matrekta yana pahala pake pakutengenezewa karakana. Mimi nilikuwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi kwa miaka mitano tumepiga kelele kuhusu karakana za matrekta, namuomba Mhe. Waziri atueleze ushughulikiaji wa hizi karakana za matrekta umeishia wapi. Kulikuwa na suala la kwamba iwe shirika si shirika, iwe idara si idara je, katika mfumo mpya huu wa mabadiliko ya mapinduzi ya kilimo, karakana za matrekta moja iliyoko Mbweni na moja ilioko pale Machomanne Pemba zimewekwa katika kifungu gani na zimepata umuhimu gani katika mabadiliko haya.

Mhe. Spika, kuhusu wadudu waharibifu. Wako wadudu wa aina mbili Mhe. Spika, wako hawa ambao wanakuja na kuondoka. Kwa mfano mipunga mara hii utasikia imeingia wadudu na mwaka ujao haiingii. Sasa namuomba Mhe. Waziri atueleze ni utaratibu gani ambao unatumika ili kufuatilia wale wadudu ambao wanakuja kwa msimu, yaani wanakuja kwa kipindi fulani na kipindi fulani hawako. Maana Mhe. Spika, tunakwenda katika mashamba tunayaona, mipunga mingine imekuwa vizuri lakini mingine imedumaa na hali ya kuwa mvua waliyoipata ni ile ile ardhi pengine wote wametia mbolea, lakini huku wamefika wadudu wale lakini kule kwengine hawakufika. Sasa katika utaratibu wa kilimo cha mpunga wadudu hawa hufuatiliwa vipi au kama ni mahindi au kilimo chengine.

Mhe. Spika, nizungumze suala maalum kuhusu hawa nzi wa embe. Mimi binafsi Mhe. Spika, nimekuwa nikizungumza suala hili tokea kipindi kilichopita, nikasema kuna tatizo gani kulishughulikia kama vile ilivyoshughulikiwa malaria hapa Zanzibar. Kwa nini nikasema hivyo, hapa katika kitabu chake Mhe. Waziri amesema kuna mitengo mingine 43,000 kukamilisha Wilaya ya Mkoani kwa Pemba na Wilaya ya Kaskazini kwa Unguja. Lakini hizi wilaya hazikuwekewa pazia Mhe. Spika, wakati mitego ilipokuwa Mkoani hakuna iko Chake Chake, baina ya Chake Chake na Mkoani hakukuwa na pazia au kizuizi cha kuwafanya hawa wasiingie hawa. Mhe. Spika, ndio nikasema hii operesheni afadhali tusiifanye kuliko kuifanya nywiri nywiri Waswahili wanasema. Kwa sababu tukiifanya nywiri nywiri wale wa

huku wataingi huku na wa huku wataingia huku gharama kubwa itapita wala nzi hawaondoki. Sasa ndio hapo nikasema kwamba ifanywe kama malaria kupata *intervention* ya serikali, ikiwa bajeti ya wizara ya kilimo itafute *intervention* ya serikali ili hili suala limalizwe, lakini hivi litatumaliza sisi.

Mhe. Spika, ikiwa Pemba hakuna embe kuna njaa. Kwa sababu mtoto akirudi skuli akishapata embe zake tatu basi amuulizi mama kama kumeshapikwa au hakujapikwa. Sasa suala la kutuondolea embe kwa hawa nzi kwa kweli linaathiri sana, hali athiri ile biashara inayosemwa ya nje tu, lakini inaathiri hata ya ndani ya ndani. Ukija kwenye hili suala la kuzika embe kwa kweli sijui nani anayelifanya. Kwa kweli kuzika embe ni jambo gumu sana, uwende kukaa chini ya muembe ukangojea embe zianguke uzizike, hii kwa kweli ni ngumu sana ni lazima tulifikirie, ikiwa kuna uganga mwingine ufanywe. Lakini sidhani kama watu watazika maembe. Kwa yale ambayo yanapelekwa sokoni yakakataliwa basi yale yanaweza kuzikwa, lakini chini ya miembe. Kwanza watoto wanayapiga kisu wakayakwatua kwatua halafu wakalitupa.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba sana suala hili Mhe. Waziri aje na jibu rasmi la operesheni gani iliyopangwa na serikali hasa ya kulitatua suala hili la nzi wa embe. Mhe. Spika, ndio kama alivyosema Mhe. Asaa Othman Hamad, bahati mbaya sana ni kwamba hakuna tunda sasa lililobakishwa, tena matunda yanadumaa, watu wanajitahidi kupanda lakini matunda yanadumaa. Sasa sijui tutaifanya nini.

Mhe. Spika, twende kwenye Chuo cha Kilimo cha Kizimbani

**Mhe. Spika:** Kwa dakika tano Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Haya *Inshaallah*. Mhe. Spika, kwanza nashukuru sana kwamba Zanzibar inaendelea kuwa na chuo cha kilimo chake wenyewe. Kama alivyoeleza Mhe. Waziri kwamba kitaunganishwa na Chuo Kikuu cha SUZA, ambapo suala hili sisi tulilipendekeza zamani sana kwamba sisi Zanzibar ni nchi ndogo sana. Tunacho chuo chetu kikuu cha SUZA, kwa nini hivi vyuo vidogo vidogo kila kimoja kiwe na walimu wake, kiwe na mabodi yake na mambo yeke. Kwa nini haviunganishwi na SUZA ili ikapunguza gharama na ikaleta ule umoja wa vyuo na kubadilishana taaluma mbali mbali. Nashukuru sana kwamba suala hili sasa linafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, tuna visiwa viwili na kwa sababu Pemba ni *bread basket* ni sehemu ambayo inatoa chakula kwa wingi hasa cha matunda. Sasa kwa nini kuna uzito gani wa kuanzisha *annex* ya chuo hiki cha Kizimbani kule konde, ili hata hao wanafunzi wanapojifunza kilimo wakajua kwamba Zanzibar kuna ardhi za aina nyingi, nyengine ni hizi ziko Pemba ziko hivi kwa nini kule

wanazalisha ndizi kwa wingi, basi kutawapa fursa hata wale wanafunzi watabadilishana hawa walioko Kizimbani wanaweza kwa miezi mitatu kwenda kule wakazona zile ardhi. Lakini tukibakisha kila kitu hapa, inakuwa kuna mashaka. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri aje atueleze kuna tatizo gani hasa hatuwezi kuweka *annex* ya kile chuo cha kilimo kule. Konde kulikuwa na historia ya kuwa na kituo cha utafiti tokea enzi hiyo. Sasa kwa nini leo tumekwenda mpaka tumefanya chuo hakuna *annex* ya chuo cha kilimo kule.

Masuala mawili ya mwisho Mhe. Spika, sijui kama yamo humu au hayamo, lakini jambo moja ambalo sikulisikia ni *acreage* ya kilimo kwa Zanzibar. Katika kila wilaya tungependelea kujua kwamba je, ni ardhi kiasi gani ipo kwa ajili ya kilimo. Hili litawasaidia hata wao kutathmini kwamba ni kiasi gani sasa hivi imeshatumika na kiasi gani bado haijatumika na kuweza kuyalinda yale maeneo ambayo yana rutma ili yasiweze kuchukuliwa au kuvamiwa na majenzi na mambo mengineyo.

Mwisho kabisa kuna maeneo Mhe. Spika, ya kilimo mazuri tu, lakini yanavamiwa na bahari, maji ya bahari yanaingia katika ardhi ya kilimo. Je, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na taasisi zozote zile nyengine na wizara nyengine, ina mpango gani wa kuyahami maeneo hayo. Kwa mfano Tumbwe, Kisiwa Paza na kwengineko, ambako maji ya bahari watu wameshalima yanaingia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atupatie ufafanuzi wa suala hili kama liko katika medali yao ya kulishughulikia.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ziwayi, ambao kama nilivyosema wengi wao ni wavuvi na wakulima, wanahitaji sana huduma za wizara hii, wanamtakia kila la heri Mhe. Waziri ili wapate huduma nzuri. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia zote. Nikiamini kwamba Mhe. Waziri anao uwezo wa kunijibu maswali yangu niliyomuuliza. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Ahsante Mhe. Spika, lakini nitakuomba radhi sitosimama nitazungumza hapa hapa. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala aliyetuwezesha tukafika katika Baraza hili leo na tukawa tuko kwenye hali ya uzima.

Vile vile nakushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunigaiya nafasi kidogo nikazungumza angalau machache, kwa sababu mimi ni mwanakamati nataka nizungumzie tu kidogo na niunge mkono.

Pia Mhe. Spika, nampongeza waziri pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba hii waliyotuletea hapa nzuri na iliyopangika. Mhe. Spika, nampongeza



Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweza kujikita kutuletea mapinduzi ya kilimo na kuweza kutukomboa wanawake, wimbi hili hasa Mhe. Spika, ni la wanawake. Kwa hivyo, naunga mkono hoja kabla sijaichangia.

Mhe. Spika, hotuba hii jinsi alivyoisoma Mhe. Waziri, kama itakuwa sio lazima watu waseme basi hata tusingesema tena, kwa sababu mambo yote ameyamaliza katika kitabu chake. Mhe. Spika, mimi kidogo nichangie nianze katika ukurasa wa 37 kifungu 55, kuhusu mpango wa maendeleo ya kilimo cha mbegu.

Mhe. Spika, katika ukurasa huu unazungumzia mfumo wa makusudi wa mpango wa kilimo cha mpunga. Mhe. Spika, kilimo cha mpunga wanawake ndio hasa tuliokuwa tunafunga sheu yaani ndio walimaji wakuu kuweza kufanya kazi hii ya kilimo. Mhe. Spika, wanawake tunajitolea sana kwa kuweza kulima mpunga na mazao mengine mbali mbali ili kuweza kujikomboa kwa sababu sisi ndio walezi.

Kwa hapa Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kutuletea mbegu bora na itakayoweza kuhimili kishindo tulichonacho cha ukame. Tunajitahidi sana Mhe. Spika, kulima lakini ukame unaturudisha nyuma na maeneo haya tunayolima, wengine tunalima maeneo ya juu na wengine wanalima maeneo ya kwenye maji. Lakini Mhe. Spika, tunasema kuwa ardhi sijui tuseme imechoka au tuseme kuwa ni hizi mbegu tunazopanda ndio zimechoka au zimepitwa na wakati. Lakini mbegu hii tulioiona hapa ya NERIKA inaweza ikatukomboa kiuchumi jinsi wakulima tutakavyofaidika.

Mhe. Spika, wanawake tunajitolea kwa kulima kwa hali na mali, namuomba Mhe. Waziri aweze kutupatia pembejeo, tuwapate mabwana shamba kwa kutuelekeza. Hiyo mbegu tukiipata Mhe. Spika, ikiwa hatuna maelekezo basi tutalima kilimo chetu cha zamani pengine halipo litakalopatikana kiuchumi.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aweze kutuona na kuweza kutupatia pembejeo na mabwana shamba wasiwe mbali na kilimo. Kwa sababu Mhe. Spika, tunalima mpaka tunamaliza, tunapiga kelele kila siku. Hao mabwana shamba tunaoambiwa wanasomeshwa, sisi hatuwaoni vijijini. Tunajilimia ukulima wetu ule wa zamani, tunamwaga mpunga tunavyojua sisi wenyewe na matokeo yake baadaye hatuna chochote kinachopatikana. (*Makofi*)

Vile vile tunamuomba Mhe. Waziri kuna pembejeo nyingi za kilimo. Kwa mfano, tunawaona wenzetu kwenye *television* kwamba kuna majembe ambayo yanayokokokwa kwa mkono, mengine yanayolima kwa magari ya ng'ombe, ili na sisi tuondokane na kilimo hiki cha mkono, kwa sababu “ukilima pantosha

wavuna pankwisha” na mkono haulimi Mhe. Waziri, yaani jitihada yako utapigana utapata hiyo nusu eka. (*Makofi*)

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri uweze kutuona wanawake tujikomboe na kilimo, kwa ajili ya kuondokana na maisha duni tuliyanayo.

Mhe. Spika, kuhusu watu wetu wa utafiti na wao pia waweze kupata mafunzo ya kuweza kutuelekeza sisi, ili tuweze kufanya ile jitihada inayotakiwa.

Kwa mfano, kule kwetu Pemba tunayo mashamba ya kilimo, lakini bado mashamba yale nayo nayaona kwa miaka mingi sana hayana kazi yoyote inayofanywa. Mhe. Spika, tulikuwa na shamba la Mtakata ambalo lilikuwa ni zuri sana, shamba lile lilikuwa likifugwa ng’ombe na mawiza mengi yalikuwa yakipatikana pale, lakini hivi sasa shamba lile limepoteza hadhi yake, sasa sijui kama Mhe. Waziri ataliimarisha tena au vipi.

Mhe. Spika, kulikuwa na shamba la Dodoani Ole ambalo lilikuwa likizalisha mpunga mwingi sana, pia kulikuwa na mifugo na mbegu nyingi tulikuwa tukipata pale za kila aina kama vile mpunga, kunde, choroko pamoja na mambo mengi. Lakini naona ule utaalumu umeondoka na sisi tunahimizwa tulime kwa ajili ya Mapinduzi ya Kilimo na sijui kama tutakidhi haja hiyo. Kwa hivyo, nadhani ni vyema kupata maelekezo, ili kuweza kuondokana na huu umasikini.

Vile vile tupatiwe nyenzo, kwa sababu ukitaka kufanya jambo lazima uwe na nyenzo Mhe. Spika. Kwa mfano, mimi nitapewa shamba sasa baada ya kupewa siwezi kulilima nitalimia nini. Kwa kweli Mhe. Waziri matrekta ni kidogo, trekta zima litakuwa ni moja na kila pahala linalimiwa trekta hilo moja na pengine hata ukijakulima wewe muda ushakupita unachokipanda hakiji juu na wala hakipatikani.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri aweze kushajihisha lile Bonde la Msaani. Kwa kweli Msaani palikuwa pakizalishwa mpunga mwingi sana. Lakini hivi karibuni nimepita naona kunalimwa matuta ya viazi nadhani ule mpunga hata haulimwi tena. Kwa hivyo, tunaomba bonde lile kwa sababu lilikuwa likizalisha sana, yaani KJU walikuwa wakizalisha mpunga mwingi sana pale.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie vilimo vyengine, kwa sababu mtu halimi kilimo kimoja. Mhe. Spika, vilimo vyengine kama vile muhogo, naomba sana tuweze kuelimisha kuhusu kilimo cha muhogo, kwa sababu mbegu tulizonazo zimepitwa na wakati, kwani tunajilimia lakini eka nzima utavuna wiki na muhogo ule pengine ni mbovu au haukuzaa kabisa.

Kutokana na hali hiyo, tunaomba hizi mbegu zitakazokuweco kilimo, basi ziweze kufanyiwa bidii pamoja na kuwafikia wananchi wa maeneo tofauti wanaolima wote, kwa sababu bila ya kilimo hatwendi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunasema tena kilio kile kile kwamba wakulima wengi Pemba wanategemea kulima migombo, lakini hivi sasa migomba ina maradhi. Kwa hivyo, watafiti wetu waweze kufika mashamba kwa wakulima kwa ajili ya kutuona, kufanya utafiti na kujua tunaharibiwa na nini. Hivyo, kweli ule ugongo haufai au zile shamba zimechoka ama hata ile migombo wakati inapokaribia kutaka kuzaa inaingiwa na wadudu.

Kwa kweli hili ndio tatizo letu kubwa kwamba migomba ikikaribia kutaka kuzaa basi tayari inanyauka majani yote na kile kinachozaliwa basi hakileti tija yoyote.

Vile vile nizungumzie kuhusu Misitu. Mhe. Spika, tunashukuru sana kwamba rasilimali tunazo. Lakini tunakuomba Mhe. Waziri uwe makini sana, kwa sababu misitu inahama. Kwa mfano, tulikwenda kutembelea Msitu wa Ngezi na tulipata maelezo, msitu wanatoka watu mbali mbali ambao si wa Visiwa hivi na kufika pale kwa ajili ya kuingia, kuudhibiti na kuharibu msitu ule, kama vile kukata miti, kupasua vigogo na kuviweka.

Sambamba na hilo tulisikia kuwa alipatikana yule aliyekata na pia hatukujua kesi ile imekwenda wapi na baadala yake tumesikia ameachiliwa na vigogo vile havikuondolewa vikaachwa mule na kuharibika.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri uwe makini sana katika misitu yetu, kwa sababu ukame umeshakuwa mwingi na misitu ndio tunayoitegemea, angalau kupata rutuba ya mvua kama vile wiki wa siku moja ama mwezi kwa siku mbili.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la ulimaji wa viungo na hivi ni vilimo vidogo, kama vile kulima mihiliki, midalasini pamoja na mambo mengine.

Kwa kweli tuna masikitiko sana kwa sababu hatuna soko na vitu hivi watu wanalima. Kwa mfano, mdalasini, pilipili manga tunalima kwa wingi tena tunazo, lakini soko linatukwaza hatuna, mtu pengine anaweza kuwa na pilipili atazivuna zinazofika kilo 10, au 20 na hata 30 ataziweka ndani na kwenda kuziua dukani na kufungwa kivunge na wala hatuna pa kuzipeleka.

Kwa hivyo, tunaomba na soko pia ni mahitaji, kwa sababu sisi tunaolima tunahitaji sana masoko kwa ajili ya kupeleka bidhaa zetu, kwa lengo la kukidhi

haja na kupata kile tunachovuna, yaani kile kinatusaidia kwa kulimia, kutumia pamoja na mambo mbali mbali, lakini soko nalo ni tatizo.

Mhe. Spika, ukulima wa kumwagilia maji. Kwanza tunashukuru sana tumekwenda kutembelea mabonde ya hapa Unguja sehemu mbali mbali tunaona ule ukulima ni mzuri sana kweli, ambao pengine unaweza kutukombo baadala ya kulima mpunga mwaka kwa kilimo kimoja, basi mpunga ule tunaweza kulima mwaka labda mara mbili au tatu kutokana na ile mbegu ya miezi mitatu au minne.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri mabonde yakaguliwe tunayolima, ikiwa mabonde yale yanafaa basi tuweze kushajihishwa kuweza kulima kilimo cha kumwagilia, kwa sababu maji yapo pamoja na vyanzo vya maji vipo, isipokuwa bado hatujaimarishwa na tunapita tukiiona mipunga, lakini watu hawajui hata waanzie vipi.

Mhe. Waziri tunakuomba wanawake utusaidie kwa sababu ndio tunaoumia sana kwa kulea watoto, kutafuta malaji pamoja na mahitaji, kwani baba akiondoka asubuhi mpaka jioni.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa kutujaalia uhai na uzima, siku ya leo Jumamosi kuendelea na kikao chetu hiki, kujadili masuala yanayohusu masuala yanayohusu maslahi ya nchi yetu na watu wake. *(Makofi)*

Kwa kweli leo tunajadili Sekta hii muhimu sana ya Kilimo, ambayo kama alivyosema Mhe. Waziri kwenye kitabu chake inategemewa na takribani na asilimia 70 ya wananchi wote wa Zanzibar na kuchangia takribani asilimia 32 ya pato la taifa.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii na mimi pia kuwa mmoja wapo ya wachangiaji wa bajeti hii.

Mhe. Spika, wakati mmoja nilipewa mkasa mmoja, niliambiwa ilipokuja MV. Mapinduzi hapa, yaani ilipoletwa mara ya mwanzo kwa kweli ilikuwa ni kitu cha ajabu kwa Wazanzibari wengi kwa ule ukubwa wale pamoja na uzuri wake. Sasa kuna malenga mmoja wa Pemba aliingia kwenye ile meli na kuizunguka na alipotoka akaja na shairi na kibwagizo chake kinasema “MV. Mapinduzi Sijui Niseme Nini” *(Makofi)*

Kwa hivyo, na mimi Mhe. Spika kwa hotuba ya leo kutokana na uzuri wake nilikuwa najiuliza hapa isije ikawa hotuba hii nzuri sijui niseme nini. Mhe. Spika, kama ilivyokuja ile MV. Mapinduzi ilipokuja hapa ikawashangaza mpaka jamaa zangu wa Kisiwa cha Pemba kule.

Mhe. Spika, kwa utangulizi huo nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa *substances*, yaani inajieleza kwa kina kabisa kila eneo linaloguswa na sekta hizi basi nini wizara imejipanga kufanya na nini tutegemee kutoka kwa katika kipindi cha miaka mitano *Inshaallah*.

Mhe. Spika, kwa sababu hiyo kama walivyosema wenzangu na wa mwisho kabisa Mhe. Raya Suleiman Hamad aliposema kwamba pengine tungekuwa hatuna hata cha kusema, lakini ni wajibu kusema machache yale ambayo tunaona labda yanahitaji kuboreshwa.

Kwa hivyo, kwanza nimshukuru tena Mhe. Waziri kwa utangulizi wa hotuba yake jinsi alivyolizamisha suala zima la maridhiano katika nyoyo zetu. Kwa kweli hotuba nyingi zimelitaja suala hili na takribani zote zilizokuja. Lakini nathubutu kusema kwamba hotuba hii ndio imeizamisha dhana nzima ya maridhiano katika nyoyo zetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, labda niseme na wengi wanaweza kustaajabu imekuwa hivi na mimi sisitaajabu. Kwa kweli kuna watu wengi waliochangia kuleta maridhiano ya kisiasa wanatajwa, lakini niliwahi kusema siku moja Mhe. Spika kwamba kuna Kamati ambayo wengi hawaifahamu na ndio iliyoasisi hasa haya maridhiano baada ya kupewa kazi chini ya Mzee wetu Hassan Nassor Moyo Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu pamoja na afya njema. (*Makofi*)

Sasa leo niwape siri Mhe. Spika, mmoja wapo ya Wajumbe wa Kamati ile ya wa Sita na aliyetoa mchango mkubwa sana na mimi najua kwa sababu nilikuwa ni sehemu ya kamati ile ni Mhe. Mansour Yussuf Himid. Kwa hivyo, naomba nimpongeze sana kwa mchango wake ule mkubwa na leo hii tukiona hali hii tunayoiona katika Baraza letu Mhe. Spika, basi ni matokeo ya kazi kubwa iliyofanywa na watu kama Mhe. Mansour Yussuf Himid, hivyo nataka nimpongeze sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wale wengine waliobakia kama tulivyosema na *Inshaallah* historia inaandikwa na itakuja kueleza nani hasa walijitolea katika kipindi muhimu sana cha historia ya nchi yetu kuweza kutufikisha Zanzibar hapa tulipo sasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wengi wamesema hapa kwamba wizara hii tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika kipindi kifupi kabisa. Katika hili nampongeza sana

hakufanya makosa naamini kabisa alipomchagua Mhe. Mansour Yussuf Himid kuiongoza, alijua kwamba yale mabadiliko makubwa yaliyoonekana katika wizara aliyokuwa akiiongoza kabla, sasa yalipaswa yasimamiwe katika wizara hii muhimu sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri ametuambia kwamba Kauli Mbiu ya Mageuzi ya Sekta ya Kilimo kwa Zanzibar si Kilimo Kwanza isipokuwa ni Mapinduzi ya Kilimo. Vile vile ametutaka sote tushajihishe wenzetu kutumia Kauli Mbiu hili. (*Makofi*)

Naamini Mhe. Rais alipokuja na hoja hii au msemo huu, alikuwa akisisitiza umuhimu wa sekta hii katika maisha yetu ya kila siku. Mhe. Spika, hili halipaswi kutiliwa nguvu zaidi tukitizama hivi sasa.

Kwa mfano, ni juzi nilikuwa nikiangalia *television* ule upande wa naoitwa Pemba ya Afrika, yaani *Horn of Africa*, tayari kuna matatizo makubwa sana ya ukame na njaa, kwa kweli nilikuwa nikishuhudia katika *television* meli zikiteremsha mizigo ya chakula pale, wanasema inaweza kuwa na athari mbaya kuliko hata ile tuliyoishuhudia miaka ya 1980's ambapo tunakumbuka sote dunia nzima ilishajihidhwa kwenda kuchangia pale. Kwa hivyo, si jambo la kupuuzwa katika suala zima la kuzungumia umuhimu wa kilimo.

Mhe. Spika, nimesema kwamba nataka nipongeze mambo mengi yaliyokuwemo humu kuanzia hasa la msingi lile la kuja na Ukombozi wa Kilimo chetu kwa kuanzisha Mpango huu wa Kutoa Ruzuku, yaani kutoka *Subsidization* kwa wakulima wetu. Mhe. Spika, hakuna hata nchi moja iliyoweza kubadilisha maisha ya wakulima wao au iliyoweza kuleta Mapinduzi ya Kilimo katika nchi zao na hasa kwenye nchi yetu hizi za kimasikini kama hatukuleta Mfumo huu wa kutoa *Subsides* kwa Wakulima wetu. (*Makofi*)

Kwa kweli hata hizo nchi zilizoendelea mafanikio makubwa waliyonayo yanakuja, kwa sababu wanalinda wakulima wao kwa kuwapa ruzuku katika pembejeo, mbolea pamoja na huduma mbali mbali. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ndio maana wanakuwa na vita kama alivyosema Mhe. Waziri na baadhi ya nchi zetu tukiendesha mfumo kama huu, kwa sababu wanaona utapelekea pia gharama za uzalishaji kwa wakulima kuwa chini na kuweza kuzalisha kwa tija. Lakini wao wanawalinda wakulima wao kule, sasa wanakuwa wakali sisi tunapotaka kuwapa motisha kama zile wakulima wetu. (*Makofi*)

Kutokana na hali hiyo, nafurahi tena napongeza kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba inahitaji serikali makini na jasiri kuweza kufanya uamuzi kama ule. Hivyo kwa serikali hii kuweza kufanya maamuzi yale, basi nawapongeza sana

Baraza zima la Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuja na uamuzi wa kijasiri huo ambao wameuonesha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama nilivyosema pengine kwa sababu hiyo kuna mambo mengi yamejikita humu ndani. Kwa mfano, kuanzia katika kufufua mikarafuu, kuwapa hizo pembejeo zote wakulima, kuteremsha bei za huduma hizi, lakini sipati eneo moja moja la kuweza kusema kuna kitu kikubwa cha kuboresha.

Sasa Mhe. Spika, ninachotaka kukizungumza kwanza kuna hili suala zima la miradi ambayo imetajwa ambayo kiasi kikubwa inategemewa kusaidiwa na washirika wa maendeleo kama ilivyo sekta nyengine. Kwa hivyo, katika hili nina wasi wasi na ndio mchango wangu mkubwa upo hapa Mhe. Spika na namuomba Mhe. Waziri anisaidie.

Katika ukurasa wa 14 hadi 16 wa kitabu hiki cha hotuba ametaja pale miradi hiyo. Sasa kwenye ukurasa wa 14 ameeleza kwamba katika kutafuta msaada wa Washirika wa Maendeleo wanashirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Setka ya Kilimo inayoitwa *Agricultural Donors Working Group*.

Vile vile ukienda mbele kwenye ukurasa wa 25 kunazungumziwa Mradi unaoitwa *Program* ya Uimarishaji Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani ya Mazao na Huduma ya Fedha Vijijini.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 28 pamezungumziwa huu Mradi unaoitwa *Tanzania Agriculture and Full Security Investment Plan*. Kwa kweli hizi ni *programs* tofauti Mhe. Spika katika maeneo tofauti ya wizara hii, lakini nimeona nizichanganye kwa sababu zote zinahusu kupata msaada au kuungwa mkono na Washirika wetu wa Maendeleo.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu unakuja na namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwamba tunauhakika gani wa kuzipata fedha hizi hasa nimechagua haya maeneo matatu kwa sababu hizi zinaonekana zinapitia katika miradi mikubwa ambayo inajumuisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa hivyo, nasema hivi kwa sababu tunayo *experience* Serikali ya Jamhuri ya Muungano inao mradi mkubwa unaoitwa *Agricultural Sector Development Program (ASDP)*. Mhe. Spika, mradi huu umeombwa kwa jina la Tanzania na unachangiwa na Washirika wa Maendeleo ule unaitwa siku hizi wa *Basket Funds*.

Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tukichangia bajeti kubwa hapa tulimuuliza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo juu ya

*component* ya misaada ya inayotoka kwa Washirika wa Maendeleo nje ya *General Budget Support (GBS)*, ile ambayo inayokuja kissekta na huu ni mmoja wapo. Kwa kweli tuliuliza mahsusi kwa ile miradi inayohusu sekta ambazo si za kimuungano, hivyo tunategemea ile ikija inakuja kwa jina la Tanzania inapaswa ifaidishe pande zote mbili za muungano.

Sasa kuna mradi unaitwa *Agricultural Sector Development Program (ASDP)* na ukienda kwenye mtandao unapata waraka mzima wa Serikali ya Muungano kuhusu mradi huu. Kwa kweli nimeuchapa Mhe. Spika na katika ukurasa kuanzia 35 kwenda mbele kuna kifungu kinachozungumzia *flow of funds*, yaani mtiririko wa mapato.

Mhe. Spika, katika ripoti hii kuna jaduveli ya 5 na 6 zinazungumzia fedha ambazo zimetengwa katika sekta hii. Kwa hivyo, amesema pale *in millions* na yako mengi lakini sitaki kuyagusa, isipokuwa nitaligusa hili moja tu, mchango wa Washirika wa Maendeleo wa kwa mradi wa *Agricultural Sector Development Program* kwa jina la Tanzania ni bilioni 311,172,000,000/=.

Kwa hivyo, *breakdown* yake akiitaka Mhe. Waziri naweza kumpatia iko katika mradi huu na pengine yeye mwenyewe ameshaiona, kwa sababu nimesema iko katika mradi huu kama nilivyosema inapatikana katika mtandao.

Sasa hoja yangu ni kwamba katika hizi sisi Zanzibar tulipata kiasi gani, kwa sababu taarifa niliyonayo na kama si sahihi, basi namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisahihishe ni kwamba sisi Zanzibar tunapokwenda kuomba misaada kwa ajili ya kilimo kuunga mkono juhudi zetu hizi tunaambiwa kuwa tayari Tanzania na hao ni Washirika wa Maendeleo tukiondoa hizi taasisi kama za kibenki, hawa wengine wanasema sisi tunatoa kupitia *Basket Funds* ya jina la Tanzania.

Mhe. Spika, ndipo pale nilipouliza na tunaendelea kuyauliza kila siku Mhe. Spika, kwa sababu hakuna sekta itakayoigusa ambapo hatuathiriki. Kwa hiyo, katika hizi nataka Mhe. Waziri anisaidie je tumefaika na kama hatukufaidika basi hapo ndipo penye hoja yangu. Sasa ikiwa hatukufaidika katika hizi hii.

Hivyo, kuhusu miradi mingine mitatu ambayo Mhe. Waziri ameitaka kwenye hotuba yake kuanzia huu ambao anaosema atatumia *Agricultural Donors Working Group* katika ukusara wa 14 wa kitabu cha hotuba yake. Vile vile ule aliouzungumza kwenye ukurasa wa 25 niliuousoma hapa *Program* ya Uimarishaji Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani ya Mazao na Huduma ya Fedha Vijijini kuhusu na zimetajwa faidi nyingi pale, lakini zimezungumzwa kwa jina la Bara na Zanzibar. Sasa nikasema kwamba hizi



fedha alizotutajia Mhe. Waziri hizi ni za Zanzibar peke yake au za Serikali ya Jamhuri ya Mungano na Zanzibar itapata sehemu yake ama vipi?

Mwisho kule kwenye ukurasa wa 28 ambapo kama nilivyosema unaitwa *Tanzania Agriculture and Full Security Investment Plan (TAFSIP)*. Mhe. Spika, huu wa mwisho ni muhimu zaidi kwa sababu huu ndio unaohusu hilo lililozungumzwa na watu wengi hapa la kuanzisha Ghala ya Akiba ya Chakula. Kwa hivyo, kama na huu tunategemea huko na halafu baadaye zinapoingizwa kama zilivyoingizwa hizi pengine hatupaki kitu sisi, hivyo tunapata wasi wasi juu ya utekelezaji wa miradi.

Mhe. Spika, niseme wasi wasi wangu huu umekuja na pia nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie, kwa sababu wakati nipokuwa nikimsikiliza kwenye hotuba yake mwisho kwenye ukusara wa 69 kuhusu fedha za miradi ya maendeleo, alituambia kwamba wamepanga kutumia fedha kutoka fungu la SMZ na wala sitaki kulihoji kwa sababu limechangia kiasi kivuzi tu kwa asilimia 76.13.

Lakini alisema mchango wa Washirika wa Maendeleo ambao ulipaswa uwe bilioni 7,187,132,000 huu zilizoingiwa na wizara iliyopokea ni bilioni 2,296,067,287 ambazo ni sawa na asilimia 31.95.

Sasa nilikuwa najiuliza huku kupata kiasi kidogo mno cha asilimia 31.95 cha fedha za Washirika wa Maendeleo. Je, kulitokana na kujiwekea makadirio makubwa ambayo tulitegemea zikitoka huko ambazo hazikuja ama kulitokana na sababu nyengine ambazo labda ziko ndani ya wizara zilizopelekea fedha hizi zisipatikane na kupatika kwa kiwango kidogo sana?

Katika hilo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie maelezo kwa maana zote mbili, kwa sababu ya kuathirika huku kutokana na kutokupata *components* zetu ama kutokana na utendaji wa ndani ya wizara umepelekea kushuka au Serikali ya Zanzibar haiku-*meet obligations* zake naomba na katika hili anisaidie.

Mhe. Spika, nimechangia sana kuhusu Washirika wa Maendeleo kwa sababu kama nilivyosema katika miradi mingi nimeridhika na maelezo mazuri ambayo aliyokuja nayo Mhe. Waziri. Vile vile na hapo nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu naona kama ni *challenges* ambazo zinazotukabili katika kupata fedha hizi. Kwa hivyo, nataka nimpongeze sana kwa kufanikisha Washirika wa Maendeleo kuelekeza nguvu zao Zanzibar.

Kwa mfano, moja ametaja kwenye hotuba yake kwamba katika Mradi huu wa *Feeder Future* ambao unafadhiliwa na Wamarekani kupitia *USAID*. Kwa kweli

Mhe. Waziri alikwenda Dar-es-Salaam kuwasilisha ikiwa ni sehemu ya mpango mzima wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika muungwana huwa hajisifu, lakini niwape siri katika watu waliokwenda kuonana na Mama Hilary Clinton nimenong'onezwa kwa kutumia kofia yangu nyengine kwenye chama kwamba Mhe. Waziri Mansoor Yussuf Himid alijenga sifa kubwa sana ya Zanzibar wakati ikijieleza mbele ya mama huyu. (*Makofi*)

Kwa hivyo, hata Serikali ya Marekani kupitia kwako walisema kwamba Zanzibar inaonekana imejipanga vizuri zaidi katika hili la uhakika wa Chakula na Lishe Bora pamoja na mipango mizima ya kuimarisha Sekta ya Kilimo na ndio maana wakakubali mpaka kuja kuanzisha ofisi Zanzibar hapa na kukubali kuendelea kutoa msaada mkubwa kwa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nimalizie kidogo katika suala la mambo ninayotaka maelezo. Kwanza namuomba maelezo kwenye ukurasa 27 kuhusu suala la kutoa Misaada ya Kifedha kwa Wakulima Vijijini (*Microfinance System*). Vile vile katika hotuba yake mwanzo alizungumzia kuanzishwa kwa *Agricultural Development Funds (ADF)*. Kwa hivyo, naomba kujua kwamba kuna uhusiano wowote baina ya *Agricultural Development Funds* na hii misaada ambayo itapelekewa vijijini ama huu utakuwa unasaidia wizara na utendaji wake na huu mradi unaosaidia utakuwa tofauti.

Mhe. Spika, pia nilikuwa naomba atueleze kidogo, yaani atupe mwanga zaidi kwamba misaada hii ambayo amesema ni hatua za mwanzo kuelekea katika kuanzisha Benki ya Wakulima. Sasa itasaidia vipi wakulima na itafanywa katika utaratibu gani? Katika hilo naomba atueleze.

Kwa hivyo, namshukuru kuhusu suala la Makurunge leo ametupa maelezo ya kunitosheleza kidogo kuliko yale niliyoyapata jana katika suala la hadhi ile ya Zanzibar katika shamba lile. Sasa amesema kwamba tumeambiwa tutapewa Hatimiliki kwa zile hekta elfu 600.

Kuhusu masuala ya maliasili na mazingira Mhe. Spika, naomba niungane na wenzangu tu na mimi kumtaka Mhe. Waziri alitizame sana suala zima la utumiaji wa misumeno ya moto hii, ambalo mwenyewe amelitaja pale, kwa sababu hii inaonekana inaimaliza nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wakati mwingine ilikuwa inaonekana kama Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inayoshughulikia masuala ya mazingira ilikuwa inazungumzia kupiga marufuku kabisa, wengine wanasema hapana kwa sababu

kuna baadhi ya maeneo kwa mfano mti umeanguka njiani kuna haja ya kupata msumeno wa moto kwa ajili ya kuondosha haraka.

Sasa ule udhibiti wa matumizi yake Mhe. Spika, atusaidie wanajipanga vipi, ili kuona kwamba misumeno hii ya moto haimalizi miti yetu hapa Zanzibar.

Vile vile katika suala la mazingira kuhusu utumiaji nishati mbadala, yaani suala zima la kushajihisha matumizi ya gesi. Mhe. Spika, nadhani hili tukifanikisha kulisimamia vizuri basi linaweza kupunguza sana utumiaji wa makaa na kuni na hivyo pia kupunguza kukata miti yetu. Sasa kama ni hiyo, ametaja pale kwamba kuna familia 1600 ambazo zimesaidia gesi kwa njia ya ruzuku kupewa bure kwa kuanzia, ili kuwashajihisha waweza kutumia wwenzi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nataka kujua kwa mwaka ujao wa fedha na miaka mingine ijayo tumejipanga vipi kushajihisha zaidi hili la nishati mbadala, kwa sababu amesema pale kwamba serikali inafikiria kuondosha ushuru na kodi katika vifaa ambavyo vinatumia hivi kama vile majiko na mambo mengine.

Mhe. Spika, suala hili la kufikiria nadhani serikali isiendeleo kufikiria tena, lakini ije na mkakati hasa wa kuona inapunguza ushuru katika maeneo haya, ili tuwashajihishe kweli watu wetu na iwe rahisi kutumia vifaa hivi kuliko kutumia makaa na kuni. (*Makofi*)

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nimeona kitu ambacho ni kidogo sana, lakini katika umakini wa Baraza lako na kuonekana unafanyakazi vizuri. Katika kifungu cha matumizi ya maendeleo Mhe. Waziri ameliomba Baraza limuidhinishie shilingi bilioni 8,183,631,000/= kwenye ukarasa wa 72, lakini kwenye kitabu cha *Estimate* ya Bajeti ya Maendeleo kuna upungufu kama wa shilingi 50,000/=. Kwa hivyo, katika mahesabu ayaweke sawa, kwa sababu kuna shilingi 8,139,849,000/=. Nadhani ni vyema hesabu hizi zikaoana, ili tutakapokuja kupitisha vifungu vionekane havikutofautiana baina ya hotuba na kitabu hiki.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nawashukuru tena nampongeza sana Mhe. Waziri kama nilivyosema mipango mizuri na tunataka kuona utekelezaji, lakini mimi binafsi sina wasi wasi kwa kumjua Mhe. Waziri Mansoor Yussuf Himid kama alivyoleta mabadiko makubwa alipoisimamia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, basi naamini kabisa katika wizara hii ataweza kutuletea mabadiliko kama hayo. Kwa hivyo, nampongeza nakumtakia kila la heri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nakushukuru na ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Kilimo na Maliasili, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kufika hapa nikawa mzima wa afya na kuweza kuchangia bajeti hii, kwa leo sina mchangia mkubwa isipokuwa nchangie Ukurasa wa 41 kuhusu matatizo ya kilimo na matatizo ya maji ya kumwagilia katika mashamba yetu.

Mhe. Spika, tatizo kubwa la jimbo langu la Koani hivi sasa lina matatizo ya maji kwa ajili ya kumwagilia mashamba kwa ajili ya kilimo, nikiangalia sehemu kubwa ina mabonde mazuri ya kilimo lakini matatizo makubwa tunayapata kutokana na matatizo ya maji. Nikiende kama Tunguu pameitwa Tunguu pale kwa ajili ya uwezo wa kulima vitunguu lakini utakuta tunashindwa kufanya hayo kutokana na matatizo ya maji, namuomba Mhe. Waziri kama alivyofanya kupunguza punguzo la mbolea kwa wananchi basi na sisi atuangalie sana kwa kutupatia visima vya maji katibu na maeneo ya kilimo ambayo tunalima mboga mboga.

Hivi sasa shehia zetu ya Bungi, Kikungwi, Machui, Ubago, Kitumba humo mote tunalima mboga mboga lakini matatizo makubwa ni kukosekana kwa maji, kama tungelipata visima vya maji basi ningelisema Zanzibar kwa masuala ya mboga mboga tayari tungelijitegemea bila ya kuagiza kokote kule.

Sasa nakwenda katika kifungu namba 42 Tatizo la msitu wa hifadhi, msitu wa hifadhi shehia ya Unguja Ukuu Kaebona kulikuwa na msitu mkubwa sana ambao wananchi wa kule wanalima kwa muda mrefu sana, lakini utakuta muda wote hifadhi ya misitu ya Minai imezulia Shehia ya Unguja Ukuu Kaebona kuweza kulima maeneo yale kwa ajili ya fadia ya wananchi, kwa hivyo ningelimtaka Waziri atuhakikishie kwamba lile eneo la kilimo la Unguja Ukuu Kaebona ni lini litaachiwa wananchi wenyewe kuweza kulima kilimo walichozowea cha maweni, kwa sababu Unguja Ukuu Kaebona ni sehemu ambayo inajitegemea kwa kilimo cha maweni kwa muda mrefu sana hasa kwa mazao yake ya Viazi tona, ndizi za koroboi, choko ni vitu ambavyo vilikuwa muda mrefu shehia ile inajitegemea kwa kilimo hicho na ilikuwa hakuna kununua vitu kama hivyo, ukenda tona ni kupewa zawadi tu hakuna kununua, koroboi ni bure hakuna kununua.

Sasa tokea kunyang'anywa hifadhi ile ya kulima mpaka leo wananchi hao wanapata matatizo na kupata umasikini kwamba mazao waliyozowea hapawati kuyalima na wanaishi katika njaa kali hivi sasa, ningelimuomba Mhe. Waziri achukue hatua mwenyewe ya kwenda kuitembelea shehia ile na kwenda kuona hiyo sehemu ya hifadhi, vipi inaumiza shehia ile kwa kilimo kwa ajili ya kuwapa nguvu shehia ya kusini ambako kunafungwa kima punju na fedha ile ya Kimapunju haifikii kwenye shehia ile. Kwa vile shehia ya Wilaya ya Kusini

ndio yenye kima punju hii shehia ya Wilaya ya kati ingeliachiwa iendelee na kilimo na iondolewe katika hifadhi kabisa.

Mhe. Spika, hivi leo wananchi wengi wamefurahia sana kumsikia Mhe. Waziri kutoa punguzo kubwa la mbolea katika nchi yetu ya Zanzibar, kwa sababu mimi mwenyewe sina historia ya kusikia kitu chochote cha kilo hamsini kusikia kinauzwa kwa shilingi elfu kumi ni mara ya kwanza kuona jambo kama hilo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi hizo alizozifanya kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile namuomba Mhe. Waziri atie mkazo zaidi kama alivyopunguza bei ya mbolea angalipunguza na angelitangaza bei ya muhogo mkavu kwa ajili ya kuweka akiba kwenye maghala yetu, kila paketi ya kilo hamsini itanunuliwa kiasi gani kwa ajili ya hifadhi ya njaa itakapotokea Zanzibar tuhakikishe Muhogo mkavu tunaweza kukaa hata mwaka mzima tukawa na hifadhi hiyo. Ningelishukuru sana Mhe. Waziri akaweza kuyatangaza mambo mengi ya vyakula ambavyo vinaweza kupata bei ambavyo hivi sasa vimeshuka bei sana, kama hivi sasa vitu vingi vimeshuka bei kwa sababu hatuna hatuna bei ya uhakika ya kuweza kuuza, utakuta kama viazi vitamu hivi sasa sisi watu wa Mwera Pongwe tunatoa vingi sana, lakini utakuta bei imeshuka sana.

Kwa hivyo angelitutangazia bei ya kilo hamsini itauzwa kiasi gani viazi vitamu basi tungelihakikisha kwamba sasa Zanzibar tumeweza kushusha bei na tumeweza kupandisha bei baadhi ya vitu tungelikuwa na nguvu ya kilimo kwa muda wote.

Mhe. Spika, kwa leo sitokuwa na mchango mkubwa isipokuwa mchango wangu ni mdogo sana lakini wa haraka haraka , mimi na wananchi wangu wa jimbo la Koani tunaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana (*Makofi*)

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutia baraka zangu japo kwa uchache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mhe. Spika, marehemu baba wa taifa alisema ili tuendelee tunahitaji mambo manne, tunahitaji tuwe na siasa safi, uongozi bora, watu, Ardhi na yote hayo tunayo na Ardhi ndio lengo la kilimo. Kwa hivyo tuna kila hali ya kupata matumaini sasa kwamba tunaelekea kwenye maendeleo.

Mhe. Waziri kwenye kitabu chake katwambia asilimia sabiini ya Wazanzibari ni wakulima, Wazanzibari wanakitegemea kilimo kwa kujikimu kimaisha kwa chakula, lakini pia Wazanzibari wanakitegemea kilimo kwa ajira ya kujipatia

rizki sasa pahali palipokuwa na tegemeo la asilimia sabiini sio pahali pa kufanyia mchezo ni mahali panahitaji mipango na miradi mikubwa mikubwa ambayo kwa kiasi fulani kama nilivyosema kwa sababu t una uongozi bora mambo haya yanakwenda vizuri.

Kwa kweli Mhe. Rais kaonyesha nia ya maendeleo hayo na katika hili basi nilisema nitumie fursa japo ya dakika moja kumpa pongezi sana Mhe. Rais kwa kutayarisha au kwa kuona kipaumbele hichi cha mapinduzi ya kilimo, Mhe. Spika, katika nchi yetu hatuna chaguo katika suala hili la kilimo kama ambavyo tumeelezwa katika kitabu na tumeelezwa katika hotuba mbali mbali za viongozi wetu kwamba sasa hivi uagizaji wa mchele umekuwa ni tatizo gumu, kwa sababu mchele umepanda bei sana duniani na hakuna njia ya kuufanya uwe rahisi isipokuwa ni kuzalisha wetu humu nchini. Kwa hivyo mimi namsifu sana Mhe. Rais kwa kuchagua hili kama ni njia moja ya kuwasaidia Wazanzibari.

Lakini pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa utayarishaji wa hiyo hotuba ya bajeti, hotuba hii unaweza kuitofautisha na hotuba nyingi nyuma za miaka iliyopita ni hotuba ambayo inaleta matumaini san asana kwa wakulima. Kwa kweli mimi nilipokuwa nasikiliza hotuba hii ya Mhe. Waziri nilisema mimi nisimame wala nishauri wala nisikosoe lakini nsimame hapa kwa kumsifu kwa kazi yake nzuri. Hotuba hii nimejaribu kuangalia sekta hii ya kilimo tu Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wamezingatia mambo mengi sana ambayo ni muhimu sana katika mahitaji ya kilimo hichi ambacho tunakusudia kwenda nacho sasa hivi, nimeona mle kuna mbegu bora, kazingatia pembejeo na madawa, kazingatia matrekta, kazingatia hata ruzuku za wakulima na mitaji, bei za pembejeo zimepunguzwa kwa kiasi kikubwa sana, kazingatia mipango ya *irrigationi* ambayo ni muhimu kweli kweli, kazingatia taaluma za wakulima, kuhifadhi wa mazao yasiharibike kazingatia mambo mengi tu.

Sasa kwa kweli huwezi kusema sasa ushauri nini katika hili isipokuwa ni kumpongeza tu, ila mimi nilitaka nishauri jambo kidogo ambalo haligusi wizara yake moja kwa moja , lakini mambo mengi katika serikali ni mambo mtambuka yanaguza kila sekta, mimi nilikuwa nadhani Wazanzibari kwa kuwa sasa tuna nia thabiti ya kupiga hatua ya maendeleo basi tunahitaji kujipanga kwa kila sekta sisi sasa tunalenga kuitumia ardhi yetu kwa kilimo lakini lazima tukubali Mhe, Spika, ni muda mrefu ardhi yetu hatukuwa tumeipangia mipango mizuri na kwa sababu hiyo tukawa tumewaachi watu wanaogolea tu mtu analima anapotaka, analima anavyotaka, anajenga anapotaka, anajenga anavyotaka.

Sasa jambo ambalo halikupangwa haliwezi kuleta tija nzuri sasa nilikuwa nashauri sana serikali kama kuna haja ya kufanya mapitio ya sera ya ardhi au kama kuna haja ya kukazia sheria maana yake nakumbuka tumeshapitisha kila kitu hapo lakini bado matumizi mazuri ya ardhi mimi binafsi sijaridhika nayo. Wazanzibari tunaongezeka kwa speed kubwa tunazaa sana Wazanzibari hiyo ni sifa yetu moja. Mhe. Spika, visiwa vyetu ni vidogo sana sasa kulikuwa na haja kubwa sana ya kupanga matumizi mazuri sana ya ardhi, mimi nilikuwa nadhani watafiti watwambie baada ya utafiti wao ni eneo gani la visiwa vyetu linafaa zaidi kwa kilimo na eneo gani la visiwa vyetu ambalo linafaa zaidi kwa makaazi ya watu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwa kweli Wazanzibari hatuna tena wakati wa kujenga hizi *horizontal* kwa sababu ardhi tutaimaliza na bado kutatokea mahitaji ya ardhi na watu watakuwa hawana pa kukaa tena na hawana pakulima tena , hawana pa kufanya *investment*, nilikuwa nafikiri sasa tuandae utaratibu wa kujenga *Vertical* tuende juu Mhe. Spika, wenzetu wenye ardhi ndogo kama yetu sasa hivi ndivyo wanavyofanya, ukenda pale Dubai mtu akitaka kiwanja huuziwa kiwanja juu ya nyumba ya mtu na mwengine huuziwa juu ya nyumba ya mtu vile vile. Sasa watu wanakwenda huko juu Mhe. Spika, ardhi ya kwenda hivi hakuna tena sasa na sisi kama tutakuwa tumefanya tathmini vizuri basi ardhi iliyopo sasa hivi haitutoshi tena. Kwa hivyo hili nilikuwa naomba sana kwa kuwa Mhe.waziri wa Kilimo kakusudia kufanya mapinduzi ya kilimo basi pia ashajihishe, serikali pia iandae utaratibu mzuri wa kumuwezesha hasa kuiipata hivo ardhi ya kuitumia kwa kilimo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilitaka niliseme kidogo sikuona katika kitabu cha Mhe. Waziri pahali alipogusia gusia habari ya mbolea ile ya samadi, Wazanzibari ni wafugaji wanafuga kuku, wanafuga ng'ombe, wakulima. Sasa sekta hizo zinazalisha sana mbolea ya samadi mara moja nilikuwa nasoma kitabu cha nyota ya rehema kitabu cha Shehe Said Ahmed Mohammed, katika kitabu chake alieleza sana habari ya mbolea ya samadi katika kuimarisha kilimo. Sasa nilikuwa nafikiri na sisi tuwashajihishe wakulima wetu badala ya kugharamika kutafuta mbolea hizi za kuagizia, lakini tunaweza kutumia mbole za mavi ya ng'ombe, mavi ya kuku, majani majani yale ya kilimo tukaweza kufanya *compos* tulivyokuwa kilimo tulikuwa tunafundishwa namna ya kufanya *compos* tunaweza kuzoesha majani yale hatimae tukapata mbolea nzuri sana kwa mambo ya mboga mboga. Sasa hili naomba watendaji walizingatie sana wataalam wa mambo haya ya kilimo haya.

Halafu Mhe. Spika, kuhusu hawa nzi wanaoathiri matunda nakumbuka hivi karibuni kulikuwa na huu mradi wa kuu hawa nzi wale, lakini ule mradi mimi nataka niseme ulifeli sana kwa sababu wale nzi wa kuharibu matunda wale sasa wameenea nchi nzima, kule kwetu Pemba hakuna pahali palipokuwa nzi wale

hawapo na ile mitego iliyokuja ililenga maeneo fulani fulani na kwa kweli ilifanya kazi kubwa ya kuua nzi. Lakini kwa sababu haikuenea nchi nzima mule mule ambamo tayari wale nzi wameshakufa basi wameambukizwa tena na sasa wamerudi kwa *speed* kubwa, sasa nilikuwa na ushauri hapa kwamba atukianzisha *project* kama ile basi ni afadhali tukae lakini tukianzisha tuwe na uwezo wa kuanzisha nchi nzima, kwa sababu zile pesa ambazo tulizitumia mimi nahisi zimepotea kwa sababu lengo halikufikiwa, sasa bora tutumie pesa nyingi lakini tukihakikisha tunauwa nzi tuwae wamalize na lile tatizo liwe limeondoka.

Jambo jengine Mhe. Spika, kwa kweli tuna athiriwa sana sana na wezi wa mazao juhudi za wananchi wanaojitegemea kwa kilimo zinarudishwa nyuma sana na wizi wa mazao mpaka kuna watu sasa hivi wamekata tamaa hata ya kufuga, wamekata tama hata ya kilimo kwa sababu mtu anafanya kazi kubwa sana katika kufuga, anafanya kazi kubwa sana katika kulima lakini hatimae matunda hayapati kutokana nawezi wale. Sasa katika hili nilikuwa ushauri mimi nina hakika Wazanzibari tunajuana sote na hawa wahalifu wanaoiba ng'ombe, Kuku, ndizi za watu wanajulikana katika mitaa wote hawa huo nido ukweli, sasa kwa sababu wanajulikana na kwasababu mgawanyo wetu wa madaraka unakwenda mpaka chini aliko sheha na siku nyengine so sheha tu lakini ana manaibu zake na kamati zake, alimradi utamkuta mtu anatawala nyumba chache sana.

Kwa hivyo watu waliomo katika eneo lake wote anawajia na tabia zao, sasa nilikuwa nashauri sana kwa sababu wahalifu hawa wanajulikana hebu serikali ichukue juhudi ya makusudi ya kuwakusanya hawa wakamatwe wote, wakishakamatwa wasiwekwe ndani wala wasifungwe lakini wapewe adhabu moja kubwa kweli kweli ya kuhakikisha kila mmoja ana eka mbili za kilimo, na ikiwa watapatikana wengi basi iwe ni ushirika wa wahalifu, tena wawe wanaangaliwa je wanalima kweli na kama ni kufuga wanafuga kweli wawezeshwe wafanye hivyo nafikiri wakishughulishwa kufanya hivyo watakuwa hawaibi tena hawa huu ndio ulikuwa ushauri wangu Mhe.Spika,. Lakini wakiachiwa tu hawa wahalifu watu watalalamika wanawajua ati huyu fulani anaiba lakini hakuna hatua zinazochukuliwa siku zote watakuwa wananrudisha watu nyuma hawa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni mwisho kabisa nataka nisema kwamba atumepoteza asset kubwa ya vyanzo vya maji, hii ilitokana na ile niliyoisema watu kuachiwa wakafanya wanavyoona wao ndio, ukulima usiokuwa wa kitaalam mimi nakumbuka nilipokuwa mdogo kule kwetu kulikuwa na mito mingi kweli kweli ile mito ilikuwa imetandwa na kama mapori fulani hivi, kuna miti *special* inaota kando kando ya mito halafu juu yake kunakuja miti ile inayotambaa mibungo inakava mle. Kwa hivyo unakuta ule mto unakuwa na



kivuli cha kutosha haupati jua wala haupati upepo maji yanayobakia mle yanaweza kukaa mwaka mzima hayamalizi. Lakini ukulima wetu ukatufanya ile miti yote tuikate sasa tulipoikata ile mito imekauka yote.

Sasa nilikuwa nafikiri Wizara ya Kilimo kwa sababu moja katika madhumuni makubwa ni uhifadhi wa vyanzo vya maji basi wakulima wetu wapewe taaluma na wahamasishwe kupanda miti ili kurudi kule kule tulikotoka tupate vyanzo vya maji ambavyo havikauki, yale mahandaki bado yapo lakini hayana maji. Kwa hivyo tupande miti mle halafu maji siku za mvua za msimu yaji yakiingia mle yawe hayatoki. Nchi yetu inapitiwa na misimu ya maji karibu mbili za mvua lakini maji yale tunayaacha yanapotea bure ambayo kama kungekuwa na utaalam wa kuyazuia yasiende baharini yangetusaidia karibu nusu mwaka mzima, kwa hivyo wizara hii pia iwe na changamoto ya kuwawezesha wananchi kuvuna maji ya mvua ili yatusaidie kwa kilimo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema humu hamna mambo ya kukosewa kosewa kwa hivyo mimi baada ya mchango huu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante (*Makofi*)

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi kuweza kutuwasilishia hotuba hii hapa leo.

Mhe. Spika, nianze kwa kupongeza Mhe. Waziri na wasaidizi wake kwa kutuletea hotuba hii ambayo leo hii imeanza kutuazisha mapinduzi ya kilimo, kwa kweli mimi nimefarajika sana kwa maneno haya, Mapinduzi ya kilimo lina maana pana sana kama ilivyo Mapinduzi Daima mwenyewe ametwambia pale Mhe. Waziri, mimi nimpongeze kwa hilo.

Kwa kujali muda niendeleo katika mchango wangu na nianze na ukurasa wa 25 kwenye *program* ya uimarishaji wa miundombinu na uongezaji samani ya mazao vijijini, kwa kweli mimi naunga mkono sana hatua hii ya kuanzisha mradi huu ambao utakuwa ni mkombozi kwa wakulima. Ukisoma haya maelezo ya hapa yanajitosheleza kuona kwamba ni namna gani serikali ilivyo jidhatiti kuweza kuwasaidia au kuwawezesha wakulima wetu ili waweze kufikia malengo yao. Katika hili mimi nimpe hongera Mhe. Waziri kwa kazi nzuri.

Mhe. Spika nikiendelea nakwenda haraka haraka kama ulivyotwambia twende kwa wepesi kidogo ili tuweze kuchangia wengi. Nasogea kwanye ukurasa wa 29, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kama alivyoeleza Mhe. Waziri katika

kitabu chake jukumu la idara hii husimamia masuala ya utawala, maslahi ya wafanyakazi na mafunzo. Lakini vile vile idara hii ina jukumu la kusimamia mali za serikali ambazo ziko chini ya wizara yake.

Mhe. Spika, mimi nina jambo naomba nimuulize Mhe. Waziri ili atakapokuja anipe ufafanuzi kidogo. Kuna eneo pale la *Living Stone* ambayo ilikuwa ni sehemu ya ghala la kilimo, kuna uzio wa mabati inasemekana eneo lile amepewa mtu binafsi. Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri juu ya suala hili kwamba ni kweli, na kama ni kweli naomba ule utaratibu ambao ulitumika mpaka kuweza kumpa mtu huyo. Mhe. Spika, kwa sababu hizi ni mali za wananchi na wenyewe wana hoji juu ya uhalali wa masuala kama haya, hivyo nilikuwa nataka kujua juu ya hilo.

Mhe. Spika, vile vile nisogee kwenye ukurasa 34 kwenye mpango maalum wa kuendeleza zao la mpunga. Mhe. Spika, kwenye hili mimi niipongeze wizara kwa kuliangalia kwa uwazi na kwa upana suala hili, kama ujuavyo mchele ni chakula chetu kikuu hapa kwetu na tunautafuta kweli kweli. Lakini kwa kweli Mhe. Waziri ameweza kutoa maelezo ya kina juu ya namna gani tutaweza kupunguza tatizo hili hasa la upandaji wa bei. Mhe. Spika, ni kwa kulima sisi wenyewe tukaweza kupunguza kuagiza ili bei iweze kushuka. Mhe. Spika, ni matarajio yetu sasa kwamba haya ambayo Mhe. Waziri ametueleza hapa utekelezaji wake utakwenda kama ulivyopangwa ili wananchi wetu waweze kupata nafuu ya chakula.

Mhe. Spika, pia niendeleo kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuelezea mpango wake kazi ule wa kuleta vifaa vya ukulima kwa ajili ya zao hili la mpunga. Mhe. Waziri ametueleza hapa kwamba mipango aliyonayo katika kuhakikisha kwamba wizara hii inaleta vifaa vya kisasa kwa ajili ya ukulima, uvunaji wa mpunga, uchambuzi pamoja na vitu vya kutwangia. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jambo hili kwa kweli yakikamilishwa haya mimi nafikiria ile dhana ambayo Mhe. Waziri ametwambia humu yakupunguza ule uagiziaji wa mchele kutoka nje nafikiri utafanikiwa. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na ametwambia jambo hili linaanza ndani ya mwaka huu, mimi namwambia ajitahidi sana na sisi tuko tayari kumpa mashirikiano kuhakikisha kwamba mambo haya yanapatikana kwa haraka ili wananchi wetu waweze kupata nafuu ule wa kuondokana na kijembe kongoroka.

Mhe. Spika, bado niendeleo kumpa pongezi Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii, na mambo yake mazuri aliyotuekea humu. Mhe. Spika, mimi nimefarajika sana baada ya kuona hatua ambayo serikali inachukua katika kupunguza bei za mbolea, dawa ya magugu pamoja na mbegu ya mpunga. Mhe. Spika, kwa kweli hili lilikuwa ni tatizo sana, kwani wakulima wetu sisi ndio tunaokaa nao kule walikuwa wakilalamika sana juu ya jambo hili. Pia mara nyingi kama

utaangalia kumbukumbu zetu hapa tumekuwa tukiihoji sana serikali ni namna gani itaweza kuwasaidia wananchi katika kupunguza bei ya matrekta kwa ajili ya kulima, kuvuruga, mbegu pamoja na dawa ya magugu.

Mhe. Spika, mimi naishukuru sana serikali kwa kutupunguzia bei hii ili wakulima wetu sasa nahisi wataweza kufaidika na kilimo cha kisasa, maana kama zana zile zitakuja basi bei hizi zitapungua naona mambo yatakuwa mazuri. Kwa hivyo, naipongeza sana serikali kwa kupitia Wizara yake hii ya Kilimo kwa jitihada inazoonesha kuwaletea maendeleo wananchi wake hasa kwa kuwapunguzia bei hizi za pembejeo. Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake hizo.

Mhe. Spika, nisogee mbele kidogo kwenye ukurasa wa 41 kwenye kilimo cha matunda na viungo. Mhe. Spika, kwenye kilimo cha matunda na viungo mimi niendeleze hongera zangu kwa Mhe. Waziri kwa kuligusa zao la manjano, zao hili katika jimbo langu lina wakulima wengi sana. Kwa hivyo, kwa kuliweka katika zao la biashara ina maana wakulima wangu watafaidika na zao hili na nina hakika hata bei itakuwa nzuri.

Mhe. Waziri hongera sana kwa hili nina hakika wananchi wa Jimbo la Mkwajuni watakupongeza sana kwa hili maana itakuwa umewasaidia, mara nyingi manjano yetu tulikuwa tunakuja kuuza Mjini tu. Na soko lenyewe mheshimiwa ndio kama unavyolijua halipo, hivyo imani yangu inaniambia kwamba zao hili litakapokuwa limeingizwa katika mtaala wa kibiashara nina hakika na mambo yao yatakuwa mazuri. Ahsante sana Mhe. Waziri maana leo nahisi kitabu hiki kazi yetu sisi kukupa hongera tu, hamkosi madoa mawili matatu kama wenzangu waliotangulia kusema, yamo kidogo lakini hongera zitakuwa nyingi zaidi.

Mhe. Spika, sasa nisogee kwenye ukurasa wa 50 kuhusu Chuo cha Kilimo Kizimbani. Mhe. Spika, chuo hiki kina kazi moja kubwa sana ya kusomesha vijana wetu kwa ajili ya matarajio ya kuja kuwasaidia wakulima wetu, nafikiri hiyo ndio dhamira yake kuu na serikali imefanya hivyo kwa kujua upungufu wa wataalamu tulionao. Lakini mimi kidogo nitoe rai nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu makusudio ya serikali ni kuhakikisha kwamba kila sehemu kunapatikana wataalamu.

Kwa hivyo, nilikuwa nina rai niombe kwamba wale watahaniwa wa kile chuo ingekuwa unatusaidia wanatoka ndani ya yale majimbo yetu ili kila jimbo liweze kupata wataalamu kwa sababu mtaalamu yule akimaliza kusoma atarudi katika jimbo husika akaweza kwenda kutoa utaalumu ule sehemu anayotoka. Mhe. Spika, kama vile ambavyo inafanya Wizara ya Afya hata Wizara ya Elimu kwa ajili ya walimu basi ningekuomba na wewe Mhe. Waziri hebu hawa

wataalamu usiwachukue tu kwa sababu wana sifa, ungeliangalia na yale maeneo wanayotoka ili tuweze kupata wataalamu katika maeneo yote ya majimbo yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele nisogee kwenye ukurasa wa 55 kwenye Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe kuhusu malengo ya mwaka amezungumzia Mhe. Waziri malengo yao katika idara hii ni pamoja na kukarabati maghala ya akiba manne ikiwa ni matayarisho ya hifadhi ya chakula ya taifa. Mhe. Spika, mimi nimepata shaka kidogo kwenye hili, maana mimi nahisi haya maghala kama yamekodishwa yote, sasa sijui Mhe. Waziri utakapokuja utasaidie hapa kwamba maghala haya unayo? Maana hapa umesema kukarabati ina maana yapo unataka kuyakarabati ili uweze kuyatumia kwa shughuli hizi.

Mhe. Spika, nafikiria tulipopita kwa mara ya mwisho katika wizara yako tuliulizia juu ya maghala haya, yapo ni makubwa tu lakini tulikuta pale yote yameshakodishwa na yana mikataba. Kwa hivyo, sijui utafanya vipi kuhusu hili kwa hiyo utakapokuja hapa Mhe. Waziri kidogo naomba utasaidie katika hili ili tuweze kuona utaratibu ambao utakaotumia kuweza kupata maghala haya.

Mhe. Spika, vile vile nizungumzie kwenye suala la upandaji wa mikarafuu kama ambavyo umeeleza kwenye hotuba yako hapa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alisema kwamba atashirikiana na Wizara ya Biashara kwa kupitisha Shirika lake la ZSTC katika kuhakikisha kwamba zao hili la karafuu linakuwa. Mimi napata shaka kidogo kwenye hili, maana huku tunafanya utaratibu wa kupanda, lakini je kuitunza hii ambayo ipo maana tunapopanda ndio tunaanza itakuwa midogo hii, lakini hii mikubwa iliyokuwepo tunaikata mno.

Mhe. Spika, mimi hivi karibuni nilikwenda Pemba kabla ya kuja kwenye kikao hiki nilikwenda kutembea. Kwa hivyo, nilipotemka meli pale Mkoani na nilikuwa nakwenda mbali Wete, kwa hiyo kila nikipita na gari njiani nikawa ninashangaa mimi jinsi mikarafuu inavyokatwa. Kwa hivyo, leo nikawa najiuliza huu mkakati wa Mhe. Waziri utatimia maana nilipitia kuanzia maeneo ya Mtuhaliwa, Mtambile mpaka Chanjamjawiri huku nakuta rundo za mikarafuu tena mengine mibichi kabisa zaidi ya mizigo 1000 ya kuni za karafuu ina maana ile ni mirafuu mibichi imekatwa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ukiangalia hilo na huu mkakati ambao tunaukusudia hapa katika mwaka huu sijui utatueleza nini juu ya suala hili. Mhe. Spika, nilipotoka tena kutoka Chake Chake kwenda mpaka Wete kuanzia Mzambarauni, Tungamaa mpaka Wete wenyewe basi nilikuta zaidi ya mizigo 2000 kwa hesabu ya haraka haraka ya kuni za mkarafuu. Nayo ni vile vile mengine mibichi kabisa, hebu Mhe. Waziri tueleze hasa mkakati ulionao juu ya watu wa namna hii. Kwa sababu kama hii mikubwa ndio inakatwa hii midogo

ndio kwanza mnataka kuipanda, hivyo mpaka hii ijekuwa tayari kuanza kuvunwa si tutakuwa ndio hatuna kitu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja tupe mkakati wa wizara juu ya hili na ni hatua gani hasa utakazochukua juu ya watu wa namna hii.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nimalizie juu ya Idara ya Misitu na Mali Asili Zisizohamishika kwenye Mradi huu wa HIMA unaofadhiliwa na Serikali ya Norway juu ya matumizi ya gesi. Mhe. Spika, mimi naunga mkono sana juu ya jambo hili kwa sababu ni kweli matumizi ya kuni na mkaa yanamaliza misitu yetu hasa sisi ambao maeneo yetu ni ya ardhi kame hatuna misitu mikubwa kule kwa hiyo inatubidi tufate kwenye misitu mengine kwenda kukata kuni. Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri mradi huu akausogeza kwenye maeneo ambayo yako kame kama majimbo yetu sisi hayana miti mikubwa, hivyo akausogeza mradi huu ili wananchi wetu wakaweza kufundishwa na kujua juu ya matumizi ya gesi na umuhimu yake na hatari ya kukata miti.

Mhe. Spika, mimi jimboni kwangu nina wananchi ambao mara nyingi sana hasa kipindi kama hiki cha kukaribia mwezi wa Ramadhani inabidi watoke pale Mkwajuni waende Kiwengwa kwenda kutafuta kuni. Lakini kama mradi huu utausogeza pale kwenye Jimbo la Mkwajuni basi utawasaidia wale wananchi wa pale. Mhe. Spika, kwanza kule kutoka kwao kwenda Kiwengwa kutafuta kuni inakuwa ni tabu, na hizo kuni zenyewe kupata ruhusa ya kukata ni shida. Kwa hivyo, mradi huu kama utausogeza pale basi utawasaidia wananchi hawa na mara nyingi sana nina hakika watakuwa wanaelewa na wataanza kutumia gesi badala ya kutumia kuni na mkaa. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri uyasaidie yale maeneo ambayo hata ule upatikanaji wake wa kuni basi uisogeze mradi huo ili waweze kuelewa matumizi ya gesi na waweze kufaidika na mradi huo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa changamoto za wizara ambazo amezionesha kwenye ukurasa wa 67, mimi niiguse tu changamoto moja ambayo inamkabili Mhe. Waziri ameisema hapa kwamba uvamizi wa maeneo ya kilimo na misitu unamsumbua sana. Mhe. Spika, mimi naamini ni kweli hilo suala lipo, lakini mimi nilikuwa nataka kujua tu je wizara yako Mhe. Waziri imejipanga vipi juu ya jambo hili. Kwa sababu hili jambo lipo wanaovamia wapo, na wanaonekana na madhali wamevamia eneo maana yupo anaishi kabisa hivyo ni hatua gani sijui wizara yako inachukua juu ya wavamizi hawa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa haya ambayo ametuonesha kwenye kitabu hiki nimuombe tu isiwe maneno bali tunataka kwa vitendo. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri bajeti yako ya mwakani tukijaaliwa haya uliyotuongia hapa tuje tuyaone utekelezaji wake na sisi tuko tayari kukuunga mkono kwa bajeti hii mna mambo mawili matatu

nimeyazungumza basi mimi nakupa asilimia 75 na asilimia 25 ukimalizia hayo mimi sina tatizo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa angalau dakika hizi chache kuweza kutoa mchango wangu kuhusu mada iliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, awali ya yote naomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe kunipatia hii nafasi ya kuweza kutoa mawazo yangu machache sana katika hotuba hii. Pili, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri Mansour Yussuf Himid kwa kuweza kutuletea hii bajeti yake, kwa kweli wataalamu wake wamekitunga vizuri kitabu hiki na yeye ametuwasilishia vyema kwa hili nasema ahsante sana.

Mhe. Spika, sisi wa Pemba kuna usemi tunasema kwamba. “Mtoto hufuata kichogo cha mzazi wake”. Mhe. Spika, kwa mnasaba huu Mhe. Waziri katika kuleta maendeleo ya nchi hii amesibu sana kufuata kichogo cha mzazi wake Marehemu Brg. Yussuf Himid. Kwa hivyo, naipongeza sana kwa hili.

Mhe. Spika, nadhani nitakuwa mbaya wa shukurani kwamba sikutumia fursa hii kuwashukuruni nyinyi wawakilishi wa wananchi kwa kuweza kutumia muda wenu hata mwisho wa wiki kwa kuwatumikia wananchi. Mhe. Spika, mimi natumia fursa hii kuwapongeza sana kwa jambo hili.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hoja iliyopo mbele yetu, mimi nataka nianze katika ukurasa wa 5. Ni kweli Mhe. Spika, kwamba mpaka sasa hivi wa Zanzibar kwa asilimia kubwa tunategemea kilimo, tunategemea sana maisha yetu katika kilimo moja kwa moja au kwa kupinda kidogo. Mhe. Spika, sekta ya kilimo kwa mujibu wa Mhe. Waziri inachangia asilimia 32.8 ya pato la taifa, halafu inachangia asilimia 75 ya pato la fedha za kigeni nchini. Kwa kweli kilimo kina mchango mkubwa sana na zile enzi za nyuma kabisa tulikuwa tukiita uti wa mgongo wa taifa hili.

Mhe. Spika, lakini hadi leo hii kilimo hiki mkulima hasa bado hakijamsaidia sana kilimo hiki na vile vile inaonekana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya umoja wa kitaifa pamoja na mambo mengi waliyoeleza lakini rasilimali mtu katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo hakuangaliwa. Mhe. Spika, yaani huyu mkulima mmoja mmoja hakuangaliwa.

Mhe. Spika, tunamshukuru Mhe. Waziri pembejeo ameturemsha kwa kiasi kikubwa, tunashukuru ameturemsha mbolea ya kulimia na ya kupalilia, lakini yule mkulima mwenyewe amemuangalia vipi? Mhe. Waziri tunakwambia kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara wamemudu kuboresha zao la karafuu lakini vipi hakushirikiana na Wizara ya Fedha wakahakikisha kwamba mkulima

anapata nguvu za kulima kwani mapembe hayanunuliki. Mhe. Spika, kwa hiyo ikiwa mkulima hakushiba atalima vipi mkulima huyo.

Mhe. Spika, kama serikali imeweza kuboresha kwenye mambo haya ya mbolea na pembejeo kwa nini ishindwe kuboresha bei ya mapembe katika nchi hii ili watu wakaweza kula, wakashiba na wakaweza kulima. Mhe. Spika, mimi nadhani nina kilio kikubwa juu ya fedha kwa sababu ipo serikali nzima hapa hivyo waangalie kama tunataka kuleta Mapinduzi ya Kilimo kweli, basi lazima wakulima washibe.

Mhe. Spika, mkulima hawezi kumudu hata mahitaji yake ile siku moja, ndio kweli ataweza kulima jamani. Mhe. Spika, mchele kila kukicha unapanda tu, mimi nasema katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo ashirikiane na wenzake wa serikali, muone ni namna gani mnaweza mkawasaidia wakulima wa nchi hii ambao ni zaidi ya asilimia 70 *population density* ya nchi waweze kumudu maisha yao, ili waweze kununua mchele, sukari angalau na huo unga ili wapate nguvu za kulimia. Mhe. Spika, ni kweli mmeshawateremshia bei ya mbolea lakini hawana nguvu kwani hawashibi. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, halafu sisi watu wa Vitongoji tunalima sana, sehemu za Micheweni kwa Mhe. Subeit tunalima mazao ya maweni na unatakiwa ukifika msimu ulime, ikifika kuvuna uvune. Mhe. Spika, na ukishavuna pale pale uyauze huu utaratibu mliotuwekea ni mzuri wa kutusaidia katika harakati hizi kama Mhe. Waziri alitwambia kwamba atatuwekea vitu vya kuhifadhia mazao haya yaliyokuwa ni *seasonal*. Mhe. Spika, lakini tuko katika *transition stage* kutoka katika *stage* hii kuna kipindi hiki tunaelekea huko. Mhe. Spika, sisi wakulima wa tungule Vitongoji tunalazimika kuuza kwa bei ndogo sana na hatuwezi kuzihifadhi. Mhe. Spika, kwa hiyo kilimo hakijatusaidia sisi watu wa Vitongoji, na tungule ukiziweka kidogo zimeshaoza, hivyo tutazihifadhi vipi na njaa iko pale pale.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri angetusaidia sana katika kipindi hiki cha mpito kuhusiana na kufanya *dusting* kwa sababu sisi tunalima mahindi kwa mnasaba wa kwamba mahindi yale yatusaidie kula yetu angalau katika miezi sita au mwaka unaokuja, lakini ukishayavuna leo baada ya miezi mitatu ukenda yanatoka wadudu. Kwa hivyo, mimi naomba mtusaidie wakulima wanyonge hatuna uwezo wa kuya-store mazao yale yatakatusaidia hata miezi mitatu yanaharibika. Kwa hivyo, mimi naomba mtusaidie mambo ya *dusting* ili kupata zile *chemical* ambazo tutaweza kuyahifadhi mazao yetu ili tuweze kuyatumia kwa chakula katika kipindi kinachokuja. Mhe. Spika, jambo hilo vile vile naomba.

Mhe. Spika, sisi ni wakulima kwa sababu sisi kule kwetu mpunga hauwi hata mkiileta hiyo *NERICA* basi nakuhakikishia kweli mawe haioti tunategemea ule ule muhogo. Mhe. Spika, muhogo siku hizi ukiupanda leo baada ya muda majani yameshakunyaa hivyo tunashindwa ku-*control* juu ya mihogo hii jinsi inavyokuwa. Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri wataalamu wake watatusaidia nini ili wanyonge wakulima wa muhogo Vitongoji waweze kulima muhogo na wafanikiwe katika kilimo kile.

Mhe. Spika, mahindi pia huwa tunalima sana Vitongoji na huwa tunayapata kweli kweli sehemu za makaani kule, lakini Mhe. Waziri jambo la kusikitisha kunguni mgunda ni tatizo akiyakamata mahindi kunguni mgunda yameshanywea na hupati mazao. Kwa hivyo, mnatusaidia nini sisi wanyonge wa Vitongoji ili mkulima wa mahindi aweze kum-*control* huyo kunguni mgunda. Mhe. Spika, kwenye migomba kuna ile *sudden death* vile vile ni tatizo.

Mhe. Spika, sasa nije na hawa maafisa ugani pia ni changamoto katika kilimo cha kwetu sisi Vitongoji. Mhe. Spika, kama kuna wakulima wazuri wa migomba, mihogo, mahindi basi ni watu wa Jimbo la Wawi kwa maana ya Wawi wenyewe, Uwandani, Kibokoni na hiyo Vitongoji wenyewe wanalima sana. Lakini Mhe. Spika, wana tatizo la maafisa ugani hawawatembelei kwa vile wanakosa *technical advise*.

Mhe. Spika, nyinyi mnasema kwamba wachimba machanga wanaharibu mazingira, lakini kilimo bila ya kuwa na mawazo ya kitaalamu basi unaharibu mazingira. Mhe. Spika, kwa kina Mhe. Subeit wao wanafanya kitu kinaitwa *mono culture*, zao hilo hilo na ardhi hiyo hiyo miaka nenda na miaka rudi *mono culture* inaharibu ardhi. Mhe. Spika, hawajui chochote kuhusu mambo ya *crop rotation*, hawajui chochote kuhusu mambo ya *shifting cultivation* kama hamjaweza kuwapeleka maafisa ugani Micheweni basi ardhi itaendelea kusinyaa.

Mhe. Spika, kwa sababu *mono culture* ni utaratibu wa kupanda zao moja katika ardhi hiyo hiyo. Mhe. Spika, ardhi hiyo hiyo miaka nenda miaka rudi unapanda uwele tu mpaka ardhi inapoteza rutuba yake. Kwa hivyo, wanatakiwa wajue haya mambo ya *crop rotation* na nini mambo ya *shifting cultivation* wanataka wajue watu, hawajui watu wa Vitongoji na Micheweni hivyo wapelekeeni maafisa ugani. Mhe. Spika, nadhani maafisa ugani itakuwa ni wachache au wanakaa ofisini tu, kwa hiyo ikiwa wapo basi wapatiwe vipandio hawana hawa vipandio.

Mhe. Spika, mimi kwanza katika hili naishauri serikali mambo yafuatayo. Kwanza ni katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo lazima serikali ihakikishe



kwamba mitaala ya skuli za sekondari yote inakuwemo hii *Agricultural Science*. Pili, nyinyi tuliowakabidhi mamlaka hii ya kuendesha serikali musione kila liloanzishwa na waasisi kuwa ni baya nyinyi serikali nawaambia kuna mengine ni mazuri. Mhe. Spika, Al-hajj Aboud Jumbe Mwinyi alianzisha michepuo wa kilimo pale Fidel Castro ulikuwa unatoa wanafunzi vizuri sana, kwa nini leo mmeondosha mambo kama haya jamani. Mhe. Spika, sisi wana mapinduzi tunaumia sana katika hili kwani mambo mazuri kama haya mnayaondosha, inakuwaje jamani. Mhe. Spika, mimi nadhani watu wa serikali hawa wayaenzi yale mawazo ya waasisi wetu, wayathamini, wayatunze na vile vile wayalinde.

Chuo cha Kilimo kilipokuwepo Fiedel Castro pale vijana wengi walifanya vizuri wengine ni madaktari sasa hivi, Naibu Katibu Mkuu huyo hapo juu Juma Ali Juma ana *master* ya *Agricultural Science* katika *crow* ya *production*, kasoma pale pale. Kassim Omar Ali ana Phd kasoma pale pale, sasa mnadharau mambo kama haya vipi. Nadhani Balozzi angekuwepo hapa sasa hivi, lakini waziri katika ofisi hiyo yupo tunataka huu mchipuo wa kilimo urudi rasmi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nije kwenye Mashamba Darasa. Mashamba Darasa kuna darasa, muda umekuwa mdogo lakini mnapoweka ardhi sisi wawakilishi tunatakiwa tuangalie matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi pamoja na rasilimali ya nchi. Lile shamba la Mambo ya Mipira liko pale njia ya Wete limekaa tu, nataka maelezo Mhe. Waziri lile shamba lilioko Maziwani njia ya Wete nataka maelezo analo nani na linasaidia vipi upande wa serikali. Kwa sababu najua alipokuwepo Mzee Jumbe tulikuwa tukiua mpira kwa wingi.

**Mhr. Spika:** Mheshimiwa dakika zangu tano niachie.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru sana, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wazi zaidi ya elfu kumi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii muda huu, ilikuwa nisichangie hata suala moja mimi katika wizara hii lakini itakuwa sio mwingi wa fadhila kwa kazi aliyofanya Mhe. Waziri. Mhe. Waziri amefanya kazi moja nzito kabisa haki yake tumpe, nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kumteua kwake na wizara aliyompa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wizara aliyopewa ni ya kwenda kuwakomboa wa Zanzibari ambao ni wanyonge wa nchi hii hasa kwa suala la kilimo. Mhe. Spika, kazi aliyofanya Mhe. Waziri kwa muda mfupi tumeiona mwelekeo wake hii ni sifa yake Mhe. Waziri. Mhe. Spika, kipindi kifupi tu wizara tayari

imegeuka na imeelekea katika njia ambayo iliyokuwa sahihi kwenye Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Spika, mimi itakuwa sikuwafanyia haki wananchi wa Jimbo la Muyuni kama sikutetea suala la embe za Muyuni zimekuwa na mafunza kipindi kirefu, na hichi ndio nilichokisimamia sana hapa kwamba embe za Muyuni sasa hivi zimekuwa na matatizo makubwa hata sifa yake ya kuitwa boribo ya Muyuni imepotea kwa muda huu kutokana na wingi wa mafunza. Mhe. Spika, nilikuwa naiomba wizara hili suala waliangalie kwa makini kabisa ili kutatua tatizo hili kwa wananchi wetu kuhusu embe.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye mbegu za mahindi imekuwa ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni hasa Kitogani, Paje na Jambiani kuhusu mbegu za mahindi. Mhe. Spika, mbegu za mahindi zimekuwa na usumbufu kupita kiasi na zimekuwa hazikidhi mpaka kwenda kuzifuata Tanzania Bara.

Mhe. Spika, kuna kilio chengine cha Shirika la Sukari kuhusu yule mwekezaji ni kipindi kirefu wananchi wamelalamika na eneo lile hakuna anayeneemeka, wananchi wamekuwa wanapiga kelele na kama mwisho haiwezekani basi hawa wananchi wapewe sehemu ili waendeleze kilimo.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye matrekta ni kwamba Mhe. Waziri utakapokuja kuyapata matrekta uangalie kwenye *priority* ya mabonde ya mpunga yamekuwa ni kilio sana kwa wananchi wetu. Vile vile nikushukuru kwa kiwango kikubwa sana cha kushusha bei za mbegu pamoja na mbolea kwa *speed* kubwa sana umeshusha hata aliyekuwa si mkulima lazima itabidi alime kwa kazi uliyoifanya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba kama itawezekana kumpitishia vifungu hivi sasa Mhe. Waziri huku backbanchors tumekaa tayari kwa hotuba yake aliyoitoea kwenye kitabu hiki hata sisi hatuna ubishi nae kwa suala alilolifanya katika kitabu hiki. Mhe. Spika, kama sheria itaruhusu bila ya majumuisho basi tupitishie hotuba hii. Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

**Mhe. Spika:** Mhe. Jaku tunakushukuru sana kwa kutumia muda mfupi sana na kuwa na imani kubwa ya kumsaidia Mhe. Waziri kwamba tumpitishie tu moja kwa moja, lakini kuna wengine wameuliza masuala ya hapa na pale inafaa na wao wapate majibu Mwenyezi Mungu akipenda kesho. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kesho tujipange vizuri sana twende kwenye points zetu moja kwa moja maana kuna wachangiaji wasiopungua 16 ambao wanahitaji na wao watoe maneno mawili matatu kumsaidia Mhe. Waziri wetu.

Kwa hivyo, naomba tuje tutumie muda mfupi kwa sababu na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto tunataka hotuba yake angalau tuisome kesho ili Jumatatu tuweze kuendelea kuichangia hotuba hiyo ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii. Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni kwa mashirikiano makubwa na sasa naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 24/07/2011 saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 9:00 kamili Baraza liliakhirishwa hadi kesho tarehe 24/07/2011 saa 3:00 asubuhi)*